BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**

9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii,**
			na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi,**

			Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**

29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Uwezeshaji,**	**-**	**Naibu Waziri wa Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg.	**Raya Issa Msellem**	**-**	**Katibu**

Kikao cha Ishirini – Tarehe 05 Juni, 2018

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe katika kikao cha tarehe 28 Februari, 2018, iliyokuwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo iliulizwa swali la msingi nambari 60 na Mhe. Suleiman Sarahan Said, kuhusu mafanikio ya mashindano ya *CECAFA* na kutokana na swali hilo, Mhe. Suleiman Makame Ali aliuliza swali la nyongeza ambapo aliahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale asome majibu ya swali la nyongeza lililoulizwa na Mjumbe huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ambalo aliuliza Mhe. Suleiman Makame Ali na nikaahidi kulileta kwa njia ya maandishi.

Mhe. Naibu Spika, Mwaka 2014 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wizara ya Ardhi, Nishati, Maji na Mazingira iliandaa mpango wa matumizi ya Ardhi. Kupitia mpango huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga eneo la Wambaa Mkoa wa Kusini Pemba na eneo la Makangale Mkoa wa Kaskazini Pemba kuwa eneo tengefu la uwekezaji ikiwemo miradi ya kitalii. Lengo la Serikali ni kuvutia uwekezaji wa daraja la juu wenye tija kwa taifa na wananchi wote. Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 96

Ujenzi wa Nyumba Zilizosababisha Kuziba Mitaro

Mhe. Omar Seif Abeid– Aliuliza**:**

Kwa kuwa msimu wa mvua wa mwaka huu unategemewa kuwa na mvua kubwa kutokana na utabiri ambao ulitolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Zanzibar. Na kwa kuwa wapo wenzetu ambao wamejenga kwenye mitaro ambayo imejengwa toka zamani lakini kutokana na kuachwa kufanyiwa matengenezo na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, mitaro hiyo imeziba.

(a) Je, ni kwanini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ikashindwa kuiendeleza mitaro hiyo sambamba na kuzuia ujenzi ambao haufuati utaratibu wa mipango miji ambapo ramani ya mji wa Konde (*Master Plan*) ipo kabla ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

(b) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ina mpango gani wa kusimamia kikamilifu ujenzi pamoja na kuhakikisha wanawadhibiti wale wote waliovunja sheria za ujenzi na mipango miji wa Konde na kwengineko.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 96 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imeshachukuwa hatua za kuifufua na kuichimbuwa upya baadhi ya mitaro ambayo inaweza kuleta athari endapo kiwango cha mvua kinaweza kuwa kikubwa, miongoni mwa mitaro iliyofanyiwa marekebisho ni pamoja na mtaro uliopo Konde katika kituo cha magari. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni itaongeza usimamizi katika matumizi ya ardhi kwa kuzingatia *"Master Plan"* sambamba na kuongeza elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuzingatia mipango ya matumizi ya ardhi iliyowekwa Kisheria.

(b) Mhe. Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kushirikiana na Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi *Development Control Unit – DCU* itaendelea kusimamia utaratibu uliowekwa kwa kuhakikisha kwamba wananchi wanajenga nyumba zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni na mipango. Mhe. Naibu Spika, Halmashauri haitasita kuwachukulia hatua za Kisheria wale wote wanaokiuka taratibu hizo. Kwa sasa zipo kesi tatu za wananchi waliojenga kinyume na utaratibu zinaendelea kusikilizwa Mahakamani.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naamini kwamba amefika katika eneo na ameliona. Lakini naomba kumuuliza swali kwa kuwa huo mtaro alioulizungumza kama umejengwa ni ulipo *stand* ambao ulifufuliwa juzi tu wakati wa ujenzi wa barabara mpya. Lakini ipo mitaro ya ndani ambayo imezibwa wananchi wameipandia migomba na mingine wameijengea na Halmashauri inajua hilo, nilitaka nijue.

(a) Je, kwa wale ambao wameshafanya hivyo, Halmashauri inachukuwa hatua gani kuhakikisha kwamba itaifufua na ile mitaro iliyopo ndani ukiachilia mbali ule wa nje aliousema.

(b) Kwa kuwa wapo watu ambao wamejenga kwenye maeneo tengefu ambayo yaliwekwa kwa ajili ya matumizi ya mji wa Konde na Halmashauri pia inafahamu hilo.

Je, ni hatua gani ilizowachukuliwa watu wale ambao wamejenga na wameiharibu ile *Master Plan* ya mji wa Konde na hali Halmashauri wanajua. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba katika swali la Mheshimiwa ambalo ameliuliza ni swali ambalo tumeshalitolea ufafanuzi mara nyingi na hata katika Mkutano huu wa Bajeti tulijitahidi sana katika kutoa ufafanuzi.

Lakini kwa faida na kwa majibu ya ziada naomba niwambie Mhe. Mwakilishi kwamba tatizo la wananchi kujenga katika maeneo ambayo yasiyoruhusiwa ni jambo ambalo kwa kweli tunakiri kwamba lipo na sio maeneo ya Konde tu liko katika maeneo mengine.

Kubwa zaidi katika Halmashauri zetu za Manispaa zetu tunaendelea na utaratibu na tumeongeza wigo mpana zaidi katika kushirikiana na hizi Kamati ambazo tumezitaja za *DCU* kwa namna bora ya kufanyakazi katika kuhakikisha kwamba jambo hili haliendelei tena kama ambavyo limekuwa likiendelea huko nyuma ambalo sasa hivi linaendelea kutupa tabu katika mjini yetu ya Unguja na Pemba.

Kubwa zaidi kwa kuwa wananchi wetu wamekuwa na utaratibu mbaya ambao unatupelekea kupata hasara za mara kwa mara niwaombe sana kupitia kikao chako hichi Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa watusaidie kwa kuwa Zanzibar ni yetu sote basi wahakikishe kwamba tunatoa mashirikiano kwa kila mmoja wetu tuhakikishe kwamba wananchi wetu hawavunji sheria yale maeneo yaliyotengwa na serikali waweze kuyathamini na hatimaye wafanye kwa mujibu wa sheria zinavyoelekeza ili kuepusha lawama na kufuatana kwenye maofisi kwa kuwaombea wananchi ambao wanakuwa wanavunja utaribu kwa visingizio mbali mbali. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuuliza swali ya nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza swali naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa na kwa kweli tumefahamu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Waziri katika barabara iliyojengwa kutoka Kojifa kuelekea bandarini Tumbe ikajengwa na *MIVAP* haikuzingatia uwekaji wa mitaro. Hivyo, basi imesababisha wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe ambao wana nyumba zao zilizopo karibu ya barabara ile kufikia kipindi cha mvua nyingi za masika kutawama maji na nyumba hizo kuharibika.

Je, wizara yako ina mpango gani wa barabara ile kuiwekea mitaro ili wananchi wale wasiathirike nyumba zao siku hadi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ni kweli hivi karibuni tumeshakabidhiana

miradi yote ambayo imejengwa imetekelezwa na mradi wa *MIVAP* ikiwemo hizo barabara na moja katika jambo ambalo tunajua sasa hivi ni kwamba ziko barabara ambazo tunakabidhiwa lakini tayari zinakuwa tayari zishaharibika na zinahitaji matengenezo makubwa na nyengine ambazo zinahitaji matengenezo madogo.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi sio barabara ya Tumbe pekee lakini katika wizara yetu tumepanga kwamba baada ya kumalizika kipindi hichi cha bajeti basi tutahakikisha kwamba tunapita katika barabara zote ambazo tumekabidhiwa ili kujionea hali halisi ilivyo baadae tukafanye utaratibu wa namna gani wa kuziendeleza kwa sababu sasa hivi tumeshapewa kama ni jukumu letu. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi tutafika Tumbe na tutafika maeneo mengine ili kuona wananchi kama barabara azma ya serikali ilivyojenga basi tuone kwamba hazileti usumbufu na baada yake zinawaletea maendeleo kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambavyo imekusudia. Ahsante.

Nam. 150

Malipo ya Nauli kwa Mashahidi katika Kesi Pemba

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza**:**

Kumekuwa na malalamiko kwa Mahakama Pemba mashahidi wanapofika kwenye kesi zinaahirishwa wakati mashahidi wameshafika na wameshatumia nauli ya shilingi 600/= kwenda na kurudi, wanapoitwa siku ya pili hawaji kwa vile nauli zao hawalipwi.

(a) Je, Mahakama Pemba hawapatiwi fungu la fedha kwa ajili ya kuwalipa mashahidi.

(b) Je, kitendo cha kutowalipa nauli mashahidi na wakiwa hawaji mahakamani hatuoni kuwa tunacheleweshe mwenendo wa kesi na kuwakosesha watu haki zao na kwa kuwa haki inayocheleweshe ni sawa na kutotolewa kabisa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 150 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Mahakama Pemba inapata fedha za kuendeshea kazi zake za kawaida (*OC*) kutoka serikalini, lakini fedha zinazopatikana hazikidhi kulipa malipo yote. Hivyo, mashahidi wanalipwa kutokana na fedha hizo wanazopewa serikalini. Hakuna fungu maalum linalopelekwa Mahkama Pemba kwa kuwalipa mashahidi isipokuwa mashahidi hulipwa kutokana na mgawanyo wa fedha zote za *OC* zinazopelekwa huko.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida shahidi hulipwa fedha mara tu anapotoa ushahidi Mahakamani. Baadhi ya wakati shahidi hutoa ushahidi na kushindwa kulipwa posho lake kutokana na upungufu wa fedha. Hata hivyo, inapotokea shahidi kutokulipwa fedha zake

kwa siku ile Mahakama bado inakuwa na deni ambalo hulipwa pale fedha zinapopatikana.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema ikafahamika kwamba kitendo cha kutowalipa nauli mashahidi sio pekee kinachochelewesha mwenendo wa kesi na kuwakosesha watu haki zao, bali kuna mambo mbali mbali kama vile kutokamilika kwa upelelezi ambao unafanywa na Jeshi la Polisi, utoro wa washtakiwa, miundo mbinu isiyokidhi shughuli za Mahakama, dharura mbali mbali kwa Mahakimu, Waendesha Mashtaka na wataalamu mbali mbali. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utawala Bora kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kilio kikubwa kwa wananchi kesi kuchelewa kutolewa ushahidi na kesi bila ya kutolewa ushahidi huwa haiendi na haipati jawabu yake.

Je, kwa kuwa mpango wa kuwalipa mashahidi ni sehemu moja ya kufika Mahakamani na kwa kuwa Mahakamani alifika kesi ikaakhirishwa, lakini siku ya pili hana taarifa ya kupata tena mafao ya kufika kule Mahakamani.

Haoni Mhe. Waziri tatizo hilo linasababisha kesi zetu kukaa kwa wingi katika Mahakama bila ya kufika ushahidi na kukosekana kutolewa uamuzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali (shihata) Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kwamba pamoja na suala la kutolipwa fedha kwa wakati hao mashahidi na kutohudhuria katika Mahakama sio suala pekee ambalo linaweza kukwamishwa suala hili zima la kupatikana kwa hati, nikatoa maelezo mbali mbali yanayohusiana na suala hilo kama vile wakati mwengine ukosefu wa madaktari kwa maana ya kwamba pengine wale mashahidi wengine madaktari kutokuja vile vile au kuakhirishwa kwa kesi mara kwa mara.

Lakini nikiri kwamba wanapokuwa mashahidi hawafiki Mahakamani bila shaka mwenendo wa kesi utakuwa hauendi vizuri. Sasa ni vyema na tunafanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba hawa mashahidi mara zote wanapokuja Mahakamani wanalipwa fedha zao. Fedha huwa tunawalipa kulingana na ile sehemu ambayo wanayotoka, hatuwezi kuweka *rate* moja kwa maana ya kwamba kwa mfano mia mbili, mia mbili hizo pengine mtu anaweza akatoka Wete mpaka Chake au mwengine anaweza akatoka pale Chake Chake hatuwezi kuwapa wote *rate* moja.

Kwa hivyo, tunazingatia hili ili kutia mkazo zaidi mashahidi tunawapa fedha kulingana na lile eneo ambalo wanalotoka. Tunawapa nauli na vile vile tunawapa posho. Kwa hivyo, hilo tunajitahidi kuhakikisha kwamba fedha zinapoingia mashahidi tunawapa

fedha zao kama kawaida na ukweli ulivyo sio mara nyingi kwa maana ya kwamba mashahidi wanakuja Mahakamani na huwa hawapewi fedha hapana inatokezea mara moja moja. Lakini mahudhurio yanaonesha kwamba mara nyingi mashahidi wanapokuja Mahkamani wanapewa fedha zao bila ya kucheleweshwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na mimi kuweza kupata kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake, lakini mimi nina swali dogo tu la nyongeza.

Katika majibu yake mama hapa katwambia kwamba kitendo cha kutolipwa nauli kwa mashahidi sio pekee kinachopelekea mwenendo mzima wa kucheleshwa kwa kesi. Lakini pia kasema kwamba kutokamilika kwa upelelezi ambao unafanyika na Jeshi la Polisi hicho kinapelekea kucheleweshwa kwa hizo kesi.

Je, kama ni Jeshi la Polisi na ndio wana haki zote za kufanya huo upelelezo mpaka kuhakikisha kwamba hii kesi imekamilika na upelelezi umekamilika. Ni sababu gani zinazosababisha kwamba wao washindwe kufanya huu upelelezi mpaka kuhakikisha kwamba hii kesi imekamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika majibu yangu mama nilisema pamoja na mambo mengine upelelezi vile vile unapelekea kutofikia muafaka katika hizo kesi. Niseme kwamba kuna mazingira mbali mbali ambayo upelelezi huwa Jeshi la Polisi wanashindwa kupata.

Pamoja na mambo mengine ni ushiriki mzuri wa wananchi wakati mwengine Jeshi la Polisi linakwenda katika sehemu husika lakini wananchi hao hao ndio ambao huwa wanakataa kutoa ushirikiano wa Jeshi la Polisi. Sasa katika mazingira kama haya upelelezi bila shaka unaweza ukakawia. Sasa hio ni miongoni tu mwa sababu ambazo upelelezi unakawia. Ahsante.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla sijauliza swali la nyongeza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ametupatia ambayo ameyatolea ufafanuzi nzuri tu. Lakini Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri alieleza miongoni mwa sababu zinazopelekea ucheleweshwaji wa kesi ni miundombinu isiyokidhi shughuli za mahkama.

Je, naomba nimuulize Mhe.Naibu Waziri au ni nimuombe atueleze ni miundombinu gani hiyo ambayo haikidhi shughuli za mahkama na kwa nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Mwantatu suala la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika ni kweli baadhi ya mambo ambayo huwa wakati mwengine yanacheleweshwa usikilizaji wa kesi ni miundombinu, miundombinu hii ikiwemo wakati mwengine inawezakana pengine chumba kimoja ambacho hakimu anasikiliza kesi hicho hicho wakati mwengine kinatumika na hakimu mwengine lakini kwa sasa hivi suala hili *Alhamdulilah* tumepiga hatua kubwa sana majaji wengi au mahakimu wengi kila mtu ana chumba chake cha kuendesha kesi kwa hivyo, suala hili mwisho wake umefikia na kwa maana hii si sababu kubwa ambayo inapelekea suala hili tayari mambo mengi yameshakaa sawa na kila hakimu au jaji ana chumba chake cha kuendeshea kesi.

Nam. 58

Ukosefu wa Huduma za Utoaji fedha katika Mashine za ATM

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:

Tunaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha mfumo wa utoaji wa fedha kwa mashine za kielektroniki (ATM) kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa urahisi kwa wananchi. Licha ya majibu yanayotolewa mara kwa mara na Wizara husika hata hivyo, bado huduma hiyo inakumbwa na changamoto kadhaa ikiwemo kukosekana kwa mtandao pamoja na kumalizika fedha katika mashine hizo.

(a) Kwa nini katika mashine zetu za utoaji wa fedha (ATM) hutokezea usumbufu wa ukosefu wa fedha mara kwa mara.

(b) Je, ni sababu zipi zinazopelekea mashine hizo kuharibika mara kwa mara.

(c) Je, Wizara imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali namba 58 la Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa viti maalum wanawake lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Si sahihi kuwa kuna usumbufu wa mashine zetu za utoaji fedha (ATM) kutokana na ukosefu wa fedha mara kwa mara. Uzoefu unaonesha kuwa kwa siku za kawaida, mashine zetu hubaki na fedha kwa takriban siku tatu. Aidha, kwa siku za mwisho wa mwezi benki huweka fedha mara mbili kwa kila siku. Tatizo ni pale fedha zinapomalizika wakati wa usiku ambapo utaratibu hauruhusu kuingiza fedha nje ya muda wa saa za kazi.

(b) Hakuna taarifa ya mashine za ATM kuharibika mara kwa mara. ATM zote ni nzima isipokuwa ATM mbili ambazo zipo katika eneo la Darajani, ATM hizo moja ina tatizo la mdomo wa kutolea fedha na mafundi wako mbioni kufanya marekebisho lakini na ATM nyengine hapo Darajani ilikuwa na tatizo la *setting*

configuration na tayari PBZ imeshawasiliana na na *vender* kwa ajili ya marekebisho hayo.

(c) Wizara kupitia PBZ itaendelea kufuatilia ufanyaji kazi wa mashine zote ili kuhakikisha kuendelea kupatikana ufanisi wa huduma hiyo muhimu. Matarajio ni kuwa ufanisi zaidi utapatikana mara baada ya kukamilika uwekaji wa mfumo mpya wa benki (*Core Banking System)* ambapo uwekaji wake umefikia hatua kubwa na unatarajiwa kuzinduliwa ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2018/19.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Kama kweli hizo mashine zinafanya kazi ipasavyo sasa mnachukua juhudi ya kuweka mfumo mpya ili tupate kitu gani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Suala la kuwa mashine zinafanya kazi ni suala la kuwa na mufumo mpya ni viti viwili tafauti, mashine tulizo nazo ATM tuna idadi ya ATM 31. Unguja tuna ATM 23, Pemba tuna ATM 4 na Tanzania Bara 4 hizo hazijatosha bado na kuna uwezekano wa kuziongeza zaidi.

Lakini la pili kuweka mfumo mpya yaani *Core Banking System* kunatokana kwamba idadi ya yawateja wa PBZ imeongezeka. Idadi tuliyokuwa nayo kule nyuma na idadi ambayo tunayo na tunatarajia kuwa nayo inalazimisha tuwe na mfumo mpya wa *Core Banking System.*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza suala dogo la nyongeza, Mhe. Naibu Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nikubaliane nae kwamba PBZ ina wateja wengi lakini vile vile niwapongeze sana Shirika hili kwa kuboresha huduma hizi ili kuhakikisha kwamba wateja wao wanapata huduma masaa 24. Mhe. Waziri, Wesha ni miongoni mwa Jimbo langu na Wesha kuna *population* kubwa ya watu hususan kule bandarini na ukizingatia kuna hoteli ile Misali je Wizara yako ina mpango gani kupia PBZ kuweka ATM kule ili kuwaondesha usumbufu wananchi wangu walikuwa maeneo ya Wesha na Ndagoni.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Makame Ali Swali kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba tuna ATM 31 na naamini kutokana na kukua kwa uchumi mahitaji ya ATM hizi katika maeneo mbali mbali yatakuwepo na yataongezeka, hivi sasa pale Chake Chake tuna ATM mbili eneo la Chake Chake na PBZ ina mpango wa kuongeza ATM katika eneo la Machomane, Micheweni, na Konde kwa upande wa Pemba. Sasa kwa vile mahitaji yapo katika eneo la Wesha hilo nalo ombi tumelisikia kadri ya hali itakavyowezekena basi na eneo hilo litazingatiwa vile vile.

Nam. 95

Ukosefu wa Mashirikiano baina ya Walimu, Kamati za Skuli na Wanafunzi katika baadhi ya Skuli

Mhe. Bahati Khamis Kombo – Aliuliza:

Pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuimarisha mwenendo mzima wa elimu pamoja na kuajiri walimu wenye sifa na viwango vinavyohitajika, kumekuwa na tatizo la kutokuwepo kwa mashirikiano kwa baadhi ya walimu na wanafunzi na skuli baina ya walimu, Kamati za skuli na wanafunzi.

(a) Je, Wizara inafahamu uwepo wa tatizo hili.

(b) Na kama inalifahamu Wizara imechukua hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo Mwakilishi wa Jimbo la Chambani swali lake Nam. 95 lenye vifungu (a) na (b), kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Kifungu Namba 25 cha Sheria ya Elimu Namba 6 ya mwaka 1982, kimeweka wazi majukumu ya Kamati za Skuli. Miongoni mwa majukumu yake ni kumshauri Mwalimu Mkuu katika uendeshaji wa skuli, kujenga mahusiano mazuri baina ya wanafunzi na walimu na jamii kwa jumla na kuhamasisha jamii katika kujitolea kwa maendeleo ya skuli na kwa jamii kwa jumla. Katika maeneo mengi, Kamati za skuli zimechangia sana katika uhamasishaji wa wananchi kujitolea, uandikishaji wa wanafunzi wapya na imejenga mahusiano mazuri baina ya walimu na wanafunzi na wanajamii kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Wizara haina taarifa rasmi ya kutokuwepo kwa ushirikiano baina ya walimu na wanafunzi na baina ya walimu, Kamati za skuli na wanafunzi wenyewe.

(b) Kwa vile suala hilo halijaripotiwa, Wizara haijachukua hatua yoyote. Hata hivyo, katika baadhi ya skuli kumejitokeza Wajumbe wa Kamati kutoelewa ipasavyo baadhi ya majukumu yake na kupitisha maamuzi ambayo yanaingiliana na majukumu ya vyombo vyengine. Matatizo kama hayo yanapotokezea, Wizara huchukua jukumu la kuandaa kikao cha pamoja ili kufahamishana mgawanyo wa majukumu baina ya vyombo mbali mbali. Wizara inazipongeza Kamati za skuli kwa mchango mkubwa unaozitoa katika maendeleo ya skuli na itaendelea kuzishirikisha katika kuleta maendeleo ya skuli zao.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsnte sana Mhe. Naibu Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri, naomba kumuuliza swali moja nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri katika miongoni mwa skuli ambazo zilikuwa na kamati nzuri ni skuli ya Ukutini na ilikaa pamoja na walimu wakaweza kushirikiana na ikajengwa skuli kwa muda mfupi sana, lakini Mhe. Waziri kama ulivyoeleza katika swali lako mama kama tatizo hili bado halijaripotiwa Mhe. Waziri tatizo hili limezungumzwa na mwenyewe katika chombo cha habari kipindi cha mawiyo kwamba hapati mashirikiano baina ya wazee na walimu na yanakwamisha maendeleo ya skuli ile.

Je! Mhe. Waziri utawaunganisha vipi wananchi hawa ili waweze kupata mashirikiano na mwalimu mkuu ili maendeleo yaweze kurudi kama muda waliokuwa nao huko nyuma. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako na kwaniaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na mafunzo ya Amali napenda nimjibu Mhe. Bahati swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hatuna taarifa na kwa kuwa unatupa taarifa hizo sasa, viongozi wa wizara kama kawaida yake itakutana na kamati ya skuli uliyoitaja, lakini pia itakutana na walimu itakutana na wazazi ili kujadiliana kwa kina nini tatizo. Lakini bado tunaendelea kusema kwamba tatizo ni baadhi ya wajumbe kutoelewa ipasavyo majukumu. Kwa hivyo, wizara itachukua nafasi yake ya kumuelewesha kila mmoja ana jukumu gani na kila mmoja ana kazi gani na tunatarajia wananchi wataunganika tena ili kuleta maendeleo ya skuli na eneo kwa jumla ahsante sana.

Mhe. Masoud Abrahaman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu vizuri swali lake. Mhe. kamati katika ziara kwenye Mkoa wa Mjini Magharibi, kamati ya Ustawi wa Jamii tulishuhudia mwanafunzi akitoa kauli zilizokuwa sio nzuri mbele ya walimu, wanafunzi, pamoja na kamati ya kuwasema walimu wake ni wambea na viongozi wa wizara walikuwepo.

a) Je! ni hatua gani wizara ilichukua juu ya mwanafunzi yule.

b) Wanafunzi wa ukanda wa pwani katika ziara yetu hiyo walituambia kuwa wao hawapendi kusoma isipokwa wanalazimishwa na wazazi wao kwenda skuli. Je, ni hatua gani wizara ilichukua ya kuhakikisha wanafunzi wake wanamaliza elimu ya lazima.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na mafunzo ya Amali, napenda kumjibu Mhe. Masoud Mwakilishi wa Jimbo la Bububu maswali yake kama ifuatavyo:-

a) Ni kwamba katika swali la awali ambalo mwanafunzi alitoa kauli mbaya, ni kwamba kuna muongozo wa wizara unaoelekeza namna ya kutoa adhabu kwa mwanafunzi ambaye amekosea. Kwa hivyo mwanafunzi huyu itakuwa amepewa adhabu kwa mujibu wa muongozo wa kutoa adhabu kwa mwanafunzi, utoaji wa adhabu katika Wizara ya Elimu inadhibitiwa si kwamba kila mwalimu anafanya

atakavyo na kadhalika kuna taratibu zake, kwa hivyo nadhani taratibu hizo zimefuatwa katika kutoa adhabu kwa wanafunzi.

Adhabu hizi zinaendelea kutolewa kwa wanafunzi mbali mbali ambao wanafanya vitendo vya utovu wa nidhamu na utovu wa adabu katika maskuli.

b) Tunakubaliana kwamba baadhi ya maeneo mwamko wa wanafunzi juu ya elimu ni mdogo. Sasa wizara inafanya kazi hiyo ya kutoa mwamko wa elimu kwa vijana hawa ili hatimae waone umuhimu wa elimu na kujiunga katika skuli. Na tunafanya hivyo kwa mashirikiano na kamati zenyewe za skuli, wazazi, masheha na viongozi wengine wa wilaya ili kuona kwamba jambo hili tunalifanikisha. Lakini pia tumekwenda mbali zaidi kwa kutoa mafunzo na maelekezo kwa walimu wa madrasa (walimu wa vyuoni). Ahsante sana.

Nam. 70

Wafanyakazi Wanaokimbia Baada ya Kumaliza Masomo

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Kny Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Hivi karibuni wakati akizungumza na watendaji wa sekta ya Afya , Mheshimiwa Waziri alisema kuwa wapo wafanyakazi wanaotumia fedha nyingi masomoni ambapo wanamaliza hawarudi tena.

(a) Hatua gani zinachukuliwa kuwatafuta wahusika.

(b) Wangapi wamepatikana na kadhia hiyo na hatua gani zimechuliwa dhidi yao.

Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako na napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi Jaku Hashim Ayoub mwakilishi wa jimbo la Paje swali lake Nam. 70 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe.Naibu Spika, ni kweli kwamba wizara ya afya ilikumbwa na tatizo la wafanyakazi wake kuomba kwenda masomoni na mara wamalizapo masomo wengi wao huwa wanachelewa sana kurudi kazini na wengine kutokurudi kabisa. Wizara baada ya kuliona tatizo hilo ilichukua hatua za haraka kwa kuwaandikia barua za wito wafanyakazi hao mmoja mmoja ikiwa sambamba kuwaita kwa kuwatangazia katika vyombo vya habari kuripoti wizarani mara moja. Kwa hatua hiyo wapo walioitikia wito na kuripoti wizarani, na kwa wale ambao hawakujali wito huo, Wizara ilichukua hatua nyengine ya kutoipitisha ya mishahara yao benki kitendo hichi Mhe. Naibu Spika, kilitusaidia sana kwani kila aliyekosa mshahara benki aliripoti wizarani haraka sana na wizara iliufata kanuni za utumishi kuwaeka sawa wafanyakazi hao na katika maadili ya kiutumishi.

b) Jumla ya wafanyakazi waliopaswa kurudi masomoni kwa mwaka 2016/17 waliotakiwa kurudi walikuwa ni mia moja na kumi na nne (114), wafanyakazi waliorudi kwa wakati walikuwa ni arobaini (40) tu. Baada ya wizara kuchukua hatua hizo nilizozieleza, wafanyakazi wengine sabiini na nne (74) walirudi wakewemo wafanyakazi wawili waliofeli na wawili walirudia mwaka yaani *Supplementary* .

Mhe. Ali Suleiman Shihata: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa afya kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, hakuna jambo zuri katika maisha ya binadamu kuliko nidhamu, na nidhamu popote ulipo unatakiwa uiheshimu na hasa katika sehemu zako za jamii na sehemu yako ya kazi.

a) kwa kuwa wafanyakazi hao walichelewa kurudi katika sehemu zao za kazi, ni sababu gani za msingi walizotoa ili wizara ikaridhika.

b) Baada ya wafanyazi hao kupewa onyo kali katika hatua za utekelezaji katika kazi zao ufanisi wao umeonekana unatosha au bado pana wasiwasi.

Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Afya: Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Shihata kwa niaba ya Mhe. Jaku swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika: hili kaliuliza Mhe. Ali Suleiman Shihata sio Mhe. Jaku.

Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Afya: Ok Naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Shihata swali lake la nyongeza kama lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida binadamu akishakufanya kosa na akijua kwamba wakati wowote atadhibitiwa kutokana na kosa alilolifanya hakosi vishingizo na sababu za kukuambia ili uridhike na kosa lake na yeye afanye lile ambalo alikusudia, hivyo wafanyakazi hao walitoa sababu mbali mbali lakini kwa wizara nyingi zilikuwa si sababu za msingi, kwa sababu kawaida ya mfanyakazi au mwanafunzi anapokwenda kusoma akirudi kwa njia yoyote kwanza aripoti kwenye kituo chake baadae kama kuna sababu au kuna tatizo lolote aeleze kwenye kituo baadae aende kwenye shughuli ambayo ameomba kwa kukubaliwa na ofisi. Kwa hivyo, sababu zote walizozieleza kwa wizara hazikuwa ni sababu za msingi.

b) Kwa sasa ufanisi wao katika kazi ni mzuri na wengine wamo katika hatua ya kuangaliwa zaidi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukafika hapa salama salmini. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa serikali kwa nia safi imempeleka mtu yule katika masomo na pia ni muda mrefu watu wanamsubiri ili amalize masomo yake na kurudi, lakini baadae yeye kama

yeye ndio anavunja mstari ambao unaiweka serikali katika kupoteza pesa hizi, zikijulikana pesa zile ni za serikali au za walipa kodi.

(a) Je, pesa zile kama mtu yule hakurudi zinarudi au inakuwa baada ya masuala yako ya kusema kwamba anatiwa adabu tu ndio zinaendelea, au yeye anarudisha zile pesa hiyo adhabu nyengine inabakia baadae.

(b) Ni hatua gani zinazochukuliwa ili wengine wasijaribu kufanya kitendo kama kile. Inaonesha hicho ni kitendo kama cha rushwa au cha kufanya vitu ambavyo havipendezi katika nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake, swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, pesa zile zinarudi wizarani. Yeyote ambaye atakutwa na hatia hiyo ya kuchukua mshahara na huku hakuufanyia kazi, basi hatua zinazofuata ni kurudisha mshahara ule na wapo ambao wamesharudisha mshahara. Wengine wameamua kuacha kazi, wengine wamerudi ofisini, lakini wamerudisha mshahara wa serikali.

Hatua nyengine ambazo tulizozichukua kuwadhibiti wafanyakazi wengine wasiendelee na kadhia au utovu wa heshima ule. Mhe. Naibu Spika, tumeendelea kuwapa elimu na kuwatahadharisha sana na kwamba likitokea kwa mfanyakazi mwengine yeyote, basi hatua za kisheria ambazo zimo ndani ya kanuni ya utumishi zitatumika haraka iwezekanavyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nafikiri hakunifahamu kidogo nilivyomuuliza. Nilimuuliza suala la masomo waliyokwenda kusoma, zile fedha alizokwenda kusomea zinarudi kama vile wanavyokopa mikopo au inakuwaje, wakati yule hakuja kurudi pale pahala alipokusudiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Masoma aliyokwenda kusoma pesa zile wizara inalipa chuo alichokwenda kusoma, kwa hivyo sio rahisi chuo kukubali kuzirudisha kwetu pesa zile. Lakini pesa za mshahara ambazo tulikuwa tunamlipa wakati yuko masomoni zile zinarudi. Hata hivyo, tunalichukua hilo suala lako tuliangalie kama kwamba itatokea tena kesi kama hiyo tujuwe nini tutafanya kwa mashirikiano na chuo kile ambacho kenda kusoma.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba nitowe maelezo kidogo hapa, maana yake naona wajumbe wanaanza kufungua kanuni kutaka kunipigia kanuni. Mimi nikiwa huku nauona mwenendo mzima huko unavyokwenda, ukiwa huku unaona mengi sana huko. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wakati maswali yanaulizwa badala ya kutoa ruhusa ya maswali matatu basi natoa ruhusa ya maswali mawili na kwa sababu, nina wachangiaji 13 ambao wanataka wachangie leo na wizara hii tuimalize leo. Kwa hivyo, mimi hapa natumia busara kupunguza hili swali moja, ili tupate wakati, kwa sababu nitakuja tena kukerwa kutaka kila mmoja atataka na mimi nichangie nipe dakika tano, nitazitowa wapi.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, nawaombeni sana m-*cool down* twende hivyo na mimi huku natumia busara zangu, najua kanuni zinasema nini nafahamu vizuri sana, lakini naomba na mimi mniachie, mkiachie kiti ili kutumia busara. Ahsanteni sana. Tunaendelea. *(Makofi)*

Nam. 72

Uhaba wa Dawa Kitengo cha Moyo Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Mnamo tarehe 3/3/2018 Waziri wa Afya ameripotiwa na vyombo vya habari akikiri kuwa Kitengo cha Moyo cha Hospitali ya Mnazi Mmoja hakina vifaa wala dawa.

(a) Je, ni muda gani Kitengo hicho kimekuwa hakina dawa na vifaa hivyo.
(b) Je, hatua gani zimechukuliwa kukabiliana na ukosefu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ina baadhi tu ya vifaa vya uchunguzi wa maradhi ya moyo, lakini haina vifaa maalumu vya hali ya juu vya uchunguzi wa maradhi hayo ya upasuaji wa moyo. Wagonjwa wanaohitaji kufanyiwa operesheni za moyo hupelekwa India na Israel. Mara nyingi dawa wanazoandikwa kwa ajili ya wagonjwa hao kwenye hospitali wanazopelekwa huwa hazijasajiliwa nchini na kunakuwa na shida ya upatikanaji wake.

(b) Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa, Hospitali ya Mnazi Mmoja imetengeneza muongozo wa vifaa na dawa zinazohitajika kwa hospitali ya rufaa. Hii itasaidia kusajiliwa na kuwekwa kwenye orodha ya dawa muhimu yaani (*Essential Drug List*), dawa zote zinazohitajika kwenye hospitali ya rufaa, ikiwemo dawa za wagonjwa wa moyo. Orodha hiyo ndio inayotumika kufanya manunuzi ya dawa kwa hospitali zote. Wizara ina mpango wa kuanzisha kitengo kitakachoweza kufanya operesheni za moyo hapa hapa nchini hali itakaporuhusu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa muda mrefu ina marafiki wazuri na wa kudumu ndugu zetu wa China, lakini kwa upande mwengine pia tuna madaktari wazuri au uhusiano mzuri na Serikali ya Watu wa Cuba.

(a) Je, hivi serikali kwa kufikia leo gharama kubwa inayotumika kuwapeleka wagonjwa wetu Israel, kuwapeleka India ni kubwa kiasi, hawaoni kuna haja ya dharura

ya makusudi kuanzisha hicho kitengo kwa haraka cha kuwasomesha madaktari wetu hapa nchini ili tatizo hilo lituondoke.

(b) Kwa kuwa wenzetu wa Tanzania Bara hivi sasa wamepiga hatua kubwa sana katika mambo ya upasuaji wa kileo kabisa, hatuoni haja ya kwenda kujifunza hapo karibu kwa wenzetu au kuwachukua wataalamu hao kuja hapa, tutapunguza gharama za matumizi kuwapeleka watoto wetu Israel na India.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, tayari tunasomesha madaktari wetu nchini India kwa ajili ya kuja kuwasaidia wananchi wetu kwa matatizo haya ya moyo na mengine. Hivi sasa tuna daktari mmoja ambaye wakati wowote kuanzia sasa anaweza akamaliza masomo na akaripoti kazi ili kuweza kusaidia katika taifa lake.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia huwa tunapata maelewano ya pamoja au elimu ya pamoja na wenzetu walioko Bara, ili kuweza kuwa-*save* na kuwasaidia wagonjwa wetu hapa nchini. Mhe. Naibu Spika, hayo yote tunayafanya kwa sababu tuna maelewano mazuri nchi yetu na nchi mbali mbali katika dunia, kutokana na uongozi bora alionao Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona, lakini nikupe pole sana kwa leo kuumwa na shingo yako upande huu wetu huoni. Pamoja na majibu ya serikali mazuri yenye kutia moyo, naomba kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali ya rufaa, ina wataalamu bingwa wangapi wa moyo yaani *cardiologist.*

(b) Kwa kuwa hospitali ya Mnazi Mmoja imekuwa ikipiga hatua kubwa mara kwa mara hadi kuanzisha Kituo cha *neurosurgery* kimepata mafanikio makubwa serikali inatuambia nini katika kipindi cha muda mfupi upi kama miaka miwili mitatu tayari kitakuwa kimeanzisha kitengo cha moyo na kupata mashine zilizokuwa bora.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa, mwakilishi makini na mwenye busara swali lake la nyongeza (a). Swali la (b) nitamuomba arudie kutokana na mashine hapa kusumbua kidogo. Lakini naomba kwanza nipate nafasi nijibu swali (a).

(a) Mhe. Naibu Spika, hospitali ya Mnazi Mmoja katika kitengo hiki cha moyo sasa hivi tuna madaktari bingwa wanne. Nilisema katika jibu la nyongeza kwamba, wakati wowote kuanzia sasa tunategemea kumpokea daktari mwengine mmoja ili kuungana na wenzake katika kutoa huduma zilizo bora kwa wagonjwa wetu.

Mhe. Mjumbe, samahani sana naomba urudie swali (b)

Mhe. Mohamed Said Mohamed:

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hospitali ya Mnazi Mmoja na serikali kwa jumla imepata mafanikio makubwa sana katika kuendesha hospitali hiyo hadi kufikia kupata kitengo cha *neurosurgery* na kimepata mafanikio makubwa.

Je serikali ina mpango gani kwa sasa wa muda mfupi kuanzisha kitengo hicho cha moyo ili kupata mashine mpya na za kisasa kwa haraka zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa, swali lake la nyongeza (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, serikali ina mpango maalum mpango kabambe ambao unategemewa kufanikiwa kwa asilimia kubwa kwa kuanzisha kitengo hicho maalum kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. Lakini pia ina mpango na katika bajeti yetu imeeleza kwamba hununua vifaa mbali mbali, vikiwemo vifaa vya matibabu ya moyo.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba tukae katika hali ya kuridhika kwamba serikali inajipanga kila mpango kuhakikisha hospitali zake zote za serikali zinatoa huduma zilizo bora kwa wananchi wake. Kila litakalowezekana serikali italifanya ilimradi ihakikishe huduma bora zinapatikana. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa. Pili nimshukuru sana Mhe. Mohamed Said Dimwa kwa maswali yake. Lakini niseme tu kwamba upasuaji wa moyo kidogo ni operesheni nzito na inahitaji taaluma ya hali ya juu sana. Srikali katika kulitimiza hilo kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Israel ambao wanakuja kuwatibu watoto wetu hapa na kuwachukua, tumekubaliana watutengenezee programu ni namna gani na sisi tunaweza tukafikia hatua, kufikia ile Kikwete *Heart Institute* iliyoko Dar es Salaam. Hiyo programu wameanza kututengenezea, tunategemea katika kipindi cha kama miaka miwili au mitatu tutakuwa na vijana ambao wanaweza kufanya operesheni pamoja na vifaa ambavyo vinahitajika.

Nam. 92

Maji ya Kisima cha Konde kwa Mchina

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-
Kwa kuwa maji ya kisima cha Konde kwa Mchina hayafai kunywa kutokana na maji hayo kuwa na mabaki ya tope na kutu ambayo inasababishwa na uhalisia wa kisima pamoja na kuchelewa kusafisha kisima hicho, ambapo wananchi huyatumia maji hayo kwa kufulia na kazi nyengine tu.

(a) Je, ZAWA kupitia watalaamu wake wanalifahamu tatizo hilo la maji yanayotoka kwenye kisima hicho na kama wanalifahamu ni sababu gani hadi leo halijapatiwa ufumbuzi.

(b) Je, ZAWA ina mpango gani wa kukisafisha kisima hicho kila mara na ni gharama kiasi gani huhitajika kukisafisha kisima hicho ili kiweze kutoa maji safi ambayo hayatakuwa na athari kwa matumizi ya kunywa.

(c) Je, ni lini kwa mara ya mwisho ZAWA walikisafisha kisima hicho ikizingatiwa kwamba hadi leo bado hali ya maji yanayopatikana kwenye kisima hicho sio mazuri ukilinganisha na maji yanayo patikana kwenye visima vilivyochimbwa na watu binafsi majumbani mwao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Uwepo wa tope katika visima vya maji ni jambo la kawaida na hutegemeana na maumbile ya mwamba wa maji uliopo katika eneo la kisima husika. Kwa kiasi kikubwa, tope katika visima virefu vya maji hufanyika kutokana na mabadiliko ya madini ya chuma (*Ferrous Iron* kuwa *Ferric Iron*) yaliyomo katika mwamba wa maji baada ya kukutana na hewa ya *oxygen*. Kwa Pemba, mfano wa visima vyenye tabia hiyo vipo Tumbe, Junguni na sehemu nyengine.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, wataalamu wa ZAWA wanafahamu kwa mapana uwepo wa tope katika kisima cha Konde kwa Mchina. Tatizo hili halina ufumbuzi wa kudumu. Hata hivyo, ZAWA hulazimika kukisafisha kisima kila baada ya muda itakapogundua kwamba tope zimejirudia.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida, ZAWA hukisafisha kisima hicho kila baada ya mwaka mmoja. Gharama za kusafisha kisima zinatofautiana baina ya kisima kimoja na chengine. Kwa kisima cha Konde kwa Mchina, jumla ya wastani wa TZS 552,800 zinahitajika kukifanyia usafi.

(c) Mhe. Naibu Spika, kwa mara ya mwisho kisima hicho kilifanyiwa usafi tarehe 23/4/2018. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Lakini nakushukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako yenye muelekeo, lakini pia kwa ZAWA kutoa majibu ya kukisafisha kisima hiki baada ya kupata swali, huo ndio ukweli. Lakini pamoja na majibu mazuri, kwa kuwa maji yanayotokana na kisima hiki cha Konde kwa Mchina huchukua muda mfupi sana baada ya kukisafisha kujirejea kwenye hali yake ya kutoa maji kama yale, sio zaidi ya miezi

miwili hadi mitatu huwa tayari baada ya kukisafisha kimeshajirejea tena, jambo ambalo husababisha maji yale kuwa na rangi nyekundu kama mtu aliyekula pariki vile, jambo ambalo hata yale masinki na *washing basin* yakiwekwa na maji yale hubadilika rangi.

(a) Sasa kwa sababu ZAWA wanalifahamu hilo nilitaka nijuwe, pamoja na kuwa wanalifahamu ni sababu gani inayopelekea kukaa mwaka mzima kabla ya kukisafisha na hali wanajua kwamba maji yanayotoka katika eneo lile yanatope na yana hiyo *rust* jambo ambalo linaweza kuleta madhara.

(b) Je, ZAWA Pemba wanajipangaje kuhakikisha kwamba wanachukua muda mfupi kuvisafisha visima hivyo cha Konde na vyengine vilivyotajwa ambavyo vinatatizo kama hilo, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata maji safi na salama sio tu bora kupata maji. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Lakini naomba nitofautiane naye kidogo kwamba ZAWA sio wamekwenda kusafisha baada ya swali, kwa sababu kabla ya tarehe hii 23/04/2018, tarehe 25/07/2017 wamesafisha. Sasa sio wamekwenda kusafisha kwa sababu ya swali, wamekwenda kusafisha kwa sababu ni wajibu na ni kazi yao.

Pia Mhe. Naibu Spika, niseme hii sio sumu ni hali ya maumbile ya eneo, lakini pia sio kama hayafai kunywa. Tumeona katika lile eneo ni *iron* inayosababisha kuweka rangi ile ambayo wananchi wana wasiwasi nayo, lakini ni masafi kwa kutumia, lakini rangi ndio inashughulisha.

(a) Kwa nini wanakaa muda mrefu. Sio kama wanakaa muda mrefu bali baada ya kugundua tayari zile tope zimejirudia, ndio tunaanza hizo harakati za kutafuta vifaa vya kusafishia, inawezekana ikawa mwaka lakini wastani ni huo inawezekana chini ya hapo pia. Lakini hatujabaini kama baada ya miezi miwili basi hizo tope ndio zimeshakuwa nyingi kama hivyo. Nadhani nimejibu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniona, kabla sijauliza swali langu la nyongeza, napenda nitowe shukrani zangu za dhati kwa serikali kwamba nimeanza kuona mashimo yanaanza kuzibwa katika barabara zetu, kwa hivyo nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe.Naibu Spika, niulize swali moja la nyongeza. Katika Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini na katika Jimbo letu au jimbo langu, ambalo ndilo ninaloliwakilisha hapa Barazani la Tunguu, katika maeneo masikini moja ni katika eneo la kisiwa cha Uzi, eneo la Kijiji cha N'gambwa. Moja tatizo, au changamoto walokuwanalo kwa muda mrefu ni kwamba, maji yao hata wakichimba kisima wanapata ya chumvi, na visima waliokua navyo au maji wanayotumia ni *system* ambayo pia ni ya kizamani. Sasa mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri, utachukua juhudi gani za binafsi, maana yake naamini bado utakuwa kama Uzi ushafika, ili uweze kwenda kuangalia wananchi hawa kutatua tatizo ambalo

walokua nalo la miaka nenda rudi, kuhusu changamoto ya maji walokua analo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusu yako naomba nimjibu Mhe. Simai Mohammed Said wa Jimbo la Tunguu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nadhani niliwahi kukujibu swali hili na nikakwambia kwamba katika maeneo maalum kama haya, ambayo maji yake hata ukichimba visima yanatoka chumvi, tunakuwa tunafikiria mpango maalum kwa kuyabadilisha maji ya chumvi kuwa maji ya kawaida, na tumefanya baadhi ya miradi katika maeneo mbali mbali. Sasa mimi nimuahidi kwamba tukimaliza mwezi Mtukufu wa Ramadhani yeye pamoja na wataalamu wetu wa *ZAWA* twende katika hilo eneo tukaone. Halafu nini cha kufanya tutashauriana huko kulingana na nguvu ambavyo itaruhusu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Makame Said Juma:

Mhe. Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata swali moja la kuuliza la nyongeza. Pia nimshukuru Naibu Waziri kwa kujibu masuala vizuri, lakini itabidi niulize suali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Waziri alikuwa akijibu swali mama alizungumzia sana katika suala ya maji haya ambayo hayako salama, mimi nasema hayako salama, kwa sababu yeye anasema yako salama. Lakini maji haya kila leo yanachafuka, chafuka na ni kweli yanaleta athari kwa jamii, maana yake mpaka kitu kikafika hakitumiwi ni athari. Sasa jee, na hasara hizi zinazoingia kwa kila muda kusafisha visima hivi. Jee, Serikali haijipangi kuchimba visima vyengine ambavyo vitakuwa na usalama zaidi ili kuondokana na tatizo hili la mara kwa mara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, si mara zote kwamba tatizo hukimbiwa, bali tatizo hutatuliwa na kwa vile maji haya tumesema ni salama kwa kunywa basi tutafute namna ya kuondosha wasiwasi kwa wananchi wetu na jambo ambalo tumefikiria baada ya nguvu kuruhusu basi tujenge matenki katika maeneo husika kama haya, kusudi yale maji yajichuje kwenye tenki na kule yende maji safi. Kwa sababu tishio la wananchi wetu ni kwamba baada ya kuweka kwenye ndoo yale maji wakiyaona yana rangi, lakini tukiweka kwenye tenki yali mabaki ya tope yatabaki kwenye tenki na maji safi yatakwenda kwa wananchi wetu nadhani hili tatizo litakuwa, ama wasiwasi wananchi kutakuwa umeisha. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe kabla ya kuendelea, nichukue fursa hii kuwakaribisha wageni wetu kwa leo ndani ya Baraza letu na wegeni wenyewe ni wa Mhe. Masoud Abrahaman Masoud, Mwakilishi wa Jimbo la Bububu. Wageni hawa wanatoka Tawi la CCM Mbuzini, na wageni hao ni:-

1. Ndugu John Mashauri Shija - Mwenyekiti
2. " Damiano Patric - Katibu wa Tawi
3. " Aziza Hassan - Katibu Mwenezi

Karibuni sana. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, Ahsante kwa kuniona, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nisimame kwa kanuni ya 42 fasiri ya 9, fasiri (d), kuomba tu hoja kidogo tu ya dharura lakini sitaki ijadiliwe. Sasa hoja ambayo nataka niizungumze kuhusu *ZBC* kukatika matangazo kama utaniruhusu naomba niendelee.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa endelea.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya mara kwa mara, aa, kituo chetu cha *ZBC* kukatisha matangazo ya moja kwa moja ya Baraza la Wawakilishi, na wakati mwingi kuna hoja maalum ambazo zinazungumzwa, lakini wanaweka kasida. Sasa hichi kitu kinatupa taswira mbaya na mbele na nilisema nililete jambo hili, sitaki nichukue muda wako lijadiliwe kutokana na kifungu kama nilivyo kizungumza. Lakini nilikuwa naitaka serikali itupe tamko kwa sababu Baraza tumekuwa tumekuwa tukiwalipa pesa nyingi na zinapotea visivyo pesa za wananchi. Sasa nilikuwa na tamko la serikali. Kwa nini *ZBC* inakatisha vipindi mara kwa mara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Serikali. Mhe. Mjumbe ameiomba serikali itoe tamko na kama serikali ina majibu basi naomba izungumze. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante. Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pili nimshukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae, na nimshukuru kwa kuona, kwa kuwa makini, kwa kuweza kubaini mapungufu ambayo yanajitokeza.

Mhe. Naibu Spika, kikawaida Baraza hili limekuwa likioneshwa *Live* kwa kipindi kirefu na kama kumejitokeza kasoro za kiufundi, lazima tukiri kwamba kasoro hizo sio dhamira ya serikali na Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuwa umelibaini hilo, sisi wajibu kama serikali kuwataka watendaji wetu na hasa wasimamizi wa chombo cha *ZBC* kuweza kuwa makini kujipanga vizuri, kuhakikisha kwamba timu zao za mafundi wanakuwepo

muda wote katika kufuatilia mtiririko mzima wa matukio. Isingependeza kwa namna moja au nyengine, hitilafu za kiufundi huweza kuwakosesha wananchi wetu kuweza kuona kwa mapana, na fursa nzuri kiasi gani wawakilishi wao waliwatuma kutoka Majimboni, wanavyoweza kuwatetea katika shughuli zao za maendeleo. Kwa hivyo nimthibitishie tu, Mhe. Mjumbe kwamba jambo hili serikali tutawataka viongozi, wasimamizi, na watendaji wa *ZBC* kuhakikisha wanakuwana timu endelevu timu ya mafundi, ili jambo hili lisijirejee isipokuwa kama kuna hitilafu kubwa za kiufundi, zinazopelekea matatizo haya, basi tutawataka *ZBC* waweze kuiarifu, ili serikali itoe iweze kutoa maelezo mengine ya ziada. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Afya

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba nilirudie hili tena, kwamba leo ni siku ya mwisho kwa Wizara hii, kwa maana ya kwamba, tunatakiwa tuimalize, sasa nina wachangiaji 13, na ningeomba sana wachangiaji tutumie dakika 10 kumi angalau wengi waipate nafasi hiyo ya kuchangia, kwa sababu kuna Waheshimiwa Mawaziri na wao wanataka kugusia. Kwa hivyo wengine kama muda hautatosha basi itabidi walete kwa maandishi, sasa nategemea kwamba wale ambao watakuwa kuna yale ambayo yameshazungumzwa basi hawatakuwa wanayarudia rudia na watatoa nafasi kwa wengine, na watazunguza *point* ambayo haijazungumzwa, ili watowe nafasi kwa wengine kuweza kuchangia. Ahsanteni.

Mhe. Naibu Spika: Mchangiaji wangu wa mwanzo atakuwa Mhe. Panya Ali Abdalla, atafuata Mhe. Hamza Hassan Juma, na ajitayarishe Mhe. Miraji Khamis Kwaza. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante. Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai kuweza kukutana hapa, lakini pia nichukue fursa hii kukushuku wewe kwa kunipatia na mimi fursa nikaweza kusema machache katika wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, Katika wizara hii mchango wangu uko katika Mradi wa kupandisha hadhi, Hospitali za Vijiji, kuwa za wilaya na wilaya kuwa za Mikoa.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wake huu. Jambo hili kwa kweli limeweza kutuweka mahala pazuri sana kwa sababu Hospitali zilivyopandishwa na Vitengo vyengine tumewekewa kule katika hospitali zetu. Kwa hivyo zimetufanya sisi watu wa vijijini sasa kuweza kupunguza mahitaji ya kuja huku mjini na kuwa tunapata mahitaji yetu kule kule vijijini ambapo tupo. Kwa hivyo shukurani zetu za dhati kwa Rais

kuliona hili na kuweza, kutaka sasa ile hospitali ya Mnazi mmoja kama alivyotuahidi, iwe ni hosptali ya rufaa, kwa hivyo inawezekana.

Mhe. Naibu Spika, masikitiko yangu yapo pamoja katika suala hili. Masikitiko yangu yapo katika hospitali yangu ya Kivunge ambayo wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja tunaitumia sana hospitali yetu hii. Hospitali yetu hii tuna daktari wetu wa upasuaji, ambaye ameondoshwa kwa sasa hayupo na nilitaka kujua Mhe. Waziri akija hapa anieleze kwa kina ili niweze kuelewa kwa sababu sasa hivi sisi tumeshasahau kutoka Kivunge kuja huku kwa masuala ya upasuaji , isipokuwa labda kuwe na kesi nzito ambazo zinakuja Mnazi mmoja. Sasa kukosekana kwa daktari huu wa upasuaji, kunaleta usumbufu na kunatutia hofu sana katika Mkoa wetu ule.

Mhe. Naibu Spika, Sasa Mhe. utakapokuja naomba unieleze ni kwa nini huyu daktari amekosekana na kama hayupo yeye ni kwa nini hamjafanya utaratibu wa kutupangia daktari mwengine, ama sivyo nazuia fungu ili niweze kuwahakikishia usalama wananchi wa Mkoa wa Kaskazini kuweza kupatiwa daktari. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana daktari aliekuwepo Dokt. Maulid Abdalla Khamis, huyu daktari ameikubali sana kazi yake, katika kuwahudumia jamii, ameielewa kazi yake vizuri, anafanya vizuri, na watu wanampenda. Kwa hivyo mnavyotuondoshea tu ghafla tukawa hatujui sababu zipi ambazo ameondoshwa daktari huyu, mnatupa masikitiko makubwa. Mheshimiwa utakapo kuja nieleze..*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali katika huduma za saratani. Mhe. serikali ilivyoleta kitengo hichi ni suala la kuipongeza, kwa sababu ilikuwa hatua ndogo tu inayohusiana na saratani, ilikuwa sisi tusafiri tuende Bara, lakini kwa sasa huduma hii pakuanzia tunapo. Kwa hivyo bado naiomba serikali yangu iweze kukileta na kile kitengo cha mionzi ambacho kwa sasa hakipo, bado tunasumbuka kwenda Bara na wagonjwa wanapata usumbufu mkubwa sana bara wanapokwenda kuhusu suala hili. Kwa hivyo naiomba sana serikali iweze kutuletea kitengo hichi ili kiwe kinapatikana hapa hapa cha mionzi, hapa hapa kwetu Zanzibar.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende tena katika Afisi ya Mkemia Mkuu. Mhe. naipongeza serikali kwa kuona ujenzi wa kuweza kumjengea Mkemia kuwa na Ofisi sasa nzuri inayotambulika tukiacha ile ya zamani ambayo iko vibaya. Lakini niseme tu Mhe. Mkemia Mkuu wa serikali ni mtu muhimu sana na ni mtu ambae anatakiwa aangaliwe sana.

Mheshimiwa huyu niseme hatafautiani sana na viongozi wale wengine ambao tunawapa ulinzi. Kwa hivyo mimi naomba sana serikali iweze kumuangalia Mkemia kwa kumpa ulinzi na yeye awe na nyumba, lakini na nyumba yenye ulinzi, kwa sababu mkemia ni mtu ambeye anakumbana na *issue* nzito nzito kwa hivyo nilazima tuweze kumjengea mazingira mazuri, ili kumuhakikishia usalama wake.

Mhe. Naibu Spika, niende katika watalamu *X-Ray* na *City scan*, wataalamu hawa kwa siku zote wanakuwa wapo kidogo katika nchi yetu. Kwa hivyo mimi naiomba serikali kuangalia kwa jicho la huruma wataalamu hawa ambao tunao ili tuendelee kuwa nao.

Mhe. Naibu Spika, katika hospitali yetu nazidi kumpongeza Mhe. Rais kwa kuona suala hili na kuwaza sasa kuingia vile vifaa vikubwa vikubwa ambavyo tunavipata katika hospitali yetu kuu ya Mnazi mmoja ikwemo kifaa hichi cha *MRI*, ni kifaa muhimu sana niombe wataalam ambao wanatumia hivi vifaa basi kuvitumia kwa uangalifu kwa sababu inaonekana sasa kwa sababu kifaa hichi kinaweza kikatumika baada ya kwishachunguzwa na vifaa vile vidogo vidogo na ikawa matatizo yako hayakuonekana vya kutosha sasa ndipo unapo unakwenda katika *MRI* kuangaliwa mwili wako wote lakini uwe ushapita katika *City scan*, ushapita katika *X-ray* lakini kwa sasa watu wanakwenda moja kwa moja katika *MRI*. Naomba sana hii mashine ni ghali sana. Kwa hivyo hata matumizi yake tuitumie pale inapolazimika kutumiwa.

Mhe. Naibu Spika, Pia naiomba sana serikali pale inapo ajiri Ma-*orderly* wetu, Ma–o*rderly* tunawahitaji wanawake kwa wanaume, lakini niombe sana kuangalia, inapoajiri ma -*oderly* wanawake basi na ma-*orderly* wanaume wawemo kwa wingi, kwa sababu si kama labda napinga wanawake wenzangu wasiwepo hapana, hapana wanawake wenzangu napendelea wawepo katika kila sehemu. Lakini sisi wanawake saa nyengine tunamahitaji yanatukwaza na hii sehemu ni muhimu sana, tunapopata *maternity leave* katika sehemu ile watu wanne,watano wameweza kuondoka pengine kwa wakati mmoja, sehemu ile inaweza kudorora katika kazi zake. Kwa hivyo hilo nalo tuliwekee umuhimu wa kuliona ili tusije tukafeli katika shemu hii.

Mhe. Naibu Spika, pia katika *lift*. Katika lift yetu kuna vijana ambao wanajitolea kwa hivi sasa wapo pale katika kusaidia huduma za pale.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana viajana wetu wanane, wapo pale naomba, hivi sasa wanajitolea lakini zinapotokea ajira naomba tuwaone vijana hawa na tuwajali na tuwape kipaumbele hasa, kwa sababu mtu ambaye ameacha kazi zote amesema mimi najitolea muhanga kwenda kulitumikia taifa langu. Mhe. mtu kama huyu, inapotokea ajira inabidi tumuangalie kwa jicho la huruma kwa sababu anaonesha uzalendo katika nchi yake.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa leo niseme sina mengi sana ya kusema katika wizara hii isipokuwa naitakia kheri kwa sababu ni wizara ambayo Mhe. Rais wetu ameipa kipa umbele katika wizara mbili kubwa ambazo zimepewa kipaumbele ni Wizara ya Elimu na Wizara ya hii ya Afya ambayo inaongezewa bajeti kila baada ya muda.

Mhe. Naibu Spika, naomba matumizi yanayoongezwa vizuri katika bajeti hizi pia yaweze kutumiwa vizuri ili tuende sambasamba na Mhe. Rais ambae anaitakia kheri wizara hii ya Afya na Wizara ya Elimu, kwa sababu ukiweza nchi ambayo itaweza kufanya vizuri katika Elimu na Afya maana yake itaweza kujipanga vizuri katika mambo yake mengine yote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza Rais kwa juhudi zake na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atamjaalia kila la kheri katika utendaji mzuri wa kazi lakini pia naiombea kheri bajeti hii na nawaomba wenzangu tuiounge mkono ili tuweze kuhudumiwa katika Afya zetu. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii lakini shukurani yako inaenda na sambamba na wote ambao nimewakusudia kuwashukuru.
Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja nataka, niipongeze serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona umuhimu wa kuboresha huduma zetu za Afya katika Hospitali zetu mbali mbali na serikali yetu hii inaongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein, imeonesha jitihada nguvu nyingi inaingiza katika Wizara hii ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo kwa serikali kuu lakini bado kuna changamoto nyingi katika wizara yetu hii hasa katika hospitali zetu kuu ya rufaa pamoja na zile hospitali zetu za wilaya ambazo zinataka kupandishwa kuwa za Mikoa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla sijaingia katika mchango wangu nasema kwamba juzi tuliunda kamati teule, tulipendekeza kuunda kamati teule na Baraza lako lilikubali na nilisema katika mchango wangu kwamba hatutaki kila wizara tuunde kamati teule lakini kwa kuwa kuna mambo yanaoana naomba ofisi yako iweze kuingiza katika kumbukumbu katika hayo maeneo ambayo twende tukayakague baada ya kuunda kamati yako.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru sana Makamu wa Pili wa Rais, baada ya kuona kadhia kubwa ya Wizara ya Afya sisi Wawakilishi wa CCM tuliamua kuunda Kamati teule ya Chama kwa ajili ya kuchunguza huduma zinazotolewa na hospitali zetu za Unguja na Pemba. Moja katika jambo ambalo tulililiripoti katika ripoti zile ni ubovu wa majengo yetu na uchakavu wa majengo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kitu ambacho bado naendelea kusikitika na hili naomba liingizwe katika ile orodha ya mambo ambayo Baraza lako litakwenda kuchunguza jengo letu jipya la hospitali ya Mnazimmoja ambalo kabla halijachukua hata miaka miwili jengo tumelikuta linavuja utafikiri chungio. Mheshimiwa hii lazima twende, lakini siyo jengo kuvuja tu tulikwenda tukakuta katika lile jengo ambalo la watoto kuna vioo vile vimefanya ukungu maana yake siyo vumbi tukauliza kwanini ma-orderly hamsafishi wanasema Mheshimiwa havisafishiki kwa sababu ukikigusa kioo kinakatika kinavunjika leo ndiyo jengo jipya hilo kwa hivyo katika maeneo ya uchunguzi.

Mhe. Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu tulikwenda hospitali ya Chakechake jengo la hospitali paa jipya linavuja kama chungio, wagonjwa hawatakiwi walale wakielekea juu mgonjwa anatakiwa akilala alale kifudifudi akielekeda juu dari inampukutikia Mheshimiwa ni aibu, lazima tuhakikishe kwamba majengo haya wale ambao waliyoyajenga tunakwenda tunayafanyia utafiti na kama wamejenga chini ya kiwango, siyo kama wamejenga chini ya kiwango lazima hatua za kinidhamu na uwajibikaji zichukuliwe.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka katika mchango huo kwa kweli nataka niendelee katika *paragraph* hii ya 100 ukurasa wa 35 hapa Mhe. Waziri anasema, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipozindua Baraza la nane la Wawakilishi Novemba, 11 alisema nanukuu "Hospitali zilizo katika kiwango cha *Cottage* za Micheni,Vitongoji - Pemba, Makunduchi, Kivunje nazo zitapandishwa daraja zifikie hadhi ya hospitali za wilaya"

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri sana siku aliyoitoa kauli hiyo Mhe. Rais tulikuwepo sote lakini vile vile ile kamati yako ikataka ikaone namna gani hili agizo la Rais zinavyotekelezwa. Mheshimiwa pamoja na kitabu hili kimepambwa vizuri kwa maneno lakini bado ukienda *field* hali haiko kama kilivyopambwa hiki kitabu.

Mhe. Naibu Spika, tumekwenda hospitali ya *Cottage* Makunduchi, tumekwenda hospitali ya *Cottage* ya Kivunge kwa kweli ni hatari uhaba mkubwa sana wa madaktari, kazi zile ambazo ilikuwa zifanye na manesi zinafanywa na ma-orderly. Ma-orderly tumewakuta wanapiga mpaka sindano. Hili kwa kweli ni tatizo lazima agizo la Rais litekelezwe kivitendo. Nimeona hapa ajira imefanyika lakini kamati yangu ilikwenda kufanya uchuguzi Pemba tukagundua kwamba yale mahitaji ya *staff* pamoja na madaktari hawapungui karibu watu 600 leo ukiangalia hapa tumeambiwa wameajirwa watu 443 kwa hospitali zote bado tuna changamoto kubwa hiyo itabidi ifanyiwe kazi.

Mhe. Naibu Spika, jengine hospitali ya Kivunge, kwanza ile hospitali haina daktari wa upasuaji labda kama kapelekwa jana na leo au na juzi. Tumekwenda tumemkuta daktari alokuwepo *theater* ni daktari ambaye tayari amestaafu serikali imeshindwa kumpatia mkataba, mganga yule ameajiriwa na kampuni moja inaitwa *Hips* ambayo ndiyo inayoshughulikia hospitali ya Makunduchi na hospitali ya Kivunge. Lakini vile vile yule *Nurse* au wale wasidizi wake, yule mfuaji wa nguo ndiye anaemsaidia yule mganga pale wa *theater* leo tunakwenda wapi.

Mhe. Naibu Spika, leo tunaambiwa tayari utekelezaji wake uko mzuri zinapandishwa hadhi ya Wilaya, hadhi ya wilaya hospitali haina mtu wa operesheni kwa sababu yule ni *part time* anaweza akafanya akachoka anaweza akaamua kuondoka, kwa nini hospitali kama ile inashindwa kuwa na daktari dhamana ambaye ni mganga katika suala zima la *Staff*. lakini leo katika changamoto kule Mhe.Waziri alieleza kwamba kuna uhaba wa wafanyakazi kupatikana Mheshimiwa kamati yetu imefanya utafiti kuna vijana wengi wamesoma fani mbali mbali za udaktari wako mitaani na vyeti vyao hawaajiriwi. Kwa kweli mimi nashindwa kushangaa yaani sielewi elewi kuna madhumuni gani huku wizara ya afya. Kama tunaweza kuunda kamati teule ya kuichunguza ile *management* yote ya wizara ya afya kujua anaekusudia kufanya kazi au wanakusudia kutuvuruga.

Mhe. Naibu Spika, kuna vitu havitakiwi labda kuzungumziwa *theory* hospitali ukienda unataka uone *pratical*, kitengo cha *emergence* hospitali ya Mnazi Mmoja pale pana daktari mmoja. Sisi kamati yetu siku tulipokwenda tumemkuta daktari pale kaja kavimba macho kalala kucha pale akaambiwa kuna kamati inakuja hakuna mtu mwingine ikabidi aamke arudi tena pale amevimba macho usingizi anasema yeye yuko peke yake leo *immanence* unampeleka pale daktari mmoja, unampeleka *orderly* mmoja. Leo gari

imepata ajali mungu aepushe mbali wanakwenda pale wagonjwa sita au saba mtu mmoja anafanya nini. oderly yule yule anasema kwamba yeye pale ndio inabidi apokee wagonjwa lakini vile vile apandishe wagonjwa juu *lift* mbovu anakwenda anabeba kwa kweli hii ni hatari. Sasa kitabu hiki ukikisoma kitamu lakini ukienda *field* kuchafu kwa kweli mambo haya Mhe. Naibu Spika lazima Mhe. Waziri kwa kweli ajitahidi kuyasimamia vya kutosha.

Mhe. Naibu Spika tumeelezwa hapa hospitali sasa hivi hizo za wilaya zinapata mgao wa kutosha. Mheshimiwa si kweli tumekwenda sisi kama si ile kampuni ya *Hips* ambayo ndio waliyofunga mkataba na Wizara ya Afya wale ndio wamekuwa na dawa za kutosha na kwa sababu pale zinapatikana kwa sababu wananchi wanachangia, lakini huku kwengine ukija unaambiwa wananchi wasichangie. Hospitali za Pemba nyingi tumekwenda hizo ambazo tumetembelea wananchi hawatakiwi kuchangia mtu akichangia ile shilingi elfu mbili tu tayari *ZAECA* wamefika. Ndiyo kama yale yaliyozungumzwa jana inafika pahala hospitali *bandage* hakuna plasta hakuna ni aibu tupu, sasa lazima tufike pahala tufanye maamuzi yaliyokuwa sahihi na labda tuweke mjadala mpana kuhusu hii sera yetu ya huduma za afya bure.

Mhe. Naibu Spika, hapa tumeambiwa mpango wa kuanzisha Bima ya Afya, mkakati ili kukamililisha mchakato wa uanzishaji wa Bima ya Afya Zanzibar uko njiani. Mheshimiwa tushachoka hiyo njiani yenyewe sijui tutafika lini maana yake siyo njiani huko mbioni. Mheshimiwa leo hospitali yetu Kuu ya Mnazi Mmoja Hospitali ya Rufaa, nimejaribu kuchukua takwimu za Bima ya Afya hapa tunaambiwa idadi ya wagonjwa waliohudumiwa kwa bima ya afya ni 4,673 tumeweza kukusanya shilingi 252,287,000 hospitali ya Mnazimmoja, hospitali ya Al-Rahma wamepata huduma ya Bima ya Afya wagonjwa 30,000 Mnazimmoja hospitali ya rufaa wagonjwa 2,673 hospitali ya Al-rahma wagonjwa 30,533 wamekusanya pesa za bima ya afya shilingi 2,743,000,000. Hebu angalia *gape* sisi tumekusanya 252,287,000 leo hospitali ya Al-Rahama ikishafika tarehe 27 Mkurugenzi pale keshafika Bima ya Afya anasubiri pesa aende akalipe mishahara. Yule anaweza kuwalipa wafanyakazi vizuri na hapo Al-Rahma ukienda unawakuta wafanyakazi wa Mnazi Mmoja kwa nini sisi tusijenge hospitali yetu tusipeleke vifaa vya kutosha wakabakia wakafanya kazi katika hospitali yetu. Leo ile tunaiita hospitali ya rufaa.

Mhe. Naibu Spika, hospitali ya Global wamehudumia wagonjwa karibu 39,000, Mnazimmoja 4000 wamekusanya karibu 2,743,000,000 samahani wale Al-Rahma ilikuwa 1,176,000,000 Global 2,743,000,000. Sasa Mheshimiwa kwanini nikasema hivi, hospitali yetu ya Mnazimmoja pamoja na kuwa tunasema hospitali ya rufaa lakini huduma nyingi pale hazipatikani. Leo pale unakwenda unaandikiwa vipimo vitatu unapata kipimo kimoja vipimo viwili unaambiwa nenda Global nenda Al-rahma nenda wapi ndiyo maana wagonjwa wetu wa Bima ya Afya wanakuwa hawendi pale, kwa sababu wanaona kwanini hapa niende nishapiga foleni halafu naambiwa huduma nyingine niende hospitali nyingine ndiyo mtu anaamua bora kwenda zake Global au bora kwenda zake Al-rahma. Kwa kweli Mheshimiwa tuna tatizo kubwa hapa lazima serikali yetu tujue tunafanya maamuzi yaliyokuwa sahihi.

Mhe. Naibu Spika, nakuja bohari ukiangalia kwa mahesabu hapa tunaambiwa walipangiwa 7,000,000,000 lakini walipata karibu 4,000,000,000, lakini dawa zilizopelekwa pale au vifaa tiba pamoja na madawa karibu 8,000,000,000 lakini kwanini ukienda hospitali unapata asilimia 60, kipindi kile Mkwezi na Mkulima Mhe. Hassan Khamis Hafidh siku moja tulikwenda tukauliza tukenda tukafanya *research* tukamtafuta mgonjwa ambae amepewa cheti pale kwenda aliandikiwa dawa karibu sita kama sikosei alipata dawa tatu, yaani karibu asilimia 50. Sasa kwa nini ukija kwenye takwimu tunaambiwa bohari imepewa pesa nyingi za kutosha lakini kule ukienda katika vituo vya afya dawa huzikuti za kutosha kwa nini. Hapa pana nini Mhe. Naibu Spika, lazima tufike pahala tuwe wakweli. Lakini huko bohari kwenyewe sisi tulikwenda tukauliza kwa nini dawa hamzipeleki za kutosha wakasema ndiyo bajeti yetu ilivyo wao walitwambia wanahitaji bajeti kama ya shilingi 9,000,000,000 safari hii nashukuru mmeweka zaidi ya 14,000,000,000 tutaona matokeo yake kama yatakuwa.

Lakini hata hao bohari mpaka sisi tunaondoka wanadaiwa karibu 1,200,000,000 na hao ma- *supplier* wa madawa. Sasa sijui kama weshalipwa au vipi tunashukuru mpango wenu mliokuja nao sasa hivi alau mnataka kwenda moja kwa moja katika ile bohari ya madawa ya Dar es salaam.

Mhe. Naibu Spika, tuje katika magari hapo wamesema hospitali hizi *cottage* wana usafiri wana *ambalance* tumekwenda tumezikuta *ambalance* Kivunge na Makunduchi miezi sita hazijafanyiwa *service* tunauliza pale wanasema pesa hawana. Leo kama ndiyo wewe hiyo gari *first truck* mtu anakimbizwa kutoka kivunge anakuja mjini gari miezi sita haijafanyiwa *service* si ndio unakwenda kumuua na huyo mgonjwa. Mheshimiwa kwa kweli ni aibu, tumekwenda Pemba pale magari mabovu, gari siyo kama hawana magari mabovu lakini vile vile hata hizo gari nzima mafuta hawana. Mhe. Naibu Spika, kila kitu utakuta ni vitu ambavyo vizungumkuti, kwa kweli hatuvielewi.

Mhe. Naibu Spika, katika eneo jengine ambalo pia nataka niliseme katika suala zima la hivi vituo vya afya. sisi kwa bahati nzuri katika maeneo ya ng'ambu wagonjwa wengi wanatoka ng'ambu kwa sababu ng'ambu ndio ambako tupo sisi masikini. Nimeshaomba sana kile kituo changu, samahani kituo cha jimbo maana nikisema changu maana yake ni changu mwenyewe. Kituo chetu cha jimbo cha Kwamtipura, kile kituo ni kituo kikubwa kinahudumia wagonjwa wanaotoka mpaka Mwera na sehemu nyingine mbali mbali. Kwa nini kituo kile ikifika saa nane kinakuwa kinafungwa, leo utakuta kuanzia saa tisa na kuendelea, hospitali za *private* nyingi zipo zinafanya kazi pale pana majirani zetu Amani fresh Asaakheir wanafanya kazi saa ishirini na nne. Leo kituo kile wananchi wamejenga kwa nguvu zao tunashukuru serikali imetuletea madaktari kwa nini leo tunashindwa kwenda alau mpaka saa nne ya usiku, alau kupunguza ule mrorongo wa wananchi katika kupata huduma ya afya.

Mhe. Naibu Spika nikiendelea na mchango wangu nakuja katika suala la huduma, ukitaka usitake ukiboresha huduma za Mnazimmoja kelele zote zinapungua, kwa sababu pale ndiyo kwenye rufaa Lakini pale Mheshimiwa utakuta kile kitengo cha matengenezo yaani *engineering* kinatengewa bajeti shilingi milioni mbili. Leo vifaa tiba matengenezo yake na spare zake ni ghali sana ukiangalia pale kuna mashine zimekuja hata miaka miwili

bado, mashine tayari zipo stoo ukienda unaambiwa sijui kuna kifaa gani kifaa gani, vifaa vyote havifanyi kazi. Lakini hata mafundi wetu hawajawa *updated* katika *skill* zao leo tunapeleka vifaa vya kisasa mafundi hawajapatiwa mafunzo. Leo viti pale viti vya kitengo cha meno tumekwenda pale wale wafadhili waliokuja wakaweka wakasema pale uwekewe mfuko maalum kuwe kuna *retention,* kwa sababu wakasema wenyewe hivi vifaa vyake ni ghali, kiti kizima kimeharibika kitu kidogo daktari hajui samahani siyo daktari tushazowea kila anaefanya kazi hospitali tunamwita daktari, fundi hajui tayari kinakaa pembeni hakifanyi kazi.

Sasa leo serikali yetu ina-*invest a lot of money* inaingiza katika hospitali zetu lakini hatuwaandai mafundi kwa ajili ya ukarabati. Hii ndiyo sawasawa na Mapinduzi II leo chombo kipya matokeo yake kinalala, yaani hii serikali yetu sasa hivi watu wanaifanya kama ngarawa ya Juma Faraji kila mtu anafanya vile anavyotaka hakuna usimamizi. Nimeshukuru humu katika hii ripoti mmesema sasa hivi mnaweka ile *perfoment contract* yaani yule mtu namna gani anafanya kazi na kuweza kuwa *awarded*.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kitengo kile cha matengenezo kama hatujakirekebisha na kurekebisha kwenyewe wale mafundi kupatiwa mafunzo, waliomba kwenda Dar es salaam wakaambiwa pesa hakuna vifaa vinaharibika wanatumbua macho pale wanatizama ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika ule mtambo wa *oxgen* pale kuna mchezo unachezwa, kuna mtambo wa *oxgen* toka umeletwa haujawahi kufungwa, umefungwa lakini haujawahi kufanya kazi. Mtambo ule ambao gesi yake ilikuwa ikisumuma ina-*supply* ndani ya jengo zima lile la hospitali. Mtambo pale umekaa umekwenda pale kile chumba kilichokuwepo ile mitambo ya gesi kimeshaota kutu kuna ma-*AC* za hospitali ya Mnazimmoja, asilimia hamsini zote hazifanyi kazi. Leo unamkuta daktari anamtibu mgonjwa anatoka nje kwanza anakwenda kujipepea anakwenda kujipepea vinginevyo yale majasho yatamdondokea mgonjwa. Mheshimiwa tatizo hii ni aibu, kwa kweli kila ninavyoangalia huduma zetu bado sipati picha.

Mhe. Naibu Spika, katika eneo la mapato mimi nitakuja kuzuia, katika hilo fungu lililokatazwa siku zote hapo unaambiwa mapato ndipo nitakapopaanza. Pale sisi tulisema mfano kama Kitengo cha *Dialysis,* leo tunaambiwa huduma za usafishaji figo bure lakini hii bure baadae ndiyo inageuka bure ghali. Mimi juzi mwezi huu wa Ramadhani kuna kijana wangu ananipigia simu mama hali mbaya unatakiwa mpira, mpira wa nini sehemu ya kusafisha mapafu mnawaambiwa bwana nyie hapa bure kila kitu nani daktari gani huyo, napiga simu naambiwa kweli mpira ule unaitwa *dialysis catheter* hakuna. Mtu anaambiwa aende akanunue Global laki mbili na nusu ndiyo bure hiyo. Kwa nini pale tusiweke mchango alau watu wakachangia elfu hamsini, hamsini. Kwa sababu kama kitu kile anaweza kukipata kwa shilingi elfu hamsini kwanini twende tukanunue kwa shilingi laki mbili na nusu. Kwa kweli hospitali zetu hizi zina mapungufu mengi na kama sisi hatukusema hapa kwa kweli tutakuwa hatujisaidii sisi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie sehemu ndogo ambayo kama ulivyosema dakika zangu zimebakia mbili, nakuja hospitali ya Vitongoji na hospitali hii ya Kivunge, kwa

sababu nina mambo mengi sijui nianze lipi nimalizie lipi. Kuna vifaa vile vya kufanyia huduma za meno ile rangi mpaka ishachujuka vina kutu, Hospitali ya Vitongoji sijui kama hao viongozi wa wizara alau kama wanaijua na wanakwenda. Tumekuta pale aibu yaani vifaa tokea imefunguliwa hospitali ile sijui mwaka arobaini na ngapi mpaka leo havijapelekwa vingine vipya. Halikadhalika Kivunge pale vifaa vimeshageuka rangi leo mgonjwa anakwenda pale ana tatizo la meno unamuingiza mkasi una kutu si unamg'oa meno mengine hayo. Sasa kwa kweli kila ninavyojaribu kuangalia wizara hii sijui nichangie vipi sijui nipitie wapi alau ipatikane hiyo salama. Lakini kitu ambacho ninachokizungumza bado tunahitaji kuboresha vifaa vyetu katika hospitali zetu lakini vile vile kuwatafuta madaktari wa kutosha katika maeneo yetu. Hospitali nyingi sasa hivi ukiangalia wale ma-*orderly* ndio wanaofanya kazi za manesi.

Laa kumalizia tuliambiwa katika hospitali sasa hivi kuna utaratibu unataka kufanywa na sijui kama mshauanza au vipi, ma-*orderly* sasa hivi mnasema hamtaki tena kuajiri, kazi za *orderly* mnataka kuwapa kampuni. Mheshimiwa mnaanza kutaka kututolea aibu zetu. Kazi ya *orderly* yule vile vile anakula kiapo, leo yule anaambiwa kapeleke mkasi anakwenda pale anamkuta mama anagaragara pale mambo mengine ndiyo hivyo, huyu hana miiko yeye ni msafishaji tu. Leo kaajiriwa na bosi wake kwenda kusafisha kesho kamfukuza kazi. Mheshimiwa kama mna kampuni zenu hazina kazi za kufanya kuna mahoteli kibao waende wakafanye kazi, lakini sio mtuletee katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika hospitali kuna maadili, kuna miiko, mgonjwa akiumwa akili zinamruka anakuwa hana akili. Kuna safari moja kule chumba cha wazazi nilifanya kama kuteleza nikamkuta mtu kabeba nguo juu ya kichwa, sasa kama kabeba nguo juu ya kichwa utegemee kuna nini hapo. Sasa kwa huyu mfanyakazi wa kawaida msafishaji atakwenda kusema daah! Isijekuwa ndio mimi nisije nikawa na mimi ndio natoa hizo siri za wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache suala hili la makampuni kuja kusafisha hospitali Mhe. Waziri nataka aje anipe ufafanuzi na kama atasema bado mpango huo wanao mimi sitokubali na nitazuia mimi fungu katika suala la utawala.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache nilikuwa sina mengi, lakini lile ombi langu la mwanzo la kufanya ukaguzi katika huo uchunguzi utakaofanywa katika majengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na haya ya Wizara ya Afya naomba uyazingatie. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma mchangiaji anayefuata ni Mhe. Miraji Khamis Mussa baadae ajitayarishe Mhe. Bahati Khamis Kombo na atafuata Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: *Bismillahi Rahmani Rahiim.* Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya.

Kwanza na mimi niwe mkweli kwenye wizara hii, na nia hasa kuzuia mshahara wa Mhe. Waziri fungu la utawala lile la mwanzo nianze na hilo lakini la pili, nina nia ya kuzuwia fungu la Hospitali ya Mnazi Mmoja, kama sikupata majibu ya kutosha maeneo mengine sina tatizo nayo lakini maeneo haya mawili.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwe muwazi na nitabakia wakati wowote Mwenyezi Mungu akinijaalia kusubiri majibu, lakini niungane na Mhe. Hamza Hassan Juma iko haja ya kuundwa Kamati Teule kwa ajili ya majengo lakini pia na kwa ajili ya watendaji katika eneo la hospitali ya Mnazi Mmoja, baadhi ya watendaji hawatufanyi vizuri, hawatufanyi haki wala hawamsaidi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye jambo zima na dhana nzima ya huduma ya afya kwenye eneo hili la hospitali ya Mnazi mmoja.

Fedha inakwenda nyingi lakini matokeo ya fedha zetu hayako vizuri, huduma tunazozitarajia hazipo vizuri leo unakwenda eneo kama la mabaara hospitali ya Mnazi mmoja, unakuta toka Februari kifaa cha maabara kinaharibika ambacho ukenda ukakinunua hakifiki hata thamani ya milioni mbili kifaa cha *chemistry analyzer* ikesha kuna viongozi, kuna watu ambao wanasimamia hili jukumu, lakini ukiuliza kimeharibika nini unapewa taarifa imeharibika balbu na feni. Yaani unachangaa sana, lakini kikiharibika kifaa kama hichi inawezekana kwamba kuna vifaa vyengine vinavyokwenda kufanikisha kazi yaani vinategemeana vinakaribia ku-*expire* ambao hivyo vina thamani kubwa kuliko ile thamani ya matengenezo ya kifaa kile.

Kwa hivyo unafika pahala unapata mchangao mkubwa hawa wenzetu kweli wako katika dhamira njema ya kuwasaidia serikali, na ndio maana nikasema sitakubaliana hata kidogo kulipitisha fungu hili la mishahara ya viongozi hawa, lakini pia na mshahara wa Waziri kwa sababu anawasimamia pale pamoja na watendaji wengine Lakini niingie eneo la pili kuna kadhia kubwa sana kwenye mtambo huu wa *oxygen,* sisi tumefatilia unafika pahala unakutana na wale mafundi wanaotengeneza ule mtambo wanafika pahala wanasema mimi nashangaa sana, sijawahi kutengeneza mtambo huu mara kwa mara kuliko maeneo yote ninayokwenda kufanya kazi ndani ya nchi karibu nne ametutajia.

Lakini wenu huu kila siku hapa hujuma ipo, na wanaohujumu maana yake ni hawa hawa wafanyakazi tunaowajiri na wakala pesa za wakwezi na wakulima ndio wanaolipa kodi za nchi hii. Sasa imefika pahala unapata mshangao mkubwa, ndio maana tukasema sura ya utendaji na wenzetu hawa hawako vizuri, hawamsaidii au hawaisaidi dhamira njema ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa tunachangia ili kuboresha maeneo hayo ili huduma iende, mtambo unaharibika mara kwa mara lakini watu wanapata tenda sasa ya kwenda kununua *oxygen* Bara na kuleta zetu huu, maana wanaharibu kwa makusudi ili wapate kazi ya kufanya hapa katikati.

Mhe. Mwenyekiti, waziri unajua kuwa temepata sisi msaada wa mtambo mwengine kutoka Uturuki huu mwaka na haujafanywa *installation.* Sasa leo huu mtambo tulionao unaharibika, lakini mnapata namna maana yake ya kwenda kununua *oxygen* ile kupitia mtungi ile ya kawaida, lakini mtambo tunao ambao tukiu-*install* tutapata, ukiharibika huu

katika hiyo dhana ambayo tunakwenda nayo wenzetu hawatusaidi, wanaiharibu kwa makusudi ndio eneo hili tunalolalamikia lakini ukiharibika huu, si tungeuufunga huu *installation* yake inafika gharama yake ni kiasi gani, kuonekana mtambo umefika pahala umepata msaada. Msaada ule wenyewe wanafuatilia lakini mpaka leo wafanyakazi hawa tulionao, huo nao uliokuweko juu wanafikiria kwenda kuhatibu. Mwenyezi Mungu atusaidie awakimbize kwenye hujuma zao ambazo wanataka kutufanyia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nende katika eneo la kinga nimpongeze sana Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya, lazima tukiri amejitahidi sana mimi nilikuwa katika moja ya wahanga ya maradhi yale ya mripuko wa kipindupindu ni mmoja wapo. Kwa sababu jimboni kwangu hakuna hawa watu lakini na kituo ambacho napokea kutoka maeneo tofauti. Katika moja ya kazi yake elimu imetoka, lakini imetoka katika maeneo mengi kwenye malaria, tunaona kwenye kichocho nimesoma taarifa nimeridhika sana na kazi yake anayoifanya. Lakini matokeo ya kazi yake ni mazuri mno lazima tumpongeze na tumpe haki yake amejitahidi na amefanya kazi kwa uweledi mkubwa, sisi tulikuwa tunaona vipeperushi na matangazo mbali mbali ambayo ametusaida kupunguza baadhi ya maradhi mengine. *(Makofi)*

Lakini naomba nishauri tu, kwenye eneo moja la kulinda haya maradhi mengine ya mripuko kutokuingia nchini aboreshe zaidi au akaze kamba zaidi ili mambo haya yaende vizuri zaidi, ili tukija mara nyengine tumpongeze vizuri zaidi. Eneo moja ajikaze zaidi kwenye maeneo wanayoshuka abiria katika maradhi hasa yale ya *Ebola* tulikuwa tunaona bandarini tunapata, lakini *Airport* ukenda hamna.

Lakini kuna vituo vyengine abiria wetu wanashuka, kama Mkokotoni maeneo mengine kama Kizimkazi hatuna sasa aidha serikali ifike pahala tuwe na maeneo mawili ya kupitia kule kwengine tuzuiwe au wizara nayo katika Idara hii ya Kinga, Ukurugenzi hii ya Kinga basi itanue wigo katika kwenda kudhibiti watu wale wanaoingia ili kama kupima tuwe tunafanikiwa kuwapima wote katika vile vituo. Lakini pia azidishe kasi ya upimaji wa afya kwa wafanyakazi tumeona taarifa zipo, zipo taarifa zimo ndani ya kitabu hichi takwimu yake wala sitaki kuisema nimempongeza lakini niseme azidishe kasi, mara kwa mara uwe upimaji huu unakwenda vizuri lakini na kazi kwa wafanyakazi wetu hiyo tuwe tumewasaidia katika kuengeza kasi hii. Lakini nimpongeze sana Mkurugenzi huyu. *(Makofi)*

Lakini naomba nende kwenye Taasisi yetu, Bodi ya Chakula yule wakala wetu naomba nimpongeze kwa dhati kabisa, Dkt. Burhan naye amefanya kazi kubwa fungu lake naomba Waheshimiwa Wajumbe na fungu la Mkurugenzi Kinga twende nalo vizuri, lakini yale mengine naomba niunge mkono katika kuyazuia mpaka Waziri atowe majibu mazuri.

Lakini Mkurugenzi huyu, amekuwa muadilifu mno maana ana kazi yenye changamoto kubwa sana, lazima tukiri anafika pahala anakwenda kufanya ukaguzi anakamata mali za wafanyabiashara ambazo zinahatarisha maisha ya watu na unaona anaangamiza. Ana riski sana, lakini uadilifu wake Mwenyezi Mungu atamsaidia. Lazima tufike pahala kwenye eneo hili maneno ya Mhe. Jaku moja iwe moja lakini mbili iwe mbili, mwenzetu

anajitahidi sana, amejitahidi sana, tumpongeze azidishe kasi tu kwenye maeneo mengine kuna wenzetu hawa maana mpaka wanatuletea bidhaa zetu hapa hatuna taarifa za kule wanakozitoa.

Aidha, wanazipata vichochoroni au wanapata kwenye maghala ya kawaida ambao na kule kuna wafanyabiashara nje ya nchi, sasa ikifika pahala ukaguzi ule wa JMP aliotufanyia sisi, sehemu ya wafanyabiashara tuliokuwa tunaleta kuku, basi na wenzetu wanaoleta peremende wanaoleta unga huu, lakini wanaoleta bidhaa nyengine basi kuna haja na wao wakaonekane wapi wanautoa, au wapi wanatoa bidhaa zao sasa niombe tu sisi tulidiriki kutoa hizo gharama maana mimi ni mmoja wa wafanyabiashara naomba ku-*declare interest* tuliokuwa tunaleta kuku nchini.

Sasa sisi wafanyabiashara wa kuku tumefanyiwa hivyo, na tumeunga mkono tunafanya jitihada kubwa kuna kuku wanaingia si rafiki, lakini sasa hivi kazi ile imekwenda vizuri, sisi tuliona dhana mbaya lakini baadae tukaelewa, dhamira njema ya mwenzetu huyu Dkt. Burhan pamoja na wafanyakazi wake. Kwa hivyo eneo hili jengine azidishe kasi ambayo na wenzetu hawa wapate fursa lakini na mwelekeo wa taasisi hii uende vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nende Kivunge, katika hospitali ya Kivunge wenzangu wamechangia lakini kuna mambo wameyabakisha, kuna eneo la kupokelewa wagonjwa OPD, sababu hasa maana yake kutaka mshahara wa Waziri uzuiliwe maana haiwezekani eneo kama hili la kupokelewa wagonjwa pia likose umeme, ile huduma ya umeme inasikitisha sana maana wewe utakuwa unapokea wagonjwa mchana tu hospitali yetu tunataka kuitoa wilaya kwenda mkoa. Usiku maana yake unakwenda kumurika kwa tochi wakati majengo yote yana umeme, sasa ndio maana unafika pahala tunasema hebu tuzuie huu mshahara wa viongozi hawa haya mambo yakafanyike.

Lakini kuna posho za wafanyakazi *food allowance*, Mnazi mmoja kule nimeondoka wenzetu wanadai toka Machi mpaka leo hawajalipwa, lakini Kivunge wanadai toka Januari hawajalipwa, mambo haya ndio yanayowapa motisha wafanyakazi kwa sababu ni haki yao ya msingi. Kwa nini sisi viongozi tunafanya vikao tunalipana, mimi naomba ukija uki-*windup* useme tu kuna viongozi wangapi walikaa ndani ya mwezi huu ikesha posho zao hawajachua. Lakini wafanyakazi wanawalikimbizia wengine kuna maneno si rafiki, wanawambia subirini baada ya bajeti maana pesa zimeisha. Pesa zimeisha kwa sababu mmeharibu mitambo yetu ya oxygen maana mmepata hizo hizo, kwenda kununua mitungi ya oxygen au kitu gani kilichotendeka, ndio maana nikasema kunako eneo hili tutazuia mafungu ili wenzetu hawa wakae vizuri, mpaka tupate majibu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kunako eneo la mwisho, ambalo nililiacha la hospitali ya Mnazi mmoja na niliacha kwa sababu nilihisi tu kama wenzangu wameshalichangia lakini nilipofikiri bado. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri katika dharura moja kubwa sana ambayo hatuwezi kuistahamilia ile dawa basi pia ya kukoshea vile vifaa vilehaipo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika moja.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Dakika moja hiyo inanitosha kwa kumalizia ile dawa maana yake mpaka sasa hivi imekuwa ni changamoto pia, maana dawa ile ukiweka vifaa vile maana yake unaweza kuvitumia kwa ajili ya mgonjwa mwengine.,Hospitali kubwa kama ile ikikosa dawa ya aina hii maana yake ni hatari mno, jambo baya sana hili maana yake unaweza ukasababisha mripuko kwa watu wengine. Tunajua madaktari wetu waandilifu lakini katika uandilifu nao katika vifaa muhimu kama hivi vipatikane.

Mwisho kabisa naomba niendelee na msimamo wangu wa kuzuia mafungu yale niliyoyasema mengine nitaandika kwa maandishi lakini sitaruhusu kwenda Mhe. Naibu Spika, kama sijapata majibu ya utekelezaji wa mambo haya, nilitaka kulizungumza suala la sera ya wageni ile lakini nitakuja kuchangia kwa maandishi. Mwisho naunga mkono kwa asilimia arubaini, sitini nabakisha kwa ajili ya kuzuia mafungu hayo, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis mchangiaji anayefuata ni Mhe. Bahati Khamis Kombo na ajitayarishe Mhe. Ali Salum atafuata Mhe. Ahmada Yahya.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kwa kupata fursa ya kuweza kuchangia machache.

Kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kututeulia Mhe. Hamad Rashid kuwa Waziri wa Wizara ya Afya. Lakini pia nikuchuwe fursa hii ya kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi kubwa wanazozichukua kufanya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja katika ukurasa 34 mradi wa kupandisha hadhi hospitali za vijiji kuwa za wilaya na wilaya kuwa za mkoa, nimeona hapa kwamba kuna hospitali mbali mbali ambazo zitapandishwa hadhi lakini chini hapa kuna maandalizi ya ujenzi wa paa la hospitali ya Chake Chake, yamekamilika mkandarasi ataanza kazi hivi karibuni.

Mhe. Naibu Spika, ningekuwa ni vizuri sana hapa Mhe. Waziri angetuliwekea yule mkandarasi ni yupi, kwa sababu na wasiwasi wangu mkubwa wa kuwa mkandarasi ni yule yule Rans, ambaye mkandarasi huyu tayari huko nyuma ameshatufanyia mambo yaliyokuwa hayaridhishi, kwa hivyo namuomba tu Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwamba ni mkandarasi gani ambaye ataanza kushughulikia shughuli hiyo.

Lakini vile vile, Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa 35 kifungu 39, Mhe. Naibu Spika, nimeona hapa kwamba tayari michoro ya nyumba ya hospitali ya Abdalla Mzee imeshakamika. Sasa Mhe. Naibu Spika, michoro hii tunaitegemea kwamba wakati wowote hospitali ya Abdalla Mzee watajengewa wafanyakazi nyumba. Lakini ningemuomba Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwamba ingelikuwa ni vizuri sana kwamba tungeliwapata wale waliojenga hospitali ile, ili kuweza kutuekea ramani hospitali ya Abdalla Mzee ikawa vizuri. Kwa sababu kwa taarifa tulizonazo kwamba hizi nyuma zitajengwa katika maeneo yale yale, kwa hivyo namshauri sana Mhe. Waziri ni vizuri sana tukawapata wajenzi wale wale waliotujengea hospitali ile.

Lakini vile vile, nimwambie Mhe. Waziri kwamba wenzetu wa China wanatusaidia sana, wanatupa mikopo mingi, lengo lao ni kuwa Zanzibar inawirike kimaendeleo. Sasa haitokuwa jambo la busara kama nyumba hizo ambazo zitajengwa na wakapewa watu wengine, yakaja yakarudia yale yale ya kuvuja. Kwa kweli tutakuwa hatujawatendea haki kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hili ulizingatie kwa kina ili uko mbele tusije tukaharibikiwa. *(Makofi)*

Lakini vile vile, Mhe. Naibu Spika nije katika hospitali ya Abdalla Mzee, nawapongeza sana wafanyakazi wa hospitali ya Abdalla Mzee, ambao wafanyakazi hawa hivi sasa pamoja na malalamiko mengi ya wananchi wanafanya kazi vizuri, na kazi hizi ambazo wanazifanya kwa kweli wanawanchi hivi sasa wanaridhika vizuri sana. Namuomba Mhe. Waziri kwamba wafanyakazi hawa uendelee kukaa nao na wao waendelee kufanya kazi zao vizuri, isiwe hapa tunawasifu na badala yake wakaja wakaharibu.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 43 kifungu cha 21, Program ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hapa nina nia ya kuzuia fungu H02, tunaamini kwamba Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ni Hospitali mama na ni Hospitali ambayo inategemewa na wananchi wote wa Zanzibar na Pemba. Inapozungumzwa sana kwa kweli tunaumia ndani ya roho zetu, kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar lengo lake ni kuimarisha huduma hizi za wananchi ili wasipate matatizo na tusiweze tena kusafiri kwenda nje kwa ajili ya kupata huduma ambazo zinaweza kufanyiwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, masikitiko yangu, nia ya kuzuia hili fungu, wiki mbili zilizopita kuna jamaa yetu alipata tatizo la mtoto wake alianguka akavunjika mkono. Mtoto yule tukampeleka Hospitali akatiwa popo lakini siku ya tatu alitakiwa arejeshwe kwa ajili ya kuangaliwa. Kufika popo lile alitolewa na akaambiwa baada ya siku tatu ili aende akafanyiwe mazoezi. Alivyokwenda siku ile ya tatu daktari akamlaumu baba mtu kwa nini huyu mtoto akavuliwa hili piopio wakati waliolivua piopio ni wale madaktari wenyewe. Akaambiwa akatiwa piopio jengine lakini akakae siku tatu mbele siku ya nne aende akafanyiwe *operation* akaambiwa mkono ule bado haujaingia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana bado madaktari wetu baadhi yao hawako makini. Mtoto huyu sababu ya kuisifia sana Hospitali hii ya Abdalla Mzee mama mtu alichukua hatua ya kumpeleka Abdalla Mzee. Mtoto katiwa piopio jengine na hivi sasa mkono umeshaingia. Lakini hapa Mnazi Mmoja ilikuwa tayari afanyiwe *operation*. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kama hapa kwenye kitengo hiki kuna watoto ambao wanajifunza kazi basi tuwapunguze, tuwaweke watu wazima ambao wanazielewa zile kazi vizuri, lakini tukiendelea kukaa hivi basi tutawaweka wananchi walemavu wengi na sio tegemeo la Rais wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niende moja kwa moja katika changamoto ambazo amezieleza Mhe. Waziri. Tunaamini kwamba Mhe. Waziri utendaji wake ni mzuri lakini hatoweza kutenda yote kama hakupata fedha akaweza kuzitatua hizi changamoto ambazo ameziandika humu. Hizi changamoto ni nyingi, Waziri wa Fedha hayupo, lakini huko huko aliko namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, fedha hizi zote zipatikane ili Mhe. Waziri

aweze kuzitatua changamoto hizi na tusiweze kumlaumu. Kila siku tutaendelea kumlaumu ikiwa fedha hizi hakupata na akaweza kuzitumia vizuri.

Mhe. Waziri nakuomba sana utakapoingiziwa fedha hizi uzitumie kwa mujibu wa utaratibu uliojipangia katika kitabu hichi, vyenginevyo tutakuja hapa hapa na kitabu hiki tutakileta na tutakuja kukusema tena kama ambavyo tunawasema wenzako.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi naunga mkono kwa asilimia 80, nyengine 20 naziweka mpaka Mhe. Waziri atakapokuja kunipa majibu ya kuniridhisha nitaunga mkono kwa asilimia zote. Ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Bahati sasa namkaribisha Mhe. Ali Salum Haji baada ya Mhe. Ali Salum ajitayarishe Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Ali Khamis Bakari.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya. Kabla sijaanza lolote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uhai na kuweza kusimama katika Baraza lako hili tukufu katika kutoa mchango wangu. Pia nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jitihada ya kuongoza Serikali yake na Wizara zake zote za nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wa Wizara ya Afya kwa namna wanavyojitahidi katika utendaji wa kazi zao za kila siku, kama tunavyoelewa sekta ya Afya ni Sekta nyeti ni sekta ambayo kila mwanadamu anaitarajia na anaitegemea. Suala la maradhi ni la kila mmoja, hukuumwa leo utaumwa kesho.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mhe. Rais kwa namna anavyojali taasisi hii kujua umuhimu wake na kwa sababu anavyojali Taasisi hii kujua umuhimu wake na kwa sababu akielewa yeye mwenyewe ni kada wa afya na jitihada zake alizonesha katika maeneo mbali mbali hususan katika maamuzi ya kuweza kuongeza fedha katika maeneo ya madawa kutoka bilioni 7 hadi bilioni 14. Ni jambo jema ni jambo la kupongezwa, jitihada za Mhe. Rais na nina imani kwamba malengo yake na matarajio yake katika kuondosha matatizo ya Wizara hii yafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme tukianza kuzungumzia mapungufu ya Wizara ya Afya na hususan katika hospitali ya Mnazi Mmoja hatuwezi tukamaliza. Kila mjumbe hapa amazungumza kwa hisia kali sana na namna wanavyoona hizi athari au matatizo yanayojitokeza. Nasema ni sehemu nyeti kwa sababu kila mtu anafika na sote tunaona, utaona mapungufu kwenye vifaa, utaona mapungufu kwenye madawa, utaona mapungufu kwenye majengo.

Hata na mimi naweza kusema kuna baadhi ya mapungufu katika maeneo ninataka kuzungumza hususan juu ya wagonjwa waliopata ajali, mara nyingi ukifika na mgonjwa ambaye amapata ajali unakutana na mapungufu mara unaambiwa daktari hayupo, mpaka apigiwe simu uhangaike na kama huna umaarufu kuweza kumpata daktari yule kwa

wagonjwa wa kawaida inakuwa shida, mpaka mtu akisha kuona uliyefika pale Mwakilishi au Waziri ndio watu wanaanza kwenda mbio kumtafuta huyo daktari wa kuja kumtibu mgonjwa. Wakati mwengine unaweza ukafika pale mgonjwa wako anahitaji vyuma unaambiwa vyuma vya viungo hakuna, ukenda kwenye sehemu ya viungo madaktari haba, vifaa vyenyewe vya viungo vimekuwa sinamatatizo havipo vya kisasa, *all most* mambo ni mengi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niwatanabaishe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu ni lazima tuelewe kwamba pamoja na changamoto hizi tunazoziona hivi sasa kwa muda mrefu, Wizara ya Afya tujue kwamba miaka miwili iliyopita hii Wizara iliongozwa na Wapinzani na ilipoongozwa na wapinzani kila mpinzani ana mbinu zake. Mimi nina hofu kwamba waliandaa *strategy* ya *demotion* katika Kitengo cha Wizara ya Afya. Sasa ni jambo ambalo sasa hivi nafikiri tuna haja ya kujipanga kuondosha zile kasoro ambazo wenzetu walizitengeneza.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kujiuliza na wewe utapata tabu namna ya fedha nyingi zinavyopelekwa namna tunavyosomesha watu, kwamba matatizo yamekuwa makubwa na hali imekuwa ngumu. Nasema kwa sababu hiyo alikuwepo Mzee Juma Duni pale, kaondoka akaja sijui Mzee wangu yule Mzee Rashid Seif, ilimradi ile Hospitali imevurugwa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri kuna jambo la kuangalia kwa umakini yale mazalia mazalia tuna hofu kwamba bado Hospitali ya Mnazi Mmoja yamebakia. Lile eneo ni nyeti, eneo la Hospitali linahitaji watu wote, wanaadamu wengi, ukiangalia tu katika maeneo ambayo Zanzibar yanatupa tabu ni yale ambayo jamii ndiyo inayoyategemea yakiwemo masuala ya afya na yakiwemo na masuala ya maji. Haya wenzetu wameandaa *strategy* ya kuyaharibu ili wananchi watoke imani. Sasa leo ndio hapa tunaona haya mashaka, kelele zimekuwa nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, tusaidie kwa sababu Mhe. Hamad Rashid pamoja na kwamba ni kiongozi wa ADC naamini kwamba una uzalendo na una imani na wananchi wa Zanzibar. Tusaidie kama kuna watu ambao bado wanakutu na wana imani kwamba labda watakapoturejesha nyuma wananchi wa Zanzibar labda ndio njia ya kuweza kuipata serikali hii wasahau, Serikali hii wasahau Serikali ya Zanzibar haitoki hivi hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu watajenga imani na Mawaziri na watendaji tutawapa nguvu na mabadiliko tutayafanya kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na jitihada za Mhe. Rais wetu. Niwaombe wanzangu wakupe imani, wakupitishie bajeti, ukatufanyie mabadiliko Hospitali ibadilike na yale mengi ambayo wenzetu waliyafanya kwa makusudi ili kuzorotesha huduma ya afya basi tusaidie mambo yakae sawa. Nina imani kwa uwezo wako na jitihada zako mambo mengi yatakaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie Bodi ya Madawa wenzangu wamemsifu Dkt. Burhani mimi narejea kumsifu tena kwa sababu nimeshawahi kumsifu sana hapa mpaka nikawahi kumwita jina la magufuli wa Zanzibar kama mwenzangu alivyosema hii ni sehemu nyeti. Unajua watu wanaangalia pande moja hawaangalii pande ya pili. Wengi

tunazungumza sana tiba si nzuri, tunahitaji madaktari bingwa wa moyo, lakini haya matatizo yanatokana na lishe. Sasa kama itakuwa tunalishwa mavyakula mabovu sote tutakuwa wagonjwa humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza kwa kufanya jitihada kwa kupambana na watu ambao hawatutakii mema kwa kutulisha vyakula ambavyo havina ubora, mavyakula mabovu na hivi ndio inatuletea athari sasa hivi tumekuwa watu wote Unguja wagonjwa. Mtoto mdogo sukari, mtoto mdogo moyo, mtoto mdogo sijui *pressure* mavyakula hayastahiki. Nimpongeze, mwenzangu alimpelekea katika suala la kwenda kuchunguza vifaa nje, lakini mimi naomba pia aangalie katika suala zima la kwamba wanaoingiza bidhaa Zanzibar kuhakikisha wanasema na maeneo wanayohifadhia bidhaa zao ili kuwa na ukaribu wa kwenda kuangalia bidhaa mara kwa mara katika kushtukiza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili namtahadharisha aangalie lazima mtu anaingiza bidhaa aseme sehemu anayoweka bidhaa ili kwenda mara kwa mara kuchunguza bidhaa. Kwa sababu mara nyingi bidhaa zinazoingizwa Zanzibar ni zile bidhaa za bei ya chini, mtu bado miezi miwili ku-*expire* ndio anatuletea mchele.Sasa wao wapite kwenye maghala kwa sababu wanapokuta vime-*expire* wakati mwengine wanaghushi mpaka vipaketi, ili kuona bei zao bado zinaweza ku-*survive* bidhaa imeshamaliza muda. Nampongeza sana juzi nimesikia kwenye vyombo vya habari wameingia katika maghala wameona michele mibovu, wameona unga mbovu. Sasa nimuombe Mungu amjaalie aongeze kasi na awe na moyo huo huo wa kutokushawishika kwa sababu hiki ni kitengo ambacho rahisi kushawishika ukaweza kuchukua hela ukawalisha watu vyakula vibovu na baadaye ukapelekea wananchi kuwa na maradhi ya aina tofauti sana.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie kuna taarifa kwenye kitabu chao kutaka kujenga jengo la Hospitali kubwa Chakechake. Niwaombe waangalie eneo la Vitongoji kuboresha Hospitali zile baada ya kuangalia uanzishwaji wa jengo jipya, lakini kama kutakuwa kuna muelekeo labda wao wenyewe wameuwona ni bora zaidi kuanzisha Chakechake watakuja kutwambia.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nitaka nimuombe Mhe. Waziri, Mhe. Hamza Hassan Juma wakati anachangia, mengi aliyoyachangia ni mambo ambayo wameyaona katika Kamati ambavyo tuliiunda kupitia *caucus* ya Wawakilishi na Kamati ile ilikuwa ina watu waliobobea, tulikuwa na watu waliopata fani wa udaktari wawili, tulikuwa tuna Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) lakini pia tulikuwa pia tuna Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerey). Tulikuwa tuna watu wanaukaribu wa kufuatilia mambo ya Hospitali, tulikuwa tuna Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Hamza Hassan Juma, tulikuwa tuna Mhe. Khadija Omar Kibano, walipita maeneo tofauti hayo ambayo yanayozungumzwa sasa hivi mengi waliyoyaona, Mahospitali mabovu, vifaa vimechakaa, uhaba wa madaktari, imo kwenye ile ripoti ambayo sisi tumemkabidhi Mwenyekiti wetu Mhe. Makamu wa Pili. Sasa sijua kama Waziri aliyepita kama amekupa ripoti, ile kama hajakupa basi mimi nitakuletea uiangalie na uipitie. Itakuwa ni dira yako ya kuweza kukusaidia kuweza kutatua zile chachu ambazo zimeonekana.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa sababu na mimi nakwenda wakati dakika yangu moja nataka nimalizie kwa wenzangu niwambie tu wengi wapo waliosema kwamba wanazuia shilingi, kwenye mapato, kwenye matumizi, ni haki yao ya msingi siwezi kuwazuia. Ninachowaomba basi pamoja na yote hayo basi tupige buti hata ikiruka kifuani lakini hatimae tuelewe kwamba tunachokizungumza kwamba hii ni Taasisi yetu ya Wizara yetu, ya serikali yetu Serikali ya Chama cha Mapinduzi tukosoe kile ambacho tunahisi pana haja ya kukosoa kwa sababu namuamini Mhe. Waziri na Mhe. Waziri atuletee majibu ambayo yataweza kuwasaidia Wawakilishi na kuwapa taaluma wananchi wetu katika zile kasoro ambazo zinaonekana.

Mhe. Naibu Spika, sina wasiwasi na hayo na Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasi wasi wakaona labda Mnadhimu akianza kusimama hapa anataka kuzuia buti, buti zipo, pigeni buti ndio mpate maelekezo kwa Mhe. Waziri, lakini hatimae tuweze kupitisha bajeti hii. Baada ya hayo naunga mkono kwa hotuba hii kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil nimesema ajitayarishe naona simuoni kwa hivyo nitampa nafasi hii Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami kunipa fursa hii asubuhi hii ya leo kuchangia hotuba hii ya Wizara wa Afya, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu na afya zetu.

Awali ya yote namumshukuru Mwenyezi Mungu name kusimama hapa nikiwa na afya katika Ramadhani hii ya 20 ambayo tunakaribia kumaliza mfungo wa Ramadhani. Nikienda kwenye pongezi za Wizara napenda kuipongeza Wizara hii ya Afya kupitia Waziri wake, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Timu yote na wataalamu wote ambao kwa namna moja au nyengine wanajitolea kufanya kazi ya kujitolea kazi ya afya ni kazi ya kujitolea. Kwa hivyo hongereni san asana.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa hakika sina wasiwasi hata kidogo kwa uteuzi wa Waziri huyu wa Afya namwita kaka yangu ni hodari na ni mahiri na ni makini mno. Naweza nikasema katika Baraza lote hili hakuna mtu ambaye aliyeshika nyadhifa mbali mbali mpaka kufikia hatua hii na anayeijua nchi kama Mhe. Hamad Rashid Mohammed. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamad Rashid ameanza *administration* ya utawala tangu enzi za Mwalimu Nyerere, sisi wakati huo tulikuwa wadogo lakini alibeba dhamana mbali mbali tena za siri, na mpaka hii leo tunae humu ndani, kwa hivyo Mhe. Hamad Rashid hongera sana sana. Mimi mara nyingi nilikuwa namtania kwamba wewe ni Afro Shirazi na huwa anacheka na anakiri kwamba yeye ni Afro Shirazi, kwa sababu historia yake naijua ni Afro Shirazi, hongera sana.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu mimi zaidi nitajikita katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tukiri tu kwamba hii ni Hospitali ya Rufaa, na kimbilio letu sote tuko pale.

Kipindi kifupi tu tangu abebe dhamana hii Mhe. Hamad unafanya vizuri mno tena wala sio kwa ubabe kwa diplomasia yako ile ile ambayo umeanza nayo miaka ya nyuma. Ushauri wangu ni huu ufuatao ambao uzingatie sana kwa maslahi ya nchi yetu wagonjwa wetu na wagonjwa watarajiwa. Tukubali kwamba maji ndiyo hatua ya mwanzo wa msingi wa afya. Hospitali ya Mnazi Mmoja haina uhaba wa maji, kama miaka minne nyuma tatizo la maji limeondoka. Nakushauri haya yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa sasa nyakati za asubuhi tumia wataalamu wako mafundi wa maji *plumbers* wafunge kifaa kinachoitwa *pressure pump* nyakati za asubuhi mahitaji ya maji yanakuwa ni mengi mno, kila mmoja anahitaji maji kusudi kupatikana hiyo afya ya msingi. Tumia wataalamu wako warekebishe huo mfumo wa maji kusudi wagonjwa na wanaolala na wagonjwa kwamba wote maji yanatoka kwa kasi japo mpaka saa 3:30 iwe *pressure pump* inafanya kazi. Hiyo ni haki ya msingi maji katika kutumia mgonjwa huo ni ushauri wangu wa kwanza.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu wa pili kwa ruhusa yako tena ni lazima tukubali kwamba afya ya msingi inatokana na pale pahala ambapo pachafu pafanye pawe safi hata maradhi yanapungua tengeneza utaratibu wa kudumu wa kubadilisha vyoo yaani *toilet* zile kila baada ya mwaka ikibidi hata miezi minane toa vyoo vikongwe weka vyoo vipya kusudi hii ni hospitali ya rufaa wanaokwenda chooni kutumia waone kuna mabadiliko wala haihitaji pesa nyingi hata kidogo.

Ushauri wangu sasa Zanzibar tumeingia na urafiki na Ras el Khaimah, Ras el Khaimah ni miongoni mwa uchimbaji wa mafuta lakini wana *product* nyingi za uchimbaji na kuuza vifaa vya *saranic*, tengeneza utaratibu kila mwaka tengeneza bajeti ndogo ya kununua vyoo viweke kila miezi minane ondoa vikongwe weka vipya utajenga heshima kubwa katika masuala ya usafi katika Hospitali yetu.

Lazima tukubali Mhe. Naibu Spika, sote kimbilio letu liko Mnazimmoja mimi sizungumzii sehemu nyengine mimi niko Mnazimmoja na huijui umuhimu wa Mnazimmoja mpaka uende Mnazimmoja, kwa hali yoyote aidha kwa mgonjwa wako au wewe mwenyewe ufanye *visit* tu wende utaona tengeneza mbiundombinu hiyo Mheshimiwa naamini hapa tulipo tutaondoka. Kwa ujumla huo usafi tunaozungumza hapa basi hauji kama hakuna maji, kwa hivyo wakati unapowasha pampu asubuhi maji watu watatumia, wagonjwa watatumia na wakaguzi watatumia.

Lakini *all in all* Mhe. Waziri na timu yako mnafanya kazi nzuri mno kazi ya kumhudumia mtu huioni umuhimu wake jaribu tu kwenda katika *private* kuona mgonjwa mmoja tu au uwe na *problem* ndogo tu ndani ya mwili wake basi akizidiwa tu anaambiwa nenda Mnazimmoja, na Mnazimmoja bado ni kimbilio letu la wanyonge. (*Makofi*)

Tunaiamini na tunaiamini mno na lazima sote humu ndani tumpongeze Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein namna alivyoibadili Mnazimmoja kwa hali na mali, hongereni sana na unakumbuka Mhe. Waziri ulipoteuliwa mimi nilikuwa mtu wa mwanzo saa tano usiku kupokea simu yangu na nikakwambia kwamba unaweza na unaweza *big up* na timu yako fanya kazi sisi tuko nyuma yako. Tutakupa ushauri wa kitaalamu, wataalamu unao

mabingwa unao, mimi naamini kwa lugha ya leo Wizara hii inatosha kufanya kazi yake apewe mafungu yake yote, isiwemo hata buti mmoja, kasma zote ili mwakani tukija hapa iwe *implementation report* kafanya haya! haya! Karekebisha haya! haya! Unguja na Pemba hongera sana timu nzima ya Wizara ya Afya. (*Makofi*)

Kwa sababu hiyo mimi naunga mkono bajeti hii asilimia 100% apewe fedha afanye kazi tupate afya nzuri. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya mchangiaji anaefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali Ajitayarishe Mhe. Ali Khamis Bakari na kwa kundi la Wajumbe tutamalizia na Mhe. Salma Mussa Bilali.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hutuba hii ya Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya kuchangia na mimi nitoe pongezi zangu kwa Wizara kwa sababu penye kasoro lakini na uzuri upo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kwenye Afya ndio kwenye maisha ya binaadamu, bila ya afya na maisha yanakuwa ni tabu au yanakuwa hayapo. Kwa hivyo mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kitabu chake hichi, ukurasa 54, katika mipango yake aliyosema kwamba ni kusimamia maadili kwa wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, kelele zote zinazokuja maana si kama hakuna kinachofanyika serikali inajitahidi kutoa fedha na sisi ndio tunaopitisha ndani ya Baraza lako hili Tukufu pesa nyingi sana kwa Wizara zote, lakini hususan wizara hii ya Afya Mhe. Panya alizungumza hapa, lakini kusema la ukweli tatizo ni usimamizi, inawezekana kwamba tatizo likawa ni usimamizi kwamba wale waliopewa majukumu yao wanashindwa kuyatekeleza ipasavyo, kwa hivyo mimi namuomba sana sana Mhe. Waziri na mimi namuamini Mhe. Waziri kwa hili kwamba asimamie vizuri ili tuondokane na hizi kelele za kila siku katika vituo vyetu vya Afya pamoja na Mahospitali, hospitali ilioko Mnazimmoja na Chakechake pamoja na Mkoani na hospitali nyenginezo za Rufaa Hospitali za Wilaya na za Mikoa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye DNA, mara hii hatukuona DNA hapa kwenye kitabu hichi, lakini vitabu vingi vilivyopita 2016 - 2017, 2017 - 2018 ilikuwa imo kwa hivyo mimi nilitaka kujua je imeshapatikana au bado? Kama ishapatikana lini itaanza kufanya kazi, kwa sababu Mhe. Naibu Spika ila siku tunapiga kelele kuhusu masuala ya udhalilishaji vijana wetu wanadhalilishwa, kwa hivyo tunataka tuone kwamba kile kichokuwa kwamba tayari kishapatikana kiweze kutumika, kwasababu naona huenda ikawa ishapatikana kutokana kwamba mara hii kwenye kitabu hiki hamna.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 51, walisema kuimarisha utoaji wa huduma katika hospitali na vituo vya afya, wengi wamezungumza kwamba huduma iliyo bora ni kuweko na madaktari pamoja na manesi na watu wengine wakiwemo na ma-*orderly* na watu wengine wanaohudumia.

Mhe. Naibu Spika, ubora huu utapatikanaje wakati kwa huko kwenye hizo hospitali kwenye hivyo vituo vya Afya kuna uhaba wa wafanyakazi ambao ni wataalamu wa sekta hiyo ya Afya.
Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo mimi niombe sana sana Wizara ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma iliyo nzuri ya afya ni kuwa na wataalamu na madaktari bingwa wazuri walioko katika vituo na hospitali zote za Unguja na Pemba, ili kuondokana na hizi kelele.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya vituo vya afya na hospitali nyengine ukenda kuna tatizo kuna vile vifaa tiba ile mikasi imefanya imefanya kutu ni taabu hata kumtibu mtu siku nyengine unaogopa kwa sababu unaona kama ukimtibu utamuongezea maradhi mengi kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, na hili pia naomba sana kwenye hili suala la vifaa tiba pamoja na madawa lipewe kipaumbele.

Kwa sababu Mhe. Hamza alizungumza ni kweli na mimi namuunga mkono, Mhe. Naibu Spika, katika kamati yetu ya Sherehe na Idara Maalum ya SMZ tunashughulikia Halmshauri na Mabaraza ya Miji na Manispaa, tumezitembelea zote Unguja na Pemba na huko sasa hivi ndiko kwenye ugatuzi waliko hao watu wa Afya kupitia vituo vya Afya.
Mhe. Naibu Spika, tatizo hili liko, dawa katika vituo vya Afya haziko inakuwa ni tabu ni mashaka moja kwa moja lakini ukenda ukiuliza Bohari Kuu unaambiwa dawa ziko tele.

Mhe. Naibu Spika, na mimi namuunga mkono Mhe. Hamza kwa asilimia mia 100% ya kwamba ipo haja ya kuunda Kamati ya kuchunguza huko, kwa sababu hizi dawa sio mchele, lakini inawezekana ikawa ni mchele kuna watu maana ukiuza unapata huo mchele sasa. Inawekana kwamba kuna watu wanauza hizi dawa kwa kununua mchele.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana suala hili liangaliwe ili kuhakikisha kwamba ikiwa kuna wabadhirifu ambao wamepewa dhamana zao lakini wanakwenda kinyume na maadili haya basi wachukuliwe hatua kali za kisheria, kwa sababu wananchi wetu wanaumia, wananchi wanateseka wengine wana bima ya Afya watakwenda Global wengine hawana masikini ya Mungu watakwenda wapi watakufa tu. Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, naomba sana.

Mhe. Naibu Spika, moja niende tena kwenye suala hili la kwenye suala lile la vituo vile vinavyouza madawa *dispensary* na vituo vyengine, sifikirii kama wizara ina wataalamu wa kutosha kuweza kupita au sifikirii kama Wizara wanapita mle kwenda kuhakikisha zile dawa. Mhe. Naibu Spika, kuna wengine hawajui *expire date* kwamba hii dawa imetengenezwa lini inamalizika lini muda wake, lakini mtu kama yeye anauza hatoitupa ile siku nyengine atamuuzia mtu atakwenda kutumia kumuengezea maradhi. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja aniambie kwamba ni mara ngapi wamepita kuangalia katika vituo vile *dispensary* zile za binafsi ili kuhakikisha kwamba wanaangalia dawa ziko salama kwa watumiaji wanaopewa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye wizara hii ya afya, Mhe. Naibu Waziri ni shahidi kama ananisikia. Mhe. Mahmoud ndio aliyetoka hapa akawachia

mkono Mhe. Hamad Rashid, Mhe. Mahmoud alikwenda kufungua Kituo cha Afya Ndagani.

Ndagoni kwanza nipongeze sana kwa kufunguliwa Kituo cha Afya Ndagoni ambacho mpaka leo wananchi wangu wa Ndagoni waliokuwa wakipata tabu kwa kufuata huduma ya afya ambacho mpaka leo wananchi wangu wa Ndagoni waliokuwa wakipata taabu kwa kufuata huduma ya afya *kilometre* 9, sasa hivi wamepata huduma ya afya kupitia pale.

Mhe. Naibu Spika, Kituo cha Afya kile kina daktari mmoja aliyekuwepo mmoja Mhe. Mahmoud alimuahidi kwamba atampatia vespa lakini mpaka leo hii daktari yule amewacha kwenda kutokana na ameomba kwamba asaidiwe kwenda kule kwa sababu Mhe. Naibu Ndagoni hakwendi hata Punda, leo siku za mvua anafika kule saa saba.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mahmoud alimuahidi kwamba atampelekea vespa ili kumrahisishia usafiri mpaka leo hii hakuna vespa aliopewa kijana yule na kusema kweli Mhe. Naibu Spika, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, unamtoa mtu Vitongoji unampeleka Ndagoni wakati kwa siku za mvua kule punda hafiki siku kama hizi hapa za jua taabu pia vile vile anashuka Wesha anakwenda kule kwa miguu akifika anakwenda kufanya kazi gani keshachoka.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri aangalie katika kituo kile kuengezwa wafanyakazi wengine ili wananchi wale waweza kupata huduma wakati wowote.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi ya kuongea lakini isipokuwa nataka Mhe. Waziri aje anipe jibu la kwenye DNA kwa sababu imekuwa ni kilio cha Taifa sasa kila siku tukinyanyuka na Mhe. Jaku DNA!, DNA!

Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kutupa majibu anipe majibu hayo ili niweze kumuachia kwa asilimia 80% ambazo asilimia 20% nitazizuia lakini ni kwamba akiwa hakunipa majibu nitapita mabuti. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Suleiman Makame Ali, sasa anaefuata kuchangia ni Mhe. Ali Khamis Bakari baada ya Mhe. Ali Khamis Bakari atachangia Mhe. Salma Mussa Bilal.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako nami kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hutuba hii ya Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyetuwezesha kwa siku ya leo tukakutana hapa, lakini vile vile tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tumalize shughuli zetu salama turejee majimboni kwetu.

Lakini nianze kwa kuwapongeza Wizara wote kwa pamoja, Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya siku hadi siku kuhakikisha kwamba gurudumu hili la Wizara ya Afya linaenda mbele.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile nichukue fursa hii kumpongeza dada yangu aliyekuwepo kuliani kwangu alovaa nguo ya rangi ya kama *blue* hivi kwa kazi kubwa anayoifanya na nimpongeze sana anafanya kazi usiku na mchana. Mimi tulikutana Kangagani katika ufunguzi wa kituo sijui uwekaji wa jiwe la msingi kilichojengwa na Milele, kwa kweli hodari sana huyu dada anafanyakazi kwa kweli anastahiki pongezi za hali ya juu hakai usiku na mchana anahangaika kuona kwamba Wizara yake majukumu aliyopangiwa yanakwenda mbele.

Mhe. Naibu Spika, nianze vile vile kwa kumpongeza Mhe. Hamad Rashid kwa kazi nzuri anayoifanya tumeona kwamba kabla hajakabidhiwa Wizara hii alikuwa anachukua jitihada za makusudi kuhakikishia kwamba hakai kwenye ofisi yake anakwenda katika vituo vyake alivyopangiwa, lakini vile vile anakwenda katika sehemu ambazo anakwenda kutafuta namna ili kujua kwamba wananchi wanahitaji nini kuweza kukwamua.

Nina imani kwamba wizara hii alivyoipata safari hii vile vile kutakuwa na weledi mkubwa na tafanya kazi kwa hali ya juu na akisaidiwa hapa na baadhi ya mawaziri tunaona kwamba kuna baadhi ya mawaziri kwa mfano Naibu Waziri wa Elimu na yeye anajitahidi, rafiki yangu hapa mzee wa Pangawe na yeye halali usiku na mchana akisaidiwa na Mhe. Shamata tunaona jitihada zao, ingawa kuna baadhi ya Mawaziri kidogo wanakuwa katika kazi zao wanaendelea kukaa sana katika maofisi yao, ingawa wengine lazima hawawezi kuondoka lazima wapate ruhusa. Lakini na shemegi yangu Mhe. Juma Makungu akishafika nyumbani tu ndio huwa anajisahau kabisa maji yanaweza yakamwagika nusu saa nzima lakini ukimpigia simu humpati, nimwambie na yeye afanye kazi aje Tumbe aangalie jinsi mambo yanvyokwenda ili aweze kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa kuipongeza serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutujengea vituo katika jimbo langu la Tumbe awali kabla ya Mapinduzi tulikuwa tunahangaika sana lakini kwa juhudi zao kiongozi wetu mpendwa Dr. Ali Mohammed Shein ameweza kutufanyia jitihada za makusudi kuona kwamba jimbo langu la Tumbe limebahatika kupata vituo vitatu ikiwemo pale Tumbe, Shumbaviamboni, na Chimba.

Lakini naomba Mhe. Waziri hapa unisikilize vizuri, ni imani yangu kwamba Tumbe hujafika katika jimbo langu lote kuvitembelea hivi vituo lakini nakuomba tu uje uone jitihada zilizopo ambazo Rais ameshazifanya lakini tu ukikumbuka kwamba katika vituo hivi kuna baadhi ya huduma ambazo hazipatikani kwa wingi zaidi, ikiwemo masuala mazima ya dawa zinapatikani lakini kwa uchache uchache. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba utakapokuja na ukapita kufanya *survey* zaidi utaweza kugundua baadhi ya yale matatizo ambayo yapo katika vituo vile sina haja ya kuyataja yote baada ya siku hadi siku.

Lakini katika kituo changu cha Tumbe kuna tatizo ambalo jengine lile halikuzingatia zaidi watu wenye ulemavu lakini nina imani kwamba jitihada zako zitachukua hatua kubwa kuona kwamba kituo kile nao kinaangaliwa katika hali nzima ya watu wenye ulemavu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije katika kipengele kizima cha hawa wakunga wa jadi, Mheshimiwa mimi nashukuru sana Wizara kwa kupitia serikali wamewatambua watu hawa kuona kwamba wana umuhimu mkubwa wa kuweza kutoa jitihada katika wazee ambao akina mama ambao wanajifungua lakini vile vile wanapata mashirikiano katika kile kipindi ambacho wanakuwa na ujauzito.

Lakini masikitiko yangu ni kwamba watu hawa wanapata baadhi ya mambo nimeyashuhudia katika baadhi ya wengine wana simu wamepewa kwa ajili ya kupata mawasiliano ama na wagonjwa ama kwa kupitia Wizara ya Afya.

Lakini vile vile wanapewa baadhi ya vifaa kwamfano *gloves* na mambo mengine, lakini chakusikitisha Mhe. Waziri watu hawa tumewatupa. Jambo la mwanzo inawezekana kwa mfano mimi pale Kijichame yupo mama mmoja ambaye alikuwa anajishuhulisha sana na shuhuli hizo kapata faradhi kafariki sifikirii kama wizara ya afya wamekwenda angalau kutoa mkono wa pole pale kuweza kutambua juhudi zake alizokuwa nazo, lakini vile vile wale waanchi wakaweza kujua kwama huyu alikuwa na jitahada za makusudi kuweza kusaidia jamii. Kwa hivyo niiombe sana Wizara watu hawa muwatambue vya kutosha.

Lakini vile vile hawa hawa wakunga wa jadi tumeona kwamba wamefungua kama ofisi katika majumba yao ningeiomba Wizara na watu hawa na wao wakawajengea sehemu maalum wakawa kama mfano wa kituo, kama kabla ya yule mgonjwa ama mzazi kwenda hospitali moja kwa moja basi kwanza aweze kupita kwa hawa wakunga wa jadi kuweza kupata ushauri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikwambie kwamba mzazi anapokuwepo huyu mkunga wa jadi basi imani yake inakuwa kubwa na anahisi mimi nitapata mashirikiano ya hali ya juu kuweza kupata afya yangu vizuri, kulikoni hata kama ndani ya kituo patakuwa na yule tunaemwita orderly, yeye ana imani yake basi inampasa kuona kwamba huyu mkunga wa jadi ana jitihada kubwa ambazo anazifanya kuona kwamba anawasaidia watu hawa. Kwa hiyo niiombe tu Wizara tuwaenzi watu hawa ni wazuri sana ili uwafungulie sehemu maalum wajikusanye kwa pamoja ndio watakaposadiana katika ushirikiano wao kuona kwamba wale wazee wetu wanapata kujifungua salama.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije katika Hospitali ya *cottage* ya Micheweni, Mheshimiwa mimi niipongeze sana serikali kwa kupitia Wizara kuona kwamba na sisi katika wana wa Wilaya ya Micheweni tumebahatika kupata jengo lile zuri ambalo linatusaidia takriban wilaya nzima ya Micheweni wagonjwa ambao tunakwenda pale kwa ajili ya kupata huduma.

Lakini masikitiko yangu ni kwamba kuna jengo ambalo lilijengwa pale na jumuiya ya maendeleo ya Konde akiwa chini ya Mwenyekiti Mhe. Omar Seif Abeid, jitihada kubwa zimefanikisha pale kuona kwamba tunaendelea kulifanikisha lile jengo na kuweza kumaliza ili wananchi wanaokwenda pale waweze kupata huduma.

Lakini la kusikitisha jengo lile limefikia asilimia 90% bado asilimia 10 % tu kuweza kuweza kukamika jengo hili limebakia na tukizingatia kuna ahadi ya Rais, ahadi ya Rais alisema kama itakapokamilika jengo hili *inshaallah* nitakuleteni *theatre* lakini na madaktari bingwa. Kwa hivyo Mhe. Waziri nikuombe tu kwamba ile jitihada ambayo wenzetu wameifanya na kufikia hatua ile basi tuenzi ili kuweza kukamilisha pale palibokia na jengo hili kuweza kupatikana ili liweze kutoa huduma kama ilivyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendea niungane mkono na Mhe. Suleiman alisema kwamba kuna baadhi ya vituo ambavyo vinafunguliwa katika vijiji vyetu ambavyo wanaouza dawa zile hawana utaalamu wa hali ya juu. Mimi nitowe mfano hapo zamani wakati mimi ni mdogo zaidi nilikuwa sifahamu kituo cha afya nini kinachouzwa yaani *pharmacy* wala masuala ya kwenda katika mambo ya kupata huduma ya afya. Nilikuwa natumwa tu mimi hebu nenda dukani kanunulie sukari lakini nichukulie na *panadol*. Kwa hiyo nimwambie tu Mhe. Waziri hata viduka vyetu tunavyouza vyakula zimo hizi dawa na wanaouza hizi dawa hawana elimu ya afya. Kwa hiyo ni vyema tukapita katika haya maeneo tukakagua na tukaona kwamba kuna baadhi ya dawa ambazo zimeshapitwa na wakati na bado wananchi wanaendelea kuuziwa wakiwa na wao hawajui lakini hata wale ambao wanauza vile vile wakiwa na wao hawana uweledi mzuri wa kuona kwamba hichi wanachokifanya labda kinaweza kikaleta taathira mbaya.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa sina mengi nilitaka kuchangia hilo lakini nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja anijibu kwamba ni lini kwanza atafanya hii ziara ya kuja hata kama mimi mwenyewe sipo, kuweza kutembelea jimbo langu kujua yale matatizo yaliopo. Lakini vile vile atakapokuja aniambie jengo hili la Wilaya ya Micheweni kupitia wananchi ambao wameshapeleka nguvu zao pale na kuona kuna hali ya kulikamilisha ili tukaweza kupata huduma ni lini litakamilika.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia thamanini na ishirini mpaka nitakapopata majibu nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru mheshimiwa mchangiaji wetu atakayefuata ni Mhe. Salma Mussa Bilali ajitayarishe Mhe. Maudline Castico Waziri wa Uwezashaji, Wazee, Wanawake na Watoto na baada ya hapo atachangia Mhe. JumaAli Khatib Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, Mhe. Salma karibu.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Azza Wa Jaallah aliyetujaalia uzima na leo hii kuweza kusimama katika Baraza lako hili Tukufu na kuchangia hotuba hii angalau machache.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze katika ukurasa huu wa 34 *item* ya 100 ya Upandishwaji Hadhi katika Hospitali za Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niende moja kwa moja katika Hospitali ya Makunduchi. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ameeleza hapa kwamba hatua mbali mbali

zimechukuliwa hadi kufikia hospitali hiyo kuwa na hadhi ya hospitali ya Wilaya ni kweli kuna baadhi ya mambo mengi yamekaa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna mambo madogo ambayo nataka niyazungumze kuna upungufu mdogo wa manesi katika hospitali ile lakini kwa juhudi za Mhe. Waziri najua hilo atalifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna kero katika Hospitali ya Makunduchi na kero hiyo ni ya muda mrefu sana kero ya Hospitali ya Makunduchi ni kero ya uzio. Suala la uzio katika Hospitali ya Makunduchi lina kero kubwa kwa wananchi wa Makunduchi kwa sababu kuna uharibifu mbali mbali unajitokeza kutokana na kukosa uzio katika hospitali ile. Kuna wanyama waharibifu, kuna binadamu waharibifu wanaitumia nafasi hiyo kufanya uharibifu katika hospitali ile. Kwa hiyo imekuwa ni kero kubwa na suala hilo tumeshalizungumza siku nyingi hata Baraza lililopita tumelizungumza sana lakini hadi leo bado hospitali ya Makunduchi haijajengewa uzio.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aatakapokuja anihakikishie kwamba katika bajeti hii ambayo tunampitishia ambayo imeongezwa kwa asilimia kubwa naomba sana suala la uzio katika Hospitali ya Makunduchi alipe kipao umbele ili iweze kweli kuwa na hadhi hasa ya hospitali ya Wilaya Hospitali ya Makunduchi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakwenda katika kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Binguni. Suala la hospitali ya ujenzi wa Binguni nalo limekuwa la muda mrefu, bajeti ya mwaka jana walitumia milioni 135,000,000 lakini kinachonekana ukipata pale ni mabango na baadhi ya nguzo, hatujui nini pesa zile zimetumika kwa hiyo, lakini bajeti ya mwaka huu wamepangia bilioni 14,000,000,000.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze milioni 135,000,000 zimefanyiwa nini halafu pia wamejipangaje katika bajeti hii kuendeleza ujenzi wa Binguni. Ujenzi wa Binguni umekuwa ni kama wimbo wa taifa labda tuseme kwa sababu ni wa siku nyingi umekaa muda mrefu hadi kufikia eneo lile kuvamia likajengwa jengo ambalo silo lilikosudiwa na Wizara ya Afya, lakini kwa bahati nzuri Mhe. Rais amezuwiya lile jengo kwa hiyo naomba akija anaieleze ni lini hasa ule ujenzi au hizi pesa watazifanya nini ili kuendeleza ule ujenzi wa Binguni.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakwenda katika vipau umbele vya wizara nimeona vipao umbele mbali mbali ambavyo wameviweka. Lakini Wizara ya Afya ilitutolea semina sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ya maradhi ya homa ya ini na wametuambia kwamba ni maradhi hatarishi yaani maradhi ya homa ya ini ni maradhi hatarishi ambayo yanakaribina na maradhi ya ukimwi, lakini katika kipau umbele sikuona kwamba ameweka hapa kipau umbele cha kupambana na haya maradhi ya homa ini.

Mhe. Naibu Spika, halafu pia katika kitabu hiki sikuona takwimu hasa jinsi haya maradhi ongezeko la maradhi haya yalipo kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atowe takwimu sahihi ya haya maradhi na ongezeko lake na kuona kwamba

anaipa kipau umbele maradhi haya katika kupambana nayo sawa na maradhi mengine kama ukimwi na maradhi mengine.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo mwisho naomba niipongeze sana Idara ya Kinga katika juhudi zake mbali mbali ambazo zinachukua hasa hasa katika Kitengo cha Elimu ya Afya. Kitengo cha Elimu ya Afya kinafanya kazi zake vizuri, kina elimisha, kina fahamisha wananchi vizuri hadi kupelekea kwamba katika mvua hizi zilizopita hatukusikia kesi nyingi za matumbo wala hatukusikia kesi ya maradhi ya kipindupindu hii inamaanisha kwamba kitengo hiki kinafanya kazi zake vizuri pengine Mkuu wa Kitengo hichi nimpongeze anaonekana ni Mkuu makini na mahiri kiasi kwamba ameweze kumudu kuzuwia maradhi haya. Lakini pia niombe wafanye tena juhudi za makusidi kuhakikisha kwamba maradhi ya miripuko ukiacha haya ambayo tumeyataja maradhi ya mripuko yote wana elemisha wananchi na wanapunguza uingiaji wa maradhi ya mripuko katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naomba kwa niaba ya wanawake Mkoa wa Kusini naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa kuwa muda wenyewe ni mchache naomba niunge mkono hoja, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Salma Mussa Bilali mchangiaji anayefuata ni Mhe. Maudline Castico baada ya Mhe. Maudline Castico atachangia Mhe. Juma Khatib na atafuata Mhe. Mohammed Aboud Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili, naam Mhe. Castico.

Mhe. Maudline Cyrus Castico: Mheshimiwa kwa heshima na taadhima kwanza napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa nafasi ya kuweza kuwepo mpaka wakati huu na pia katika suala zima la ibada inayoendea ambayo wananchi wanaendelea kufunga naendelea kuamini kwamba nawatakia afya ili waweze kumaliza salama.

Lakini pia mheshimiwa napenda nikushukuru wewe pamoja na baraza lako pamoja na watendaji wako wote wanaofanya kazi humu ndani na hasa hawa vijana wanaozunguka wanapotuletea huduma tunawazungusha sana kuwapekea *message* hapa na pale ukipima kilomita wanazotembea hapa ni nyingi sana lakini miye najua kabisa wanafanya kazi na tunawashukuru.

Mheshimiwa kwa heshima pia kabisa napenda nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine na kumshukuru Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi anazofanya kubwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea katika hali ya amani na utulivu. Pia nichukuwe nafasi hii pia kumpongeza mama yetu Mama Mwanamwema Shein kwa jitihada anazofanya kila tunapomuhitaji katika majukumu mbali mbali na hasa pale alipokuwa amezindua zoezi maalum ambalo limefanyika katika nchi yetu la kuhakikisha kwamba watoto wa kike wa miaka kumi na nne wanapewa kinga ya tatizo la shingo ya uzazi, jambo ambalo ni zuri kwa sababu mara nyingi vyema sana kukinga kuliko kuanza kutibu, wengi ambao wanawake wako wengi wanaumwa ugonjwa kwa kansa ambao unahitaji sana msaada.

Lakini pia niseme nipende kuwapongeza watendaji wote wa Wizara ya Afya pamoja na wale wanaofanya kazi katika maofisi pamoja na manesi wanafanya kazi kubwa sana ngumu na wale walioko katika sehemu za uzazi za kuzalisha watoto wanafanya kazi ngumu ambao wahitaji mara nyengine kuvumiliwa kwa sababu mara nyengine wanazidiwa kutokana na kazi walizonazo. Pia nimpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa, nadhani amejibu masuali mengi ambayo yamekuwa yakiruduia rudia katika bajeti zetu zilizopita. Kwa mfano mheshimiwa kwenye suala la DNA ni tayari ameshaeleza jinsi gani DNA ambayo imeandaliwa na kwamba watu tayari wakuweza kutaka kununua wako njiani na pia suala la *lift* kuhakikisha kwamba zinapatikana ili kuweza kuwa ni rahisi kuwahudumia wagonjwa, lakini pia suala la MRA ameweza kulieleza kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia katika ukurasa wa 48 Ujenzi na Huduma za Afya zilizotolewa kumi na tano ni pongezi kubwa kwa Serikali yetu ya Mapinduzi na kwa Uongozi wa Wizara katika kufatilia ni ushindi katika kazi tunazofanya ambazo wanapaswa tuendelee kuwatia moyo ili vituo hivi viendelee kuongezeka mahala pengine. Pia vituo hufanyika kuwa vya rufaa kitu ambacho kinasaidia sana, vituo vinavyokuwa vya rufaa katika Wilaya mbali mbali inapunguza ule mzigo kila mmoja angeweza kukukimbilia katika Ofisi Kuu angeweza kufikia Hospitali ya Mnazimmoja.

Mheshimiwa pia jitihada za uanzishwaji wa chanjo mbali mbali kama nilivyosema pamoja na hata hizi chanjo huenda na sisi zikafika kwetu za kinga ya ukimwi ambao sidhani kama imeshaanza lakini naamini kabisa serikali yetu ikiona kwamba unafaa unaweza kuwa kuingia kwenye masuala ya majaribio.

Elimu ya VVU Mheshimiwa ambayo hadi sasa tunaona kama ni asilimia moja lakini nataka niseme tu wananchi tuwe na tahadhari suala la ukimwi linaendelea na sio suala la kulipuuza. Kwa hiyo nitowe wito kwa wananchi wote kuwa makini katika maisha kuhakikisha kwamba kila mtu ahakikishe kwamba anajikinga ipasavyo na wale ambao tayari wameathirika kuwapa upendo na kushirikiana nao ili wasiweze kuathirika zaidi na kuweza kuambukiza watu wengine. Kwa sababu katika suala hili, linachangia katika suala zima la kuleta yatima katika nchi linafifirisha nguvu kazi na kwa kweli nchi yetu pia bidii ya kuhakikisha kwamba mambo haya yanapatikana katika chanjo na sisi tuweze kushirikiana na mataifa mengine.

Naipongeza serikali yetu kwa sifa hizi ambazo hii kwani ni sifa kwetu sote hasa pale tunaposifiwa sana kwenye suala la malaria. Malaria imepingua sana katika nchi yetu na watu wengi wanashangaa lakini ni mashirikiano pia ya Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba watendaji wake wamekuwa wakifuatilia kwa karibu na kwa wageni utaona kwamba kama magonjwa mengine yanavyoingia tunapopata wageni, ni vyema wageni wetu wanapokuja tuweze kuwa karibu nao kuhakikisha kwamba wanapata matibabu ya malaria mapema kabla hawajaiacha katika nchi yetu. Naamini kabisa kwamba lengo la taifa lolote lile ni kuona kuwa wananchi wake wanalindwa mali zao kwa amani na afya haitaki watu wapoteze maisha hata kidogo.

Katika hili nataka kuzungumzia suala zima la wanawake ambao kwa kawaida wanapaswa wakiolewa wapate watoto na kila mmoja anatarajia mama akiolewa apate mtoto na katika mazingira ya kupata mtoto wengine wanaolewa wakiwa na umri mdogo, wengine wanaolewa wakiwa watu wazima lakini suala zima la kufanya kwamba mama pale anapopata kuwa mjamzito ni vyema sisi wote wananchi tunapokuwepo katika maeneo yetu katika familia tuhakikishe kwamba mama huyu analindwa ipasavyo...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri naomba ukae kidogo. Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa utulivu wenu katika kipindi hiki ambacho nimekuwa nikiendesha kikao na sasa hivi nitampisha Mhe. Spika, aweze kuendelea na shughuli hii.

Lakini kabla ya kumpisha Mhe. Spika, naomba nitowe tangazo hili ambalo limeletwa na Makamu wa Pili wa Rais na kuwataka Waheshimiwa Mawaziri wafuatao waende katika ofisi yake hapa Barazani baada ya kuakhirisha Baraza nao ni.

1. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
2. Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda
3. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati
4. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi
5. Mhe. Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Ahsanteni sana Mhe. Spika karibu.

(Hapa Mhe. Spika Zubeir Ali Maulid alikalia kiti)

Mhe. Spika: Tunaendelea waheshimiwa.

Mhe. Maudline Cyrus Castico: Mheshimiwa nilikuwa naendelea kwenye suala zima la wakina mama wapopata ujauzito nikitaka tu kutoa ombi kwa wananchi kuhakikisha kwamba mama anapopata ujauzito ni vyema watu wakawa karibu naye kuhakikisha kwamba anapata huduma zote husika. Sasa hivi kuna utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba wanaume na wao wanakwenda *clinic* pamoja na wake zao ili waweze kupewa mafunzo namna gani wanaweza kuwahudumia watoto.

Lakini pia ni kuhakikisha kwamba wanapata hudma ya kupata chakula bora, wanapata lishe na pia kuhakikisha kwamba wanahimizwa kuhakikisha kwamba wanakwenda hospitali ili kuangalia ratiba na taratibu nzima za kutaka kupata watoto, kwa sababu inatisha kabisa mheshimiwa kuona kwamba kina mama wanapokwenda kuzaa wanapoteza maisha, wanapoteza maisha katika mazingira ambayo yangeweza kuzuiliwa na wanaacha watoto wakiwa ni mayatima halafu wengine ni wadogo kabisa katika mimba za mwanzo, wengine wanapata ugonjwa wa fistula ambao niseme tu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mwenyewe kuhakikisha kwamba wanaweza kupata matibabu waliopatiwa kwamba Dar es Salaam kwenye *CCBRT* wanafanyiwa *operation* na wanakaa katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nisingependa kusema sana lakini nipende pia kuwashukuru wananchi kuhakikisha kwamba tumejitahidi sana katika suala zima la kuzuia masuala ya mripuko ambayo ni maambukizi ambayo yanatokana na mazingira wengine hatuwi makini tunaacha mazingira yetu yanakuwa machafu, tuendelee kushikana kuhakikisha kwamba tukifanya hivi tunapunguza bajeti isiyokuwa na muhimu kwenye wizara yetu ya Afya. Pia mheshimiwa nipende tu kusema kwamba mimi kwa pamoja kwa nafsi yangu napenda nichangie kuhakikisha kwamba bajeti inapita kwa asilimia mia moja, lakini nawashauri wenzangu wote waatakapokuwa wanachangia waiweze kuiunga mkono ili iweze kufanya kazi kwa sababu ina majukumu mengi na bahati nzuri inaendelea kufanya vizuri na kwa ajili ya uongozi wa Mhe. Rais wetu tumefikia mahali ambapo tunastahili heshima kwa nchi yetu.

Baada ya kusema hayo nachangia asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Maudline Cyrus Castico Waziri wa Jinsia naomba sasa nimwite Mhe. Juma Ali Khatib atafuatiwa na Mhe. Mohammed Aboud kabla sijamwita Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Juma karibu.

Mhe. Juma Ali Khatib: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kutoa mchango wangu.

Mhe. Spika, kwanza napenda kuwapongeza wawakilishi wote waliochangia hotuba hii ya Waziri wa Afya.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamechangia hotuba hii kwa hisia kutokana na hali halisi ya afya kwa Wizara ya Afya. Kwa kweli wameonesha hisia zao kubwa sana, lakini na mimi nataka kuwaambia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba pamoja na yote waliyozungumza na changamoto zote walizozionesha, kwanza ni haki yao ya msingi ya kikatiba, sheria na kanuni. Lakini mwisho wa siku lazima sisi sote tujue kwamba tupo hapa kwa sababu ya kupitisha bajeti ya Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, bajeti hii ni ya serikali na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo kwa ajili ya Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi ndicho kilichounda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tusisahau hilo kwanza hapo. Halafu jambo jengine Mhe. Spika sisi sote hapa katika Baraza hili lako tukufu, Baraza hili halina kambi ya upinzani, ingawa kuna wawakilishi watatu wanatoka kambi ya upinzani nikiwa mimi Mhe. Juma Ali Khatib, Mhe. Hamad Rashid Mohamed na Mhe. Said Soud Said lakini tupo hapa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Spika, hotuba hii si yake binafsi Mhe. Hamad Rashid Mohamed, hotuba hii ni ya serikali kupitia Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, nawapongeza wale wawakilishi wote waliochangia, lakini nataka kuwasihi jambo moja kwa namna moja au nyengine serikali imepiga hatua kubwa sana kwa Wizara ya Afya. Mhe. Spika, jambo hili halitaki tochi ukiangalia nchi za wenzetu na sisi Zanzibar tulivyo tuko tofauti sana na tuko mbali sana.

Mhe. Spika, tulikotoka na sasa tulipo tupo mbali sana. Kwanza mimi nataka kuwapongeza Wizara ya Afya, Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu na

Wakurugenzi wote na uongozi wa hospitali ya Mnazi Mmoja na Afisa Mdhamini Pemba. Mhe. Spika, kwa kweli serikali yetu imefanya juhudi kubwa sana, walichokisema wawakilishi ni changamoto ambazo zipo, lakini sisi sote tuna wajibu wa kupambana na changamoto hizi.

Mhe. Spika, si suluhisho kuondoa mafungu kwenye kitabu hiki, si suluhisho. Mhe. Spika, haya yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wawakilishi majibu yake yako humu. Sasa tukikubaliana tukapitisha bajeti hii ndio mafanikio kwa hayo malalamiko waliyoyasema na changamoto walizozitoa hapa. Ndio maana nikasema kwamba Baraza hili halina kambi ya upinzani, nikimaanisha kwamba sisi sote tunatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, madaktari wetu wanafanya kazi kubwa sana lazima tuwapongeze. Tukiangalia Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu hospitali ukipiga hesabu kwa takwimu Unguja na Pemba si chini ya watoto 100 wanazaliwa kila siku. Ukitizama kwa mwezi utapata watoto 3000, ukitizama kwa miaka mitano si chini ya watoto watakaozaliwa 180,000. Sasa kama hivyo ndivyo ina maana sisi tuna ongezeko kubwa sana la watu na huduma zetu serikali inajitahidi kila baada ya mwaka kuongeza bajeti. Ukitizama bajeti iliyopita mwaka jana na mwaka huu ni tofauti, sasa hili nalo sisi kama Waheshimiwa Wawakilishi tuna jukumu katika kusimamia uzazi wa mpango.

Mhe. Spika, serikali ilikuwa inatoa elimu ya uraia kwa huduma ya uzazi wa mpango. Sasa ukipiga hesabu Mhe. Spika ongezeko kila mwaka watoto wakizaliwa madaktari wao ndio wana jukumu la kuwatibu hawa watoto. Mhe. Spika, pia ukitizama uwezo wetu wa kifedha pamoja na kwamba ni mdogo, lakini serikali imekuwa inabana matumizi makubwa sana kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, na sisi tumebahatika kwamba tuna Rais ambaye kabobea katika mambo ya afya, ni daktari wa binadamu. Kwanza Rais Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ana uchungu mkubwa sana na wizara hii kwa sababu ndio kazi yake na ndio fani yake. Tunapokuwa katika vikao vya serikali mara nyingi unamuhisi kwamba ana hisia sana. Kwa hivyo, nataka niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tumuunge mkono Rais katika kazi yake ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata huduma bora ya afya.

Mhe. Spika, tulipo tupo pazuri sana ukitembelea vituo vya afya madawa yapo. Mhe. Spika, mimi na mwenzangu Mhe. Said Soud Said mwezi wa nne tulifanya ziara Pemba, tulikwenda hospitali zote za kule Pemba karibu nyingi tu. Tulikwenda Kisiwapanza, tulikwenda kituo cha afya pale Michenzani, tulikwenda Abdalla Mzee Hospital. Mhe. Spika, juhudi kubwa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pale hospitali ya Abdalla Mzee tuna vifaa vingi na tuna madawa mengi. Msemaji mmoja hapa aliipongeza sana Wizara ya Afya kupitia hospitali ya Abdalla Mzee, lakini si Abdalla Mzee tu hata Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, tatizo letu ni kwamba sisi wenyewe tunazaa sana na tumeongezeka sana, hatufikirii hilo na kila tunapozaa tunawabebesha wale madaktari wale wachache tulionao

tunawabebesha kazi ya kututibu. Kwa hivyo, nawasihi wenzangu kwamba tulitizame vizuri suala hili la uzazi wa mpango pia litatusaidia huko mbele.

Mhe. Spika, tunashuhudia kwamba madaktari wetu wanafanya kazi usiku na mchana, na wale wauguzi nao wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kuna msemaji mmoja hapa alikuja akasema kwamba iweje wale wanaosafisha wanaokwenda usiku. Hebu Mhe. Spika itizame hospitali ya Mnazi Mmoja saa 12 ukifika pale asubuhi watu wamejaa tele. Watu wanakwenda kuangalia wagonjwa kile kitanda Mhe. Spika mgonjwa anaumwa lakini kazungukwa na watu zaidi ya 40. Baada ya hapo madaktari wanapita kufanya ukaguzi, hebu tujiulize saa ngapi yule anayekwenda kusafisha atafanya usafi kama si usiku. Kwa hivyo, hili pia tulitizame kwa sababu hili tusimuoneshee kidole Waziri wa Afya au Naibu Waziri wa Afya au uongozi wa afya.

Mhe. Spika, hili ni letu sote na ni jukumu letu sote tutafakari vipi tutalibeba na vipi tutalitatua. Tulipo nasema tena tupo pazuri pamoja na takwimu hizi nilizozitoa hapa kwamba kuna ongezeko kubwa sana jinsi vizazi vinavyoongezeka *alhamdulillah* tumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia Mhe. Spika tuna wageni wengi wanatoka nje ya visiwa vya Unguja na Pemba wanakuja kufata matibabu mazuri. Wizara ya Afya hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Spika kuna watu wanatoka Bagamoyo, kuna watu wanatoka Tanga, kuna watu wanatoka Dar es Salaam, kuna watu wanatoka Comoro, kuna watu wanatoka mpaka nchi za jirani Mombasa na Kenya. Kwa hiyo, wanakuja hapa kwamba hospitali zetu zina huduma nzuri.

Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba hapa Waheshimiwa Wawakilishi nawaheshimu sana…

Mhe. Spika: Una dakika mbili mheshimiwa.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Michango yenu ni mizuri sana na naungana na nyinyi sana wala siwadharau ni majukumu yenu na mmeonesha mfano na mmeguswa sana, lakini mwisho wa siku sisi ndio wenye bajeti hii serikali, Baraza la Wawakilishi ni sehemu ya muhimili wa serikali. Maneno yenu na changamoto mlizozitoa serikali imesikia. Kwa hivyo, kwa pamoja sasa tupitishe bajeti hii, tupitishe mafungu haya, tumpe Mhe. Waziri pesa hizi aende akafanye kazi na sisi vile vile tuhamasishe katika vituo vyetu vya afya.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni Mhe. Shamata Shaame Khamis anajitahidi kule katika kituo chake cha Micheweni. Jana kupitia mfanyabiashara Said Nassir Nassor (Bopar) tumeona pale kapelekewa vitanda 20, magodoro 20, mashuka hizi ndio juhudi kwamba na sisi hili ni letu kwa namna moja au nyengine tuchangie kuboresha na tuwape moyo madaktari, tuupe moyo Mhe. Spika, uongozi wa Wizara ya Afya, tukisema tu kila siku tunawalaumu, tunawalaumu kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki. Ni wajibu wao wawakilishi kuonesha mapungufu kama walivyoonesha, nawapongeza sana lakini mwisho wa siku Mhe Spika, tuungane sote kwa pamoja tupitishe bajeti hii.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono mia kwa mia hotuba hii na nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tumpitishie Mhe. Hamad Rashid Mohamed bajeti yake akafanye kazi na wataalamu wake. Ahsante Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha, nimshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya na Naibu wake na watendaji wote kwa namna walivyowasilisha hotuba nzuri ya bajeti yenye mwelekeo inayoonesha wazi dhamira ya serikali katika kukidhi haja ya huduma za afya nchini. Aidha, nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kuwapongeza sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Kama alivyosema ndugu yangu Mhe. Juma Ali Khatib Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum kwamba Waheshimiwa Wawikilishi wameonesha hisia zao za dhati katika kutetea wananchi kwa msingi wa kuimarisha huduma za afya nchini. Mimi niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba dhamira yenu, nia yenu ndio hiyo hiyo ambayo serikali inayo katika kuhakikisha tunaimarisha huduma za afya nchini.

Mhe. Spika, ni kweli baadhi yetu tumesema kwa hisia kali sana, lakini dhamira ni kutaka kuimarisha zaidi huduma za afya. Kama alivyosema ndugu yangu Mhe. Juma Ali Khatib na dhamira ya serikali ni hiyo hiyo ya kutaka kuimarisha huduma za afya. Hata ukitizama bajeti yetu kwa mwaka huu katika sekta ya afya tuko zaidi ya bilioni 107, kutoka bilioni 82 hiyo ni zaidi ya asilimia 31 ya nyongeza katika fedha za bajeti. Maana yake ni kuwa serikali inaelewa na wizara husika inaelewa kwa kina matatizo yanayowagusa wananchi katika sekta hii. Serikali ingependa sana kuongeza bajeti zaidi lakini kama mnavyojua kutokana na hali yetu, uwezo wetu wa kiuchumi hapo ndio tutapoweza kujibana na kufikia hatua hii. Naamini sana kwa kiasi kikubwa sana tutasaidia na mabadiliko makubwa hususan yale ambayo waheshimiwa mmeyaeleza yatajitokeza kuhudumiwa zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa dawa mwaka uliopita wa 2017-2018 zilitengwa bilioni 7, lakini mwaka huu 2018-2019 zimetengwa zaidi ya bilioni 12.7 zaidi ya asilimia 40 nyongeza yake. Hiyo ni kwamba dhamira ya serikali ni kuhakikisha madawa yanakuwepo katika hospitali zetu na vituo vyetu vya afya. Serikali itaendelea kufanya hivyo kadri ya uwezo utakavyoongezeka ndipo tutakapozidi kuimarisha huduma hiyo.

Mhe. Spika, vile vile katika hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja ambayo imekuwa kilio kikubwa, serikali imeliona hili kwenye zile kazi za kawaida mwaka jana ilikuwa ni bilioni 1.3 lakini mwaka huu serikali imetenga bilioni 4,378 kwa ajili ya Mnazi Mmoja. Pamoja na mishahara kwa Mnazi Mmoja ni zaidi ya bilioni 14 kwa Mnazi Mmoja peke yake. Kwa hiyo, serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba tunaimarisha hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, lakini tunaimarisha na hospitali zetu nyengine pamoja na vituo vyetu vya afya.

Mhe. Spika, dhamira ya serikali kwa sasa zile zilizokuwa hospitali za Wilaya zipandishwe hadhi na kuwa hospitali za Mikoa, na zile zilizokuwa hospitali za vijiji cottage hospitali kuwa hospitali za Wilaya. Pamoja na kuifanya hospitali ya Abdalla Mzee kuwa kama hospitali ya rufaa kwa Pemba. Na pia jitihada zinafanywa kujenga

hospitali kubwa huko Binguni Unguja kuongezea jitihada hizi ambazo zinafanywa katika kuimarisha hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, tunaelewa changamoto zilizopo ni kweli zipo nyingi na kubwa, lakini katika kuzitatua hizo katika fedha za maendeleo zilizopangwa kwa mwaka huu ni zaidi ya bilioni 48. Katika hizo karibu bilioni 16 zinatoka SMZ, bilioni 10 ni mkopo na bilioni 22 tu ndio kutoka kwa wahisani. Kwa hiyo, ni jitihada kubwa zinafanywa ili kuimarisha sekta yetu hii ya afya tuweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na maana yake ni kwamba serikali inasikia kilio cha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kuimarisha utoaji huduma bora katika hospitali zetu na vituo vya afya ili wananchi wetu wapate huduma bora na kwa wakati.

Mhe. Spika, serikali itaendelea kuwaajiri madaktari na wahudumu kwa nia ya kukidhi mahitaji, na mwaka huu Mhe. Waziri wa Afya ameelezea kwenye bajeti yake idadi ambayo madaktari, wahudumu na wafanyakazi wa sekta ya afya watakavyoajiriwa. Vile vile Wizara yetu ya Afya imo katika utaratibu wa kuanzisha namna ya kuhudumia wale wagonjwa wenye bima za afya. Msingi wake ni kuwa na wenye bima ya afya sasa kwenye hospitali zetu ziweze kutoa nafasi hiyo.

Mhe. Spika, vile vile tunaendelea kuimarisha huduma za maabara, huduma za uchunguzi na kuhakikisha kwamba tunasimamia sasa maadili ya kufanya kazi katika sekta ya afya hasa kwa madaktari wetu na wahudumu wetu. Hapa Waheshimiwa Wajumbe jambo hili lazima tushirikiane maana madaktari hawa, wahudumu hawa ni watoto wetu, ndugu zetu, marafiki zetu, majirani zetu kuna kila sababu ya kuwaeleza na kufahamu juu ya namna ya kuhudumia ndugu zao vizuri zaidi hii kazi ni ya kujitolea ijapokuwa serikali inafikiria zaidi kutenga fungu kubwa zaidi kwa maslahi ya madaktari wetu na wahudumu wetu, lakini bado unapotoa huduma bora kwa mwanadamu mwenzako Mwenyezi Mungu anakutengea fungu kubwa zaidi, kwa leo duniani na kwa kesho akhera unakokwenda. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kuambizana kuacha kuwanyanyasa wagonjwa wanapokwenda hospitali, kwenye vituo vya afya ni ndugu zetu, watoto wetu, ni Wazanzibari wenzetu tuna kila wajibu ya kuwapa huduma bora, huduma rafiki za unyenyekevu na uadilifu wa hali ya juu, ili kila mmoja hata hajatibiwa ajihisi amepona. Si vizuri hata kidogo kwenda katika vituo vyetu vya afya ama hospitali zetu ikawa yupo miongoni mwetu mtoa huduma akazitoa kwa kebehi, jeuri na kiburi haitusaidii sote. Kwa hiyo, tuna kila wajibu kwa sote kushirikiana katika kuwaelewesha wenzetu na wenzetu wakaelewa.

Mhe. Spika, naelewa wapo madaktari wanafanya kazi nzuri sana, wapo wahudumu wanafanya kazi nzuri sana katika mazingira magumu tunawapongeza sana na waendelee na imani hiyo na Mwenyezi Mungu atawasaidia mambo yao yawe mazuri zaidi. Aidha, serikali inachukua jitihada kubwa zaidi sasa licha ya kuimarisha Bohari Kuu la madawa Zanzibar kuna mpango mkubwa wa kuanzisha Bohari Kuu la Madawa kwa upande wa Pemba. Kwa hiyo, kila kinachofanywa Unguja na Pemba kinafanywa ili huduma ziwafikie walengwa kwa ukamilifu wake.

Mhe. Spika, halikadhalika wizara yetu hii na serikali kwa jumla inajipanga katika kujenga nyumba za madaktari na wahudumu wake katika maeneo mbali mbali yaliyo

karibu na hospitali zetu na vituo vyetu vya afya. Yote hiyo ni dhamira njema ya serikali yetu lakini ni imani kubwa aliyonayo Rais wetu kwa wananchi wake wa Zanzibar na yeye ndiye wakati wote anasema kwamba tuhakikishe huduma za afya Zanzibar zinatolewa bure, anafanya kila jitihada kuhakikisha kila mpango kuimarisha huduma hiyo na wananchi wazipate bila ya malipo yoyote; kuendeleza ile sera yetu ya msingi ya tokea Chama cha Afro Shirazi na Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Kwa hivyo, ni imani yangu kabisa Waheshimiwa Wajumbe wataiunga mkono kwa ukamilifu wake bajeti hii ili kuhakikisha tunaipitisha kwa dhamira ya kuwasaidia wananchi wetu. Nataka niwaambie siku nyingi tulilizungumzia suala la *lift*, karibuni suala la *lift* ya Mnazi Mmoja litakuwa historia. Nia ya serikali ni kununua *lift* mpya pale kwa hivyo, sasa tutakuwa na *lift* mbili si muda mrefu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mambo mengi yanafanywa katika kuimarisha sekta hii ya afya, mafunzo ya madaktari, ya wahudumu, wafanyakazi na kadhalika na hata usafi katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja na hospitali nyengine mtapokwenda mtaona mabadiliko makubwa. Naamini sana Waheshimiwa Wajumbe waliyoyaizungumza serikali imeyazingatia tutakwenda kuyafanyia kazi zaidi na naamini kabisa Mhe. Waziri, Hamad Rashid Mohamed; Mhe. Naibu Waziri, Bi Harusi Said Suleiman; Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Afya wana dhamira na lengo jipya la kutoa huduma zaidi za afya kwa wananchi wetu. Tuwatakie kheri, tuwatakie mafanikio bajeti yao ipite vizuri wakafanye kazi nzuri zaidi.

Mimi kwa upande wangu naiunga mkono bajeti hii asilimia mia moja na naomba Waheshimiwa Wajumbe tuunge mkono ili kuweza kutoa huduma zaidi. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Khadija Omar Kibano: Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ajira kwa wanafunzi waliokwisha kusoma na wapo nje na hajaajiriwa, katika hospitali zetu za Pemba za mikoa na wilaya na vijijini, kuna uhaba wa madaktari katika kutembelea maeneo hayo. Afisa Mdhamini wa Pemba ana uhaba wa wafanyakazi mbali mbali, kwa mfano madereva, fundi, wakaguzi, walinzi na kadhalika na hao ni 276 wapatiwe ajira. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti ushauri wangu kwa Mhe. Waziri naomba waombe uwajiri kwa kuwa wafanyakazi wetu ni kidigo sana.

Mhe. Mwenyekiti, vifaa hospitali nyingi za vijijini vifaa vya kutumia ni chakavu, kwa mfano mikasi, koleo na vyenginevyo vinavyohusiana na hivyo. Mhe. Waziri katika jimbo langu kuna vituo viwili vya uzazi kituo cha Uondwe na Mzambarauni, havina vifaa vya kutosha. Vile vile, naomba kupatiwa nyumba ya daktari hakuna katika vituo hivyo, daktari ni mmoja tu na analala mbali na kituo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aongeze madaktari katika hospitali ya Vitongoji, Wilaya Chake. Pia naomba aongeze madawa katika hospitali za Jimbo la Ole. Vile vile namuomba afanye ajiri za wafanyakazi hasa maodali. Mwisho namuomba kuondowa wafanyakazi wazembe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia katika sehemu ya huduma za kinga dhidi ya maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma.

Kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya na timu yake yote kwa kujitahidi katika kuisimamia vizuri hospitali mbali mbali nchini ikiwemo Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ni hospitali ya rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikiha kuwa elimu dhidi ya UKIMWI inaendelea kutolewa kwa kasi kubwa zaidi, ili wananchi waweze kukumbushwa athari za ugonjwa huo thakili, ambao umekuwa ukiua wananchi wetu siku hadi siku. Kwa hivyo, ni vyema wizara ikaendeleza na ule utaratibu wa kutoa elimu hiyo kwa kutumia semina na kupita mjini na vijijini, ili kuwafikia wananchi wetu kirahisi. Ni vyema viongozi wakatilia mkazo kuwa UKIMWI Zanzibar bado upo na unaendelea kuua wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya afya dhidi ya malaria ni vyema ikatiliwa mkazo kutolewa kwa wananchi wetu ni vyema wananchi wasiridhike na hali nzuri ya kutokomeza malaria iliyokuwepo sasa, ila ni vyema wananchi waendelee kuweka mazingira safi ili mapambano dhidi ya malaria Zanzibar yaimarike zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono. Ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuchangia sehemu zifuatazo:-

i Sera ya Afya kwa wageni
ii Theater Lamp
iii Ukosefu wa *Films* za *X-Ray*
iv Majibu ya *HIV* - Kuchelewa.

Mhe. Mwenyekiti, Sera ya Afya kwa Wageni. Nataka kujua hatua ya wizara katika upatikanaji wa Sera ya Afya kwa Wageni imefikia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, Theater Lamp katika Hospitali ya Kivunge karibu mwaka sasa taa hii imeharibika. Kwa hiyo, naomba wakati atakapokuja kufanya majumuisho naomba ufafanuzi anielimishe wizara yake itachukua hatua gani za dharura kurudisha hali hio.

Mhe. Mwenyekiti, ukosefu wa *films* za *X-Ray* kuna tatizo kubwa tena la muda mrefu sana la ukosefu wa *films* za kupelekea wagonjwa wanapopelekwa kwenye upereshen na dokta apatikane akasome pale pale, hii ni hatari sana. Nataka kujua hatua ya serikali kurejesha huduma hii.

Vile vile kuhusu majibu ya *HIV*, kuna tatizo la kuchelewa kwa majibu ya wanaopima *HIV* kwa muda mrefu sana, nataka kujua hatua ya serikali ya kuondoa tatizo hili.

Mwisho naiomba wizara kuipatia gari Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa ajili ya kuongeza kasi ya kufanya doria za mara kwa mara, ili majukumu yao yatekelezeke vizuri zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa ulimwengu aliyetuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema. Vile vile, nampongeza sana Mhe. Rais kwa nia njema ya kuendeleza sekta hii ya Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, kwanza naaza kuchangia mradi wa kupandisha daraja Hospitali za Wilaya kwenye kifungu cha 100.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipofunguwa Baraza la Wawakilishi Novemba 11 alisema naomba kunukuu, "Hospitali zilizo katika kiwango cha Cottage za Micheweni na Vitongoji kwa Pemba, Makunduchi na Kivunge kwa Unguja nazo zitapandishwa daraja, ili zifkie hadhi ya kiwango cha hospitali za wilaya", Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, wafanyakazi wakukidhi, suala hili sio kweli kwa sababu siku zote tunalizungumzia suala la madaktari wa upasuaji hakuna. Je, Mhe. Waziri ni lini daktari huyo atapelekwa hospitali ya Kivunge.

Mhe. Spika, nazungumzia kituo cha Afya cha Chaani Masingini, kituo kile wamejenga wananchi kwa ajili ya kuondoa usumbufu wa kufatilia huduma ya matibabu Gamba na Chaani. Mhe. Spika, wanawake wale wamebeba mawe kutoka Kandwi ili kupata kituo chao, kwa bahati mbaya kituo kile kimepata matatizo la kuliwa *hardboard* na mchwa.

Mhe. Waziri aliyepita na alikiona kituo kile hadi leo hakijafanyiwa ukarabati. Je, naomba kumuuliza Mhe. Waziri ni lini atakitembelea na kikifanyia ukarabati kituo cha wananchi wa Chaani na wao wapate huduma ndani ya shehia yao.

Mwisho, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, naunga mkono hoja hii asilimia thamanini mpaka anijibu masuala hayo. Ahsante.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Waziri kwanza nakupongeza sana kwa umahiri wako ubunifu, ushupavu na usimamiaji wako wenye kuleta tija kwa Wizara ya Afya.

Pili, nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kutujengea kituo cha afya cha kisasa, pamoja na nyumba ya kisasa ya daktari katika shehia ya Sizini katika jimbo la Wingwi Pemba. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awajulishe wananchi wa shehia ya Sizini lini kituo hicho kitafanyakazi.

Vile vile, naomba kumkumbusha Mhe. Waziri ombi la Mkuu wa Wilaya ya Micheweni alililiomba siku ya kuweka jiwe la msingi kwamba kutokana na wingi wa watu wa shehia hiyo itabidi paongezwe wafanyakazi wawili na waajiriwe kutoka shehia ya Sizini.

Mhe. Spika, kuhusu madaktari wazoefu, wanakawaida wanapopata madaktari wapya katika vituo walimu yaani katika vituo wanavyofanya kazi wazoefu hao huwaachia kazi za kutibu wale madaktari wapya ambao wanatoka chuoni sasa. Hili ni tatizo ambalo hupelekea wagonjwa kupata athari za nyongeza hasa katika utumiaji wa sindano. Kutokana na hali hiyo, naomba mtindo huu wakumbushwe wafanyakazi na pia naelewa kuwa wanapatiwa mafunzo kila mara, lakini asichoke kuwahimiza na kuwakumbusha.

Mhe. Spika, pia tunao vijana ambao wamefanyakazi ya kujitolea na ambao wameshasoma katika vyuo mbali mbali vya afya vinavyotambuliwa vilivyopo hapa Tanzania, lakini jambo la kusikitisha vijana hao mpaka leo hawajapatiwa ajira na huku kila kituo cha afya kina upungufu wa madaktari, naomba ili likumbukwe na lizingatiwe.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mgaza Jecha: Kwanza napenda kumshukuru Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Naibu wake pamoja na watendaji wake wote wa wizara, pamoja na pongezi za kazi.

Kwanza naungana na Mhe. Waziri aendelee na kusimamia wizara hii kwa umakini sana, kwa sababu wizara hii ina shughulikia masuala ya matibabu kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuumba, viumbe vyote na nchi. Pili nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kusimamia vizuri serikali yake kwa amani na utulivu.

Vile vile, napenda kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya kwa hotuba yake nzuri ambayo imejibu maswali mengi ambayo yamekuwa yakijirudia rudia katika *budget* zetu kama swala la *DNA, lift, MRI* na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 48 Ujenzi wa Huduma za Afya vituo 15 ni ushindi katika kuendeleza kutoa huduma muhimu na pia vituo vyengine kufanyika vya rufaa, pongezi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na uongozi wa hospitali.

Kuhusu jitihada za uanzishaji wa chanjo za saratani ya shingo ya kizazi kwani kukinga ni bora kuliko tiba kwenye ukurasa wa 6.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya VVU ambayo hadi sasa ni asilimia moja. Naomba kuendelea kutoa wito kwa wananchi kuwa makini katika maisha ya kila siku ugonjwa huu tusipozingatia elimu tunayopewa licha mbinu za kimataifa zinazofanywa bidii ya kutumia kinga au chanjo.

Kwa kweli, naopongeza serikali na sifa hizi ni zetu sote, kwani tunatolewa mfano kimataifa juu ya hatua tulizopiga dhidi ya maradhi ya malaria. Kwa hiyo, pindi tukipata wageni wanatoka nje ya nchi kuwaomba wapime afya zao mara watakapoonesha watakaa muda mrefu.

Naamini kabisa ni lengo la taifa lolote lile kuona kuwa wananchi wake wanalinda mali zao, amani pamoja na afya zao. Haitaki watu wapoteze maisha yao ovyo hasa haya yanayotokea kwa wanawake na watoto, vifo vya wanawake wakati wa uzazi. Serikali inaandaa kila aina ya mazingira mazuri kwa wanawake hao lakini bila ya kuwa na juhudi za makusudi za wahusika kama wazazi, walezi, wake kwa waume na wote wanaohusika.

a) Mwanamke anaolewa bila shaka anataka ajizae hivyo mazingira yote salama lazima yawepo baina ya mume na mke, pamoja na familia. Asiachwe mwanamke peke yake, ahimizwe kuhudhuria *clinic*, atumie lishe bora, awekwe karibu na

huduma ya afya kwa mujibu maendeleo ya afya yake ya mimba, ili kuepuka vifo ikiwa atapelekwa hospitali mapema maisha ya mama na mtoto yataokolewa, maelezo haya kwenye ukurasa wa 12 katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri.

b) Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru hadi sasa maradhi ya mripuko Mwenyezi Mungu katuepushia, lakini haina maana tubweteke, tushirikiane na Wizara ya Afya katika juhudi zao na juhudi hizo zitapatikana kama hatujabariki *budget* walioiomba, Wizara ya Afya hivyo naomba wajumbe wote tupitishe ili watekeleze kama walivyoomba, maelezo haya kwenye ukurasa wa 48 katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante na mbarikiwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze wote wawili Mhe. Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wote kwa ujumla.

Naomba kuchangia *budget* hii ya Wizara ya Afya. Mhe. Waziri naomba nifahamishwe lini huduma ya Bima ya Afya hospitali ya Mnazi Mmoja itaanza, kwani wafanyakazi wengi wa serikalini wanapata tabu sana pale inapofika wanahitaji matibabu kutokana na hali ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu Hospitali ya Wagonjwa wa Akili iliyopo Kidongochekundu, majengo yanavuja sana na madaktari hakuna. Kwa kweli, najua ufanisi wa Mhe. Waziri wa kazi, naamini anaposimamia kazi anahakikisha inakuwa nzuri.

Baada ya maelezo mafupi hayo naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia ahsante sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, moja pongezi Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Afya.

Pili Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa juhudi za kuimarisha sekta hii ya afya.

Tatu kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, pongezi kwa juhudi zenu ni jambo zuri kuingia mkataba na Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*) Bara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuto ushauri kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Afya, kushughulikia changamoto ya wizi wa dawa, sio tu katika bohari lakini katika hospitali na vituo vya afya.

b) Uwepo utaratibu utakaohakikisha mlengwa wa dawa zinamfika, kwani dawa zinapelekwa hospitalini na vituoni, lakini muda wa siku chache tu unaambiwa zimekwisha.

c) Dawa zote za serikali ziwe na nembo ya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali kuhusu zile dawa za wahisani kama zitakosa nembo mtadhibiti vipi.

d) Kuweka *CCTV camera* hata katika hospitali na vituo vya afya sio katika bohari tu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu huduma za *Oxygen* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa kwei, namuomba Mhe. Waziri, angalia sana Kitengo cha Huduma za *Oxygen* pana matatizo mengi.

i. Mtambo kutoka Uturuki haujafungwa hadi leo, kwa nini.
ii. Kwa nini, mtambo uliopo unaharibika mara kwa mara.
iii. Utaratibu gani wa Sheria za Manunuzi unatumika katika kununua *oxygen* - Bara.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia kuhusu Bima ya Afya na Sera ya Afya kwa Wageni. Kwa kweli, umefika wakati Zanzibar kuanzisha Sera ya Bima ya Afya ili kupunguza gharama za tiba. Vile vile, Zanzibar iwe na Sera ya Afya kwa wasiokuwa Wazanzibari serikali inatumia fedha nyingi kutoa matibabu kwa wageni.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali za *Cottage*. Pongezi kwa azma hiyo ni jambo jema, lakini je *Cottage* za Micheweni na Vitongoji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri. Kabla ya kutangaza serikali inahakikisha kuwa imejipanga vyema isiwe kama Mnazi Mmoja, bado kabisa hadhi yake kuwa Hospitali ya Rufaa. Huduma bado haziridhishi na malalamiko mengi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja asilimia mia moja, lakini naomba ufafanuzi wa baadhi ya hoja zangu na naomba ushauri wangu uzingatiwe. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Afya. Kwanza naomba nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kuwepo hapa na tukawa tupo katika utulivu. Lakini kwa kutumia nafasi hii hii uliyonipa naomba uniruhusu kumshukuru sana kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake mwema kwa Wazanzibari wote. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema ili aweze kutimiza dhamira yake ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Afya nachukua fursa hii kupongeza juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipaumbele kikubwa kilichoipa wizara hii na kufanya juhudi za makusudi kuweza kuhakikisha huduma za afya hazisiti zinazidi kuimarika kwa maslahi ya wananchi. Wizara tunawashukuru viongozi wetu wakuu wa serikali, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Idd na tunawaahidi kwamba tutafanya kazi kwa bidii na maarifa ili dhamira njema ya serikali ya kutoa huduma bora za afya kwa wananchi ipatikane.

Mhe. Spika, nakushukuru wewe binafsi pamoja na Mhe. Naibu Spika, na Wenyeviti wetu wa Baraza Mhe. Mwanaasha Khamis na Mhe. Shehe Hamad Mattar pamoja na watendaji wote kwa jinsi mnavyotuongoza na kutuelekeza. Nawashukuru pia shukurani za pekee Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano na michango yao, michango ambayo kwetu Wizara ya Afya ni maelekezo tosha na huwa tunayafanyia kazi na kwa kweli yanaleta tija.

Mhe. Spika, nitakuwa sina fadhila kama sitoishukuru familia yangu kwa kunipa mashirikiano pamoja na wananchi wenzangu wa Jimbo la Wete. Lakini shukurani za pekee zenye uzito wa pekee nazitoa kwa wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya Unguja na Pemba kwa kuanzia na Katibu Mkuu wa wizara, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini Wizara Pemba, Mkurugenzi Mkuu, Wakurugenzi wengine na wafanyakazi wote hadi vituo kwa mashirikiano wanayotupa mimi na Mhe. Waziri ambayo yanatupa nguvu na hamu ya kuendelea kufanya kazi nao.

Nimalize shukurani zangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri Mahmoud Thabit Kombo kwa maelekezo yake ambayo yanaendelea kunisaidia kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa nikiwa pamoja na Mhe. Waziri mpya, waziri wangu wa Afya Mhe. Hamad Rashid naye namshukuru sana kwa kuendelea kuniongoza na kunielekeza.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo sasa naomba kufafanua baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe. Naanza na Mhe. Masoud Abrahman Masoud, Mwakilishi wa Jimbo la Bububu ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, yeye aliuliza ni lini Hospitali ya Bububu Jeshini itaanza kupata mgao wa dawa? Mheshimiwa wizara tayari tumeshaanza kuwapatia mgao wa dawa Hospitali za Jeshi na Vikosi vya Ulinzi, dawa zenye thamani ya shilingi 2.5 milioni wamepatiwa Hospitali ya Bububu Jeshini. Aidha, hospitali nyengine nazo zitaendelea kupatiwa dawa baada ya kuzifanyia ukaguzi wa kina na kuridhishwa na huduma zao.

Mhe. Asha Abdalla Mussa, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kiwengwa yeye alitaka kujua fedha za *DNA* za mwaka jana, yaani shilingi 1.8 bilioni zilitumika kwa kitu gani? Na za mwaka huu shilingi 900 milioni zimepangwa kwa kitu gani.

Matumizi ya fedha hizo mradi wa mwaka 2017/2018 ni shilingi bilioni moja, milioni mia nane ni kama ifuatavyo:

Malipo ya Mkandarasi ni shilingi 183 milioni; malipo ya *DNA* ya matengenezo ya chumba cha maabara ni shilingi 1,617,000,000. Matumizi ya shilingi milioni tisa zilizotengwa kwa mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo:

Shilingi 400 milioni ni malipo ya thamani za maabara, shilingi 500 milioni kwa ajili ya malipo ya vifaa vya maabara na mengineyo.

Pia Mhe. Asha alitaka kujua pamoja na serikali kuongeza bajeti ya dawa lakini bado vituoni dawa hazipatikani. Je, vifaa vinafika vituoni anauliza na je, watoa huduma ambao hawawajibiki wanachukuliwa hatua gani?

Mhe. Spika, wizara inajitahidi kununua dawa nyingi na kuzifikisha kwenye hospitali na vituo vyote vya afya Unjguja na Pemba. Kwa kweli dawa tunaendelea kusema kwamba zipo, wizara tutafuatilia kwa kwa karibu sana kuhakikisha kila mwananchi anapata dawa na kama kuna kituo ambacho hakina dawa tunawaomba Waheshimiwa msisite kutupa taarifa ili tufuatilie. Kwa sababu wanaofanya kazi katika Hospitali na Vituo vyetu vya Afya ni binadamu na binadamu ana ila na hekima mbali mbali za kutaka kupitisha mambo ambayo si ya kawaida, mtakapotubainishia sisi na sisi tutafuatilia ili tuchukue hatua zinazoridhisha.

Kuhusu kuwajibika kwa watendaji mhudumu yeyote atakaebainika hawajibiki na anazuiwa wananchi wasipate huduma hii ya dawa hatua kali dhidi zake zinachukulia. Tunawaomba wananch wote ushirikiano wa kutupatia taarifa pale inapotokezea. Tunawaomba Waheshimiwa na wananchi wasifiche taarifa.

Pia Mhe. Asha Abdalla alitaka kujua kuhusu watoto wawili waliotafunwa na mbwa na mmoja kupoteza maisha. Mheshimiwa hili tumeliundia kamati maalum na nitamuomba Mhe Waziri alijibu kwa ufafanuzi zaidi ili aweze kuridhika. Mhehsimiwa pole sana msiba ule sio msiba wake yeye peke yake bali ni msiba wetu sote.

Mhe. Ali Sueiman Ali Jimbo la Kijitoupele. Mheshimiwa michango yake tumeipokea na tunamshukuru sana kwa ombi lake la kukitembelea kituo cha Kijitoupele Magirisi, tutawasiliana tukitembelee na kwa mashirikiano sisi na yeye naamini tutafanikiwa lile ambalo anahisi limemtanza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said alitaka kujua takwimu ya maradhi yasiyoambukiza na sababu zake. Mheshimiwa takwimu za maradhi yasiyoambukiza zimeelezwa vizuri kuanzia ukurasa wa 15 hadi 16 katika kitabu cha bajeti cha Wizara ya Afya. Hivyo, tunamuomba kwa heshima kubwa kwa ku-*save* muda uliopo basi aangalie tena katika kitabu kile atayapata yote kwa jinsi yalivyoelezwa. Isipokuwa ongezeko linasababishwa na maisha fetevu yaani kukaa tu na kulala, pia kutofanya mazoezi, pia matumizi ya tumbaku na pombe na kutozingatia milo yenye afya.

Mhe. Suleiman Sarahan pia alitaka kujua kwa nini Hospitali ya Abdalla Mzee isiwe na rufaa na kupewa jila la Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Mheshimiwa serikali imeshaamua na kutangaza jina la Hospitali ya Abdalla Mzee ya Mkoani kuwa ni *Abdalla Mzee*

Hospital kutokana na historia yake. Ni nia ya serikali na hatimaye Hospitali ya Abdalla Mzee kuwa hospitali ya pili ya rufaa.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali amependekeza shilingi 12.7 bilioni za dawa zinunuliwe kutoka viwandani. Wazo lake Mheshimiwa tumelipokea na napenda kumfahamisha kwamba, wizara tayari imefunga mkataba na *Centro medical store* Tanzania Bara na tayari imeshaanza kununua dawa moja kwa moja kutoka viwandani, ambapo kwa kiasi kikubwa inapunguza gharama.

Pia Mhe. Mohamedraza alitaka kujua tatizo la *X-Ray* za Hospitali ya Abdalla Mzee kutokufanya kazi. Ni kweli mashine za *X-Ray* zilikuwa mbovu katika Hospitali ya Abdalla Mzee kwa muda mrefu. Hata hivyo, baada ya kuajiri mtaalamu *biomedical engineer* hivi karibuni mashine hizo zimeshatengenezwa zote na zinafanya kazi ipasavyo, pamoja na mashine nyengine zote ambazo zilikwama kwa muda mrefu basi sasa zote zinafanya kazi. Kijana huyu kwa kweli ni kijana hodari, mahiri na tunaomba kwa kweli tumpongeze ni kijana ambaye anaokoa mali za serikali katika hospitali ile na hospitali nyengine.

Kuhusu suala la umeme tayari wizara imeshawaandikia na kuonana nao Shirika la Umeme *ZECO* na wameahidi kulifanyia kazi suala hilo, nasi tunafuatilia kwa ukaribu zaidi kuona kwamba kadhia hii, shida hii ya umeme katika hospitali ile inaondoka.

Mhe. Mohamed Said Dimwa alizungumzia suala la maradhi ya kichocho. Napenda kumjuilisha Mheshimiwa kwamba kichocho kwa ujumla kimepungua na sasa kimefikia asilimia 1.7 kwa Zanzibar, kutokana na jitihada mbali mbali zinazoendelea kufanyika. Ni kweli kuna baadhi ya maeneo maradhi haya yamekuwa sugu, tayari wizara imeshayapangia mikakati maalumu ikiwemo maeneo ya Mahonda, Mwera, Kinyasini na Kadhalika. Changamoto kubwa inayotukabili kwa sasa ni kumalizika kwa mradi uliokuwa unagharimiwa na *STORE*. Hivyo, serikali kwa mwaka ujao wa fedha imetenga kiasi cha fedha kutokana na bajeti yake ya serikali yaani *OC*.

Mhe. Mohamed Said pia alitaka aeleweshwe namna ya kiashiria cha asilimia ya watoto wanaonyonya maziwa ya mama pekee kinavyopatikana. Jibu ni kwamba, kiashiria hiki kinapatikana kupitia tafiti zinazofanywa kitaifa ambapo Zanzibar huwa tunashiriki katika tafiti hizo *Tanzania National Nutrition Survey*. Aidha, kuhusu takwimu ya wajawazito waliogunduliwa na upungufu wa damu kwa mwaka 2017 asilimia 1.7 ya mama wajawazito waliohudhuria kliniki waligunduliwa na upungufu wa damu na kupatiwa dawa na matibabu yanayohusika. Aidha, shabaha kwa mwaka 2018/2019 ni kufikia asilimia 0.

Mhe. Mohammed Said Mohammed pia alitaka kujua kuhusu nyumba za wizara zilizotolewa na serikali kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya kwamba ziko wapi na wizara ina mpango gani kuhusiana na nyumba hizo zimeshachukuliwa na watu.

Mhe. Spika, jibu ni kwamba, Wizara ya Afya imeshafanya uhakiki kwa rasilimali zake zote kwa madhumuni ya kuzitambua rasilimali hizo, uhakiki huo umejumuisha utambuzi

wa nyumba ambazo Mhe. Mohamed Said Mohamed amezieleza. Kutokana na uhakiki huo umeonesha kwamba kuna jumla ya nyumba 32 ambazo zinamilikiwa na Shirika la Nyumba ambazo zilitolewa na serikali kwa ajili ya matumizi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Wizara inaendelea kutafuta taarifa zaidi ili kubaini kama kuna nyumba nyengine kwa madhumuni ya kuziwasilisha Shirika la Nyumba ili tuweze kubaini wakaazi wa nyumba hizo na kuendelea na hatua za kuzidai. Nyumba zilizobainika hadi sasa ni kama ifuatavyo:

Unguja: Mombasa 'A' nyumba moja, Mombasa 'B' nyumba tano, Vuga nyumba nne, Kikwajuni nyumba mbili, Michenzani nyumba nne, Vuga iko nyumba moja.

Pemba: Madungu ziko nyumba tatu, Tenis Cot nyumba tatu, Uzunguni nyumba saba, Micheweni nyumba mbili, Bomani nyumba mbili na jumla nyumba zote ni 32.

Mhe. Spika, naomba sasa kumjibu Mhe. Zulfa Mmaka Omar, yeye alizungumzia mambo mengi yakiwemo ubovu wa paa la nyumba pale Hospitali ya Chakechake, harufu isiyopendeza chumba cha *Neonatal* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Jibu. Nakiri kuvuja kwa paa katika Hospitali ya Chakechake na maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha bajeti ingawaje hakupenda kukisoma kwa hasira ndio hatua iliyofikia kwamba mkandarasi ameshapatiwa kazi hiyo na kutengeneza, tunategemea aanze muda wowote mara baada ya bajeti yetu hii.

Kuhusu *Neonatal Ward* tunakubali kuwa chumba ni kidogo na kinamama wanaokwenda kunyonyesha watoto wachanga ni wengi. Kiutaratibu chumba hicho hakitakiwi kuwa wazi. Hivyo, ni dhahiri kwamba kutokana na udogo wake kitaleta harufu isiyo ya kawaida kutokana na maumbile ya kibinadamu. Hata hivyo, wizara haikukaa kimya inalishughulikia suala hilo hasa baada ya kukamilika wodi ya zamani ya wazazi tunategemea chumba kile wagonjwa wenye watoto waliomo katika chumba kile tutawahamishia katika jengo lile baada ya kumaliza na naamini kwamba baadhi ya changamoto zitakuwa zimetatuka.

Mhe. Zulfa pia alizungumzia upungufu wa mashine za *phototherapy* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika: Una dakika tano Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Nashukuru Mheshimiwa. Ni kweli kuwa mashine hizo zilikuwa ni mbili katika hospitali hiyo, lakini wiki iliyopita tumepata mashine nyengine nne. Kwa hivyo, kwa hivi sasa tunavyozungumza tunatumia mashine sita. Tunamuomba Mhe. Zulfa apate nafasi ili atembelee sehemu zile na ataona kama kuna mabadiliko.

Mhe. Spika, napenda sana niendelee kuwapongeza na kuwashukuru wafanyakazi wa Wizara ya Afya wanavyofanya kazi kwa juhudi na maarifa katika kuokoa maisha ya wananchi wetu. Changamoto zinazojitokeza Mheshimiwa hawa wafanyakazi ni binadamu na anayefanya kazi binadamu hakosi mapungufu, hakosi kasoro, nawaomba

sana Waheshimiwa wenzangu na pia wananchi tusiwavunje moyo wafanyakazi hawa, tusiwavunje moyo madaktari wetu, tusiwavunje moyo wataalamu wetu hawa mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi ambaye niko kule nikonao naona jinsi wanavyo-*struggle* katika kuokoa maisha ya binadamu, naona jinsi wanavyojitolea kwa hali na mali katika kuokoa maisha ya wagonjwa. Mheshimiwa tunapopata taarifa, tunaposikia kwamba wanalaumiwa na bila ya kusifiwa hata jambo moja basi inatuuma ndani ya roho. Kwa sababu kwa vyovyote vile iwavyo hata ufanye baya kiasi gani lakini na jema japo dogo litakuwepo, unapaswa umshukuru, unapaswa umpongeze kwa lile jema dogo alilolifanya, lakini sio kumlaumu tu moja kwa moja unamvunja moyo na tukiangalia ule msemo wa Kiswahili unasema: "Tusidharau wakunga na uzazi ungalipo".

Kwa hivyo, mimi naomba nichukue nafasi hii kushukuru Baraza lako, kuwapongeza sana wajumbe wako kwa ajili ya michango yao. Michango ya Wajumbe wako Mheshimiwa kwetu sisi ni maelekezo, lakini kwetu ni dira na huwa tunaifanyia kazi na kupata ufanisi wa kutosha.

Mhe. Spika, baada ya hapo machache naomba sasa nitamke rasmi kwamba naipongeza hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima na taadhima sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Afya ili aje atoe majumuisho ya hoja yake. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, awali ya yote naomba tuendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma na utukufu kwa kutujaalia kupata fursa hii adhimu ya kuweza kufanya majumuisho ya hotuba ambayo niliwasilisha jana mbele ya Baraza lako tukufu.

Pili naomba niendelee kumshukuru sana Mhe. Rais Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuendelea kuniamini nakumbuka tarehe 9/04 aliniteuwa kuwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na tarehe 28/02/2018 aliniteuwa kuwa Waziri wa Afya. Muda ambao nimekaa Wizara ya Kilimo ilikuwa ni siku 628 na sasa Wizara ya Afya nafikiri inakaribia siku tisini na kidogo sana.

Kwa hiyo, kwanza nataka nimwambie tu ndugu yangu rafiki yangu, swahiba wangu Mhe. Hamza Hassan Juma sio kweli kama zile tarehe alizozitaja za siku tano si za kweli kabisa kabisa nimekaa siku 628 kama ni miaka mitatu ingekuwa siku elfu moja na thamanini. Ningeomba tu asahihishe sitaki tuingie kwenye malumbano asahihishe tu kwa sababu *hansard* isomeke vizuri. Namshukuru sana Rais kwa kunipa nafasi hiyo ya kuiongoza wizara hii nyeti.

Lakini pili nataka nimshukuru Mhe. Rais pekee kabisa wakati ananikabidhi wizara hii aliniita na akanambia kwamba hii wizara ndio uhai wa taifa letu, taifa limekuamini na sisi

tunaendelea kukuamini kama tunavyowaamini wenzako kajitahidi msaidiane na wenzako ili watu wapate afya inayostahiki na wapate huduma inayostahiki.

Nataka nimshukuru Mhe. Rais amekuwa karibu sana kila wakati kutupa maelekezo miongozo namna gani tutaiendesha wizara. Nataka niseme tu Mhe. Waziri aliepita Mhe. Mahmoud Thabit Kombo amefanya kazi kubwa sana. Nilishuhudia utekelezaji wa ilani ya CCM asilimia sabini na mbili kazi kubwa sana aliyofanya sio kazi rahisi hata kidogo. Lakini nasema huu ni mchele na mchele unaupika kila mmoja na mapishi yake na katika mapishi niliyoyakuta mimi moja na nilipokaa na wataalamu walinambia tatizo la kwanza lililopo pale ni *attitude* hulka. Hulka ndio kwanza tatizo la msingi na mimi nataka hili nikubaliane kabisa na wenzangu wote Wawakilishi kwamba tunalo tatizo la msingi la hulka, hulka tu ya mtu, alinambia Mhe. Waziri Mahmoud Thabit Kombo kwamba hili limemshinda nakuombea dua umsaidie.

Tatizo la pili ni mawasiliano, sio kwamba vitu havipo lakini mawasiliano baina ya sekta moja na moja ni tatizo. Nimekaa na daktari dhamana wa Mnazi Mmoja amenambia tatizo hilo hilo. Kwa hivyo, kazi yetu kwanza ni kutengeza mazingira ya watu kubadilika ki fikra na kuweka mawasiliano ambayo yatasaidia hizi huduma na *facility* zitazotumwa na serikali ziwafikie wananchi naomba hili mtusaidie sana. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, kwa utangulizi kwanza nataka nitoe shukurani sana za dhati kwako Mhe. Spika, Naibu Spika, na wenyeviti wote lakini na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli aliezungumza hapa alizungumza kwa uchungu kwa sababu anaona uchungu wa maisha ya binaadamu. Ni muhimu sana kwetu sisi kama viongozi kuona maisha ya binaadamu wetu yanakwenda vizuri ili taifa libaki na watu wenye afya nasema niwashukuru sana. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Spika, waliochangia kwa kujieleza humu ndani ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Masoud Abdrahman Masoud - alizungumzia kwa niaba ya kamati lakini pia akatoa mchango wake yeye ni Mwakilishi wa Jimbo la Bububu ninamshukuru sana.
2. Mhe. Asha Abdalla Mussa
3. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
4. Mhe. Simai Mohammed Said
5. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
6. Mhe. Suleiman Sarahan Said
7. Mhe. Mohamedzara Hassanaali Mohamedali
8. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
9. Mhe. Omar Seif Abeid
10. Mhe. Hidaya Ali Makame
11. Mhe. Mohamed Said Mohamed
12. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
13. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
14. Mhe. Panya Ali Abdalla
15. Mhe. Hamza Hassan Juma
16. Mhe. Miraji Khamis Mussa

17. Mhe. Bahati Khamis Kombo
18. Mhe. Ali Salim Haji
19. Mhe. Ahmda Yahya Abdulwakil
20. Mhe. Suleiman Makame Ali
21. Mhe. Salma Mussa Bilali
22. Mhe. Ali Khamis Bakari
23. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
24. Mhe. Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum (Juma Ali Khatib)
25. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais
26. Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
2. Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni na Sanaa
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi
4. Mhe. Said Omar Said
5. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
6. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
7. Mhe. Miraji Khamis Mussa
8. Mhe. Naibu Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Katiba, Sheria n Utumishi wa Umma
9. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale
10. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
11. Mhe. Khadija Omar Kibano
12. Mhe. Mussa Ali Mussa

Mhe. Spika, kama kuna mmoja nimemsahau au wawili naomba mniambie tu ili niweze kuwatambua. Nawashukuru sana kwa michango yenu michango mizuri sana.

Mhe. Spika, ningeomba kwanza nianze na kamati, nataka niishukuru sana Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza lako imefanyakazi kubwa sana chini ya Mwenyekiti wake kwa kutuongoza katika wizara hii kwa ushauri. Lakini vile vile kwa kuwa karibu sana na kamati na pale watakapoona kuna tatizo hawangoji vikao wanatutafuta. Mimi hili nasema nataka niwashukuru sana. Wameipongeza bajeti na wametuelekeza maeneo ambayo tunahitaji kuyasimamia. Nataka niwaahidi kwa jumla maelekezo yao yote sita waliyoyatoa watayakuta katika taarifa ambayo tutawasilisha baadae kwao.

Naomba niwashukuru sana katika suala zima la kusimamia bajeti, wamezungumzia sana suala la kuimarisha huduma za afya na mazingira. Nasema haya yote waliyoyahimiza nakuahidi kabisa Mhe. Spika, tutayasilisha kwa kamati.

Pili nataka nimshukuru sana Naibu Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuweza kujibu baadhi ya hoja. Lakini nianze kwanza na Mhe. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto amefanya kazi kubwa sana namshukuru sana kujibu baadhi ya hoja. Mhe. Waziri asiekuwa na Wizari Maalum Mhe. Juma Ali Khatib nae amejibu

baadhi ya hoja na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili nae amejibu baadhi ya hoja, sitaki nirudie hizi hoja. Ila nataka niende kwenye mambo ya msingi kwanza.

La kwanza Mhe. Spika, jana Mjumbe mwenzetu hapa Mhe. Asha Abdalla Mussa alilia ndani ya Baraza hili na kutoonesha hisia zake za watoto wawili ambao walitafunwa na mbwa kutokana na kichaa cha mbwa na bahati mbaya wakapoteza maisha kati ya wanne. Baada ya kupata tatizo lile Naibu Waziri mimi na yeye kwa pamoja tukampigia simu nikamuomba mambo mawili la kwanza kwa sababu mimi nimeshapata taarifa ya maandishi ya wataalamu nikamuomba na yeye atusaidie taarifa ya maandishi ili hatimae tuunde timu ya wataalamu kwenda kuchunguza na kuangalia taarifa hizi mbili. Kwa bahati mbaya hakupata muda wa kufanya hivyo na amesema hapa kwenye Baraza namshukuru sana.

Kwa hiyo, jana tutakutana kwa dharura na kamati ya uongozi wa wizara na tukakubaliana kufanya yafuatayo. Kwanza tumuombe Mheshimiwa atusaidie kutupa taarifa za zaida chini ya kamati ya wataalamu maana yake kila fani ina wataalamu wake madaktari wana bodi yao ya wataalamu ili tuwakabidhi bodi ile kwa muda wa wiki moja wafanye uchunguzi na ndani ya wiki moja wanikabidhi mimi taarifa na taarifa hiyo na mimi kwa utaratibu wa kiserikali niiwasilishe rasmi serikalini.

Namuahidi katika kipindi cha wiki tatu taarifa hii itakuwa imekamilika na itakuwa imewashilishwa rasmi serikalini na hapo baadae serikali itatoa maelekezo nini cha kufanyika. Namuomba radhi sana kwa kilichotokea lakini utafiti utakaofanywa ndio utabaini nani amekosa na nani si mkosa.

Kwa hiyo, naomba sana na namshukuru sana kwa hilo alililofanya lakini tena azidi kutupa ushirikiano zile taarifa ambazo yeye anazo na sisi hatunazo tuchanganye pamoja tuwakabidhi wataalamu wetu watakaofanya kazi ya uchunguzi na hatimae tuweze kupata matokeo.

Mhe. Spika, kwa sababu jambo limesemwa humu nakuhakikishia kabisa taarifa itakayotoka serikalini tutakuletea na wewe rasmi ili uione tena utaamua wewe mwenyewe Spika nini cha kufanya. Lakini kwanza tutaiwasilisha serikalini ili serikali ifanye maamuzi ya pamoja hili si jambo la mtu mmoja ni jambo la pamoja na tulifanye kwa pamoja. Lilikuwa ni jambo la kwanza niliseme ndani ya kikao chako.

Pili Mhe. Spika, niseme kwa mara ya kwanza Wizara ya Afya ndio imepata fedha za kutosha sana na kabla ya kupewa fedha nataka nimshukuru sana Mhe. Rais alituuliza swala hili. Hivi mkipata fedha hizi nyie mnaenda kufanya nini matokeo ya watu uawe nini, matokeo ya serikali yawe nini? Akatupa muda wa wiki mbili tujibu hayo maswali. Tukaenda kwenye kikao tukaa nae tukamueleza fedha hii ikipatikana jambo hili na hili litaonekana. Akasema sawa nitakupeni fedha katengenezeni *Budget Speech*.

Budget Speech hii kabla haijaja hapa imepita tena kwake je yale tuliyoyazungumza tuliyokubaliana ni sawa au si sawa, akasema sawa endeleeni *Budget Speech* hii ni *Budget Speech* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar si yangu wala si ya mtu yoyote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, anaekuja akasema kwamba hii *Speech* mbovu na kadhalika kwa kweli anaisema serikali na serikali hii imekuwa makini sana na uthibitisho wa umakini wa serikali hii angalieni vigezo vya kiuchumi tulivyofikia. Hakuna mtu anayeweza kuendesha uchumi ambao sio tegemezi ukaondoka kwenye tegemezi ukajitegemea wenyewe sio rahisi. Ni kuonesha serikali ni makini na ni madhubuti sana tumetoka kwenye utegemezi wa asilimia thalathini na tuko kwenye asilimia saba, tumetoka kwenye Bajeti ya Afya 72 bilioni tunakuja 93 bilioni sio rahisi. Tumeondoka katika wizara ambazo wenzetu wote wanachangia serikali hii inasema hakuna kuchangia hatutaki kubadilisha sera ya serikali. (*Makofi*)

Ni sera iliyoanza tokea mwaka 1965 ya Matibabu bure Rais huyu sisi tumembana kwa taarifa yenu, Rais tubadilishe gharama hizi ni kubwa, akasema hapana hatuwezi kutoka kwenye misingi, tulinde Mapinduzi yetu, tulinde sera zetu. *Afro Shirazy Party* 1965. Nimekwenda Cuba kwenye mkutano wa watu elfu moja na mia mbili nilikuwa na Dr. Jamala. Watu wanazungumzia *political willingne*ss, mimi nikasema sisi tumeanza mwaka 1965 nyie mnazungumzia leo huduma za Afya ziwafikie watu sie tumezungumza 1965 chini la Ilani ya *Afro Shirazy*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sisi tuna kila sababu ya kujitamba zaidi kuliko wenzetu tuliochukuwa mzigo huu tokea 1965 mpaka leo, sio jambo rahisi hata kidogo, wenzetu wameshaanzisha taratibu chungu nzima za kuchangisha watu sie tumekataa. Asili ya kuona mapato kidogo yamepungua Mnazi Mmoja ni kwa sababu kipindi fulani tulilegeza kamba tukasema watu wachangie Mhe. Rais akasema hapa tumesema wasichangie ndio mkaona mapato yameteremka Mmazi Mmoja. Mkitataka kubalisha Sera rudini kwenye Vikao vya CCM mkabadilishe Sera sio hapa. (*Makofi*)

Utaratibu wa kubadilisha Sera za Nchi mnarudi kwenye Chama chenu kinachotawala ni Chama cha CCM mlileta Azimio la Zanzibar hapa mlikwenda Kisiwanduwi kubalisha kama mnataka kubalisha sera ya matumizi ya afya rudini kwenye CCM mkaseme jama tunataka kubadilisha sera ya *Afro Shirazy* tuliyotoka nayo ili tubadilishe sasa kafanyeni huko halafu leteni hapa hatuna matatizo. Sisi wengine hatuingii huko mkituletea tutafanya kazi, kazi yetu ni kutekeleza yale tuliyokubaliana. Wananikaribisha. (*Makofi*)

Kwa hiyo la kwanza niliseme la jumla kwamba hili jambo la matibabu bure ni sera na sera ya msingi kabisa na mnakumbuka kabisa wale tuliotoka kwenye *Afro Shirazy* kwamba wananchi wetu walikuwa wanapata matibabu kwa kubaguliwa Mzee Abeid Aman Karume akasema hapana huduma hizi lazima ziwe bure, maji, afya, elimu bure tusisahau tulikotoka. Hilo lazima tulilinde kwa nguvu zetu zote na mimi nashukuru sana Mhe. Rais amelisimamia pamoja na *pressure* zote anazozipata tutaendelea kulilinda mpaka dakika ya mwisho. (*Makofi*)

La tatu niliseme la jumla Mhe. Spika, mtaona katika Mafungu ya fedha kweli kuna mabadiliko. Ni kweli kuna mabadiliko tumekoka kwenye *72 billion to 93 billion* lazima kutakuwa na mabadiliko. Kwa hiyo, ukiuliza fungu gani kwa nini limepungua hili limeongozeka, limeongezeka kwa sababu bajeti imeongozeka hilo la kwanza.

Lakini la pili tuna vituo 192 vya Afya tumevigatua tunavipeleka wilayani mtakuta mafungu mengine fedha zimekwenda kwenye Halmashauri zenu mkasimamie huko chini sasa. Kwa hiyo, yako mafungu mtakuta yameongezeka yale tunayosimamia kwenye wizara moja kwa moja kuna mafungu yatakuwa yamepungua yamekwenda kwenye huu ugatuzi huko chini mtakwenda kuyasimamia huko chini. Ndio tafauti mnayokuta *data* zote hapa nnazo za kuonesha mafungu haya yamebadilika kwa nini. Yamebadilika kwa sababu hizo mbili tu. Moja tumepata fedha ya ziada ya kununulia dawa kwa mfano tumetoka kwenye *70 billion* kwenye *to 12.7* utaiona tafauti tu na kwa nini tukafanya hivyo, Rais anasema dawa ni bure ni kuhakikisha kila mtu anapata dawa bure na dawa zifike kwa wananchi. (*Makofi*)

Katika lile nililolisema tatizo la *communication* ndio tatizo lililosababisha upungufu wa dawa na ndio maana Mhe. Spika, mimi mwenyewe nimetembelea Mnazi Mmoja mara 17 Mnazi Mmoja tu peke yake usiku mchana saa nane za usiku kuona hili tatizo wapi tu-*unlock* hili tatizo liko wapi. Nakupeni mfano ulio hai unakwenda kwenye ward unaambiwa dawa fulani hakuna, unachukua simu unampigia mtu wa bohari anakwambia dawa mbona tunazo nyingi tatizo liko wapi. Tatizo mtu ambaye hana dawa anatakiwa apeleke *order* ya dawa hakuipeleka, kwa hivyo yeye kakaa hakuna dawa akija mgonjwa anamjibu hakuna dawa anaondoka mgonjwa anakwenda kununua dawa kumbe dawa iko kwenye ghala.

La pili nikapata matatizo ya watu wanao *supply* dawa, wakawa wanadai fedha mimi nikawambia mtutudai fedha sawa tuleteleteini dawa kama hamutuletei dawa tunakata mkataba tunakwenda kwengine, wakatuletea dawa. Serikali tunashughulika na kulipa maanake serikali haiwezi kushtakiwa ki ovyo ovyo. Ndio maana ukaona tume-*unlock* haya matatizo leo nathubutu kusema nimepita kwenye kitanda cha mgonjwa mmoja mmoja Mnazi Mmoja, Chake Chake Hospital, Makunduchi Hospital, Kivunge Hospital namuuliza shida yako nini dawa hupati napata wananambia shida moja tu tuliyonayo wafanyakazi wachache hawatoshi.

Kila nilipokwenda ongeza wafanyakazi hawatoshi waliopo ni wachache tunaomba utusaidie zaidi hilo ni tatizo la msingi nalikubali na ndio maana serikali mara hii imetoa ajira ya watu 680 tuajiri. Tatizo limeeleweka tumetafuta *solution* tupeni pesa tukafanye kazi mje mwakani mtusute, mbona mlisema hili halikuwa na nashukuru sana ninae kamanda hapa Mhe. Haji Omar kakabidhiwa vituo huko chini, tuje hapa mtusute lakini leo ni kutuonea tu maana pesa hamjatupa matatizo tumeshayaeleza na sisi tumeandika makusudi changamoto zote ambazo zipo katika wizara hatukuficha tumeisema moja baada moja changamoto iliyopo, twende tukakabidhi changamoto hizi muone tuje mwakani mutwambie mbona hichi hakikufanyika, hiki hakikufanyika. (*Makofi*)

Bwana Hamza ukitaka nijiuzulu wakati huo mimi nitajiuzulu tu. Kama ni kujiuzulu kama hatukutekeleza tutajiuzulu kwa nini tuone haya, huwezi kuwa muungwana ukashindwa kazi ukasema unabaki kazini. Alivyosema ndugu yangu Yahya tokea 1977 napewa majukumu sina *fail* ya pahala popote nashukuru mungu *I am no failure* nenda serikalini

nenda kwenye *opposition* nenda popote nilipofanya kazi *I am no failure, I am record* lakini lazima tupate nafasi ya kufanya kazi.(*Makofi*)

Kwa hivyo kilio chenu ni kilio chetu ni kilio cha Rais, Rais katika jambo ambalo linamuuma ni kwamba yeye 1969 ameanzia kazi Wizara ya Afya ni wizara yake ni mwanawe, hatofurahi kabisa aondoke hapa madarakani aone kamuacha mtoto katika hali mbaya na ndio maana akasema hebu sasa tuzipandisheni *grade* hizo hospitali, *criteria* ya kuipandisha Makunduchi iwe hospitali ya Wilaya ni nini tukaziorodhesha pale, ili tuidhinishe Makunduchi iwe Wilaya sifa moja, mbili, tatu, nne, tano.

Nataka niwashukuru sana watu *Hips* wamefanya kazi kubwa sana wameshirikiana na wizara na serikali wamei-*develop* ile hospitali hali yake sio kama unavyozungumza Nataka niwape tena sifa nyengine watu wa Kusini, nimepitia vitanda vyote vya kina mama, namuuliza umezaa watoto wangapi ananambia watatu wa mwisho ana miaka mingapi ana miaka sita, nasema *alhamdulilah rabil alamin* kama kuna pahala pamefanikwa uzazi wa mpango nendeni Mkoa wa Kusini Unguja makajifundishe. Tukifanya hilo nakuhakikisheeni kabisa matatizo ya matibabu tuliyonayo sasa hivi wanaopata madaktari wetu itapungua.(*Makofi*)

Population gross ya Zanzibar leo ni 2.8% ni kubwa ukienda Mnazi Mmoja na tunawalaumu hawa vijana nimekwanda pale saa saba za usiku, kwenye *ward* nimekaa kama mtu wa kienyeji.....

Mhe. Spika: Waheshimiwa tusikilize majumuisho tafadhali.

Mhe. Waziri wa Afya: Nimekwenda pale nikaa kama mtu wa kienyeji tu hawanijui siku za mwanzo. *Labour room* kuna vitanda viwili wanaozaa wakati ninakwenda kumi, unategemea wale manesi na madaktari wataweza kuhudumia watu kumi katika *labour room* ya vitanda viwili wakaita kwenye *labour ward* wanazaa kwenye *labour ward* chini, tunawalaumu vipi, baya zaidi nilikwenda Kivunge watu wanajifungua watu waliokuja kwenye dirisha kutizama watu wanaojifungua ni wengi zaidi kuliko wanajifungua ndani, daktari ashughulikie nani ashughulikie aliyekuja kutazama mgonjwa au ashughulikie mgonjwa.

Nimekwenda Wete saa sita za usiku nakuta watu wamepiga kambi nje utafikiri wanataka kuchuma karafuu, nawauliza mnangoja nini tunangoja wagonjwa wetu wanataka kuzaa, saa sita za usiku daktari huyu anakwenda anawambia jamani ondokeni mazingira haya hayaruhusu tuna matatizo ya vyoo havitoshi vyoo vya kuhudumia wagonjwa, vyoo vihudumie wazima wanalala na wototo wadogo pale watoto wadogo wanapata maradhi, tunamlaumuje huyu daktari tunamlaumu vipi huyu nesi.

Kwa hivyo, sisi lazima tuwe binaadamu tuyaangalie mazinmgira halisi yaliyo utazame nafasi uliyonayo ukiingia wewe utafanyaje? Maana usipovaa kiatu cha mwenzako huwezi kujua shida mimi nilikuwa nalaumu kama nyinyi *but I did some thing* nikenda nikaa nao nikaangalia mazingira halisi yalivyo hospitali kwa hospitali na nikakubali kabisa wakati mwengine tu ni uzembe wa makusudi na nitakupeni mfano.(*Makofi*)

Nimekwenda *Mkoani hospital*, hospitali mpya nzuri namshukuru sana Dkt. Shein tunawashukuru sana ndugu zetu wa China *beautiful* nakwenda kwenye jiko watu wanapikia mkaa. Nauliza jamani mnapikia mkaa kwa nini mitungi ya gesi ipo majiko ya gesi yapo wanasema hatuna utaalamu, hamna utaalamu mwaka nzima. Nimeondoka pale nikaja Unguja nikaenda mpaka *technical college* kuomba wataalumu wakasaidie napigiwa simu Pemba mtaalamu amepatikana majiko yanafanya kazi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, hatusemi kwamba uzembe haupo, upo lakini tusiujumlishe sana tumchukue mzembe tufanye naye kazi tushughulike nae tumalizane nae na ndio mkaona sasa tunachukua hatua, *so what we have done* tumefanya nini tumeunda *compact team, compact team* hii ina madaktari, ina watu wa usalama, ina watu wa *anti corruption* hawa kazi yao ni kupita kila wiki kila hospitali kuhakikisha tunaangalia kama dawa zimefika, huduma zimepatikana nani kakorofisha tunamchukulia hatua *immediately*, tumeshafanya *trip* mbili na tumeona athari ziliopo matatizo yaliyopo na kuhakikisheni kabisa tutapata dawa ya matatizo ya watu ambao ni sugu hawataki kufanya kazi tunachohitaji ni *support* yenu.(*Makofi*)

Jengine ninaloliomba kwenu na kwa wananchi kwa jumla, watu wanatoa taarifa fulani kanifanyia hivi na hivi tupe ushahidi hataki, hatoi ushahidi kwa hivyo ananung'unika pembeni ukimwendea atoe ushahidi hatoi na una ushahidi mimi nimefanya ujasusi, nimekwenda kwenye tukio tukachuka *record* baada ya kumaliza *record* kila kitu nauliza na *video* kila kitu hana habari mwenyewe. Siku ya pili nikamwita nikamwambie bwana tupe ushahidi wa jambo fulani nasikia limetokea pahala fulani anasema mimi sihusiki kabisa, nikawambia hii sio ya kwako, haa, haa!

Nakuonesheni tatizo la kupata ushahidi sasa unapokuja kumu-*accuse* mtu huna ushahidi utafanyaje maana yake sheria za utumishi hazikubali lazima uwe na *evidence* ili tumchukulie hatua watu wetu wengine hawataki kutoa ushahidi hawashiriki. Hili nalo ni tatizo naiomba jamii yetu tumeleana vibaya jamii yetu tumefanya udugu ni mkubwa zaidi kuliko ubinaadamu wakati mwengine, hili naliomba sana tuwasaidie, nilikua na daktari Ali Mnazi Mmoja anambia nimemchukulia hatua daktari baada ya kuona mambo aliyofanya.

Anasema watu walimwendea nyumbani kumuomba achaane na hilo tatizo na hilo tatizo na hili jambo na hio hatua aliyoichukua mpaka mwenyewe akapata tabu, lakini kosa lako unasababisha maisha ya mtu. Kwa hivyo, nalo vile vile lazima tukubaliane mila zetu na desturi zetu zinasaidia au zinasababisha watu kuwa *not-efficient* katika kazi zao, lazima tubadilike aliyekuwa haheshimu taratibu za sheria na kazi achukuliwe hatua tu tuache muhali, muhali umetuharibia nchi.

Kazi kubwa iliyofanyika tumekwenda kwenye mkutano wa kitaifa tumejitapa kwamba sisi tumeweza kupambana na malaria tuko 0.4% mpaka leo na tunataka kuimaliza kabisa tuna *record* nzuri duniani pamoja na sisi wenyewe hatujui, tuna *record* nzuri duniani kama tumefanya vizuri, tufanya vizuri kwenye maradhi mengine haya ambayo hayatambuliki sana tuko kwenye 0.4% . Sasa hivi tunataka kuhakikisha tunamalizana na

cholera katika nchi yetu kipindupindu tunataka kupambana na *cholera* kipindupindu kwa nguvu zetu zote. Haya ni matunda ya Chama Cha Mapinduzi yalianza na Afro Shirazi ndugu yangu Hamza unga mkono tu hoja tumalize kazi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, watu wamezungumzia sana suala la hospitali ya Binguni nataka nimshukuru sana Mhe. Rais na mimi naomba sana musome muongozo wa CCM nikutoleeni *copy* nyote nikupeni ni ilani ya CCM ilinayosema tujenge Binguni, na katika eneo ambalo bado hatujafanya vizuri ni la Binguni, na ndio maana Rais akaagiza yafuatato:-

Kwanza akasema eneo lote kalipimeni mulieke mipaka tumemaliza kulipima tushaliweka mipaka yote. Pili akasema nendeni mukaeke ngozi, tukatumia pesa tulizinazo zile tukaenda tukaekea nguzo. Tatu akasema chukueni ramani ya zamani ambayo wachina walipendekeza kujenga tuangalie namna gani itafaa au haifai gharama yake mradi mzima ni dola milioni 200, hichi tunataka 2020 tumkabidhi Mhe. Rais mradi huu Mhe. unaondoka salama na Binguni hapa iko salama.(*Makofi*)

Tunamshukuru Rais amefanya ziara nchi za kiarabu ameomba misaada na wamekubali kutusaidia sehemu katika hili tumekaa sisi tumezungumza na ndugu zetu wa kichina, tumezungumza wengine na makampuni mengine wako tayari kuangalia *package ya program* wataichukuaje ili tuikamilishe katika kipindi cha miaka miwili na nusu iliyobaki, nakuhakikishieni kabisa mungu akipenda Binguni itasimama tukijaaliwa.(*Makofi*)

Kwa hivyo, wale wanaobeza wanafikiri tunatembea na makaratasi, hatutembei na makaratasi mradi wa dola milioni 200 sio mchezo, hatutembei na makaratasi 200 *million dollars project* sio kitu kidogo hata kidogo. Kwanza huyo kiongozi kufikiria hilo jambo tumshukuru nani katika hali ya umasikini tulionao leo akafikiria jambo kubwa kama hili, lakini ana mawazo ya muda mrefu mawazo muhimu ya kuona taifa hili hatimae itakuwa nini, nini maana yake hii tulikuwa Cuba juzi, katika kitu wenzetu walichofanikiwa ni *health industry* wao hawazungumzii matibabu wanazungumzia *health industry*. Ukitaka madaktari wengi nenda Cuba, ukitaka *nurses* nenda Cuba, ukitaka orderly nenda Cuba, kwanza wao hakuna ku-*retire* , leo tuna madaktari wanane kutoka Cuba wapo hapa.

Tuna vijana wetu wanane tumepeleka kesho kutwa tunapelea saba 15 Cuba kusoma, tunataka *specialization* tubadilishe huu mfumo wetu wa madakatari tulionao tatizo moja ambalo nakubaliana na nyinyi kabisa tunao wataalamu tunawaita *specialist, unfortunately* hawataki kujitahidi kufanya mazoezi na hili ndio tatizo la msingi tulilonalo lakini tume-*manage* leo *euro department* yetu hapa imepata *recognition* katika Afika hii tunafanya *operation* mkubwa sana hapa sasa hivi kuliko pahala popote hapa Afrika, kwa ndugu zangu kutoa Spain wanakuja hapa wanaungana na sisi na vijana wetu tunafanya kazi tuna *train* vijana wetu sasa waweze kuingia katika *field* hiyo.

Ninachowaomba madaktari ma-*specialist* wajitahidi sana kufanya mazoezi waende muhimbili wakafanye mazoezi wakija madaktari hapa washirikiane nao kufanya mazoezi tunapata madaktari kutoka nje wanakuja *camp* 13 tulizoziweka hapa wametibu watu wa

kutosha kabisa naamini tukiendelea na *exercise* hio tutabadilika kadiri inavyowezekana lakini vijana wetu nao wabadilike katika *active* ya kufanya kazi.(*Makofi)*

Hiyo ni kazi ya Rais ameanzisha *research institute* hapa sasa hivi ndio yale majengo manayoyaona pale Binguni waliojenga wale ndugu zetu wa *Africa Muslim Agency* yamechukuliwa, sasa hivi *research institute* itahamia pale bajeti hii mukiipitisha tunaanza angalau majengo mawili matatu kwa haraka sana wahamie tuanze kufanya kazi ya utafiti wa mambo ya afya. Wizara ya Afya Cuba inatafiti vyuo vya utafiti 13 Wizara ya Afya peke yake. Kwa sababu afya bila utafiti hakuna na moja ambalo tumegundua tumegundua dawa sasa hivi *vex-vaccine* waliogundua Cubans kwamba sasa ukiwa mgonjwa wa sukari badala ya kumkata mguu au mkono kwa sababu ya kuoza unamu-*inject* tu na anapona 72% wamefanikiwa katika hilo. (*Makofi*)

Tumewaomba watashirikiana na *research insitute* yetu sisi waweze kutupatia dawa zenyewe lakini hatimae na *vaccine* na sisi tuzalishe hapa hapa Zanzibar. Hizo ndio *effort* za daktari Ali Mohammed Shein. tumpeni *support* Rais tumpeni *full support* kama kuna mtu anaumwa na Wizara ya Afya anaumwa na maendeleo ya nchi hii, Dkt. Ali Mohammed Shein anaumwa sana.(*Makofi*)

Ndio wengine tukajitoa muhanga saa nane saba za usiku hakuna kulala tuhakikishe kama tunatoa huduma kwa watu hebu tumuungeni mkono. Hasa ukitoka Chama Cha Mapinduzi huwezi kumuacha usimuunge mkono, kama mimi wa ADC nimejitoa 100% wewe utashindwaje kujitoa 100% naomba sana, nirejee. Nasema kama mimi wa ADC nimejitoa *more than* 100% wewe wa CCM utashindwaje, hakuna cha buti hapa nakuombeni sana hoja zenu zote mlizozisema hapa Naibu Waziri kajibu sehemu lakini majibuyake rahisi ni changamoto tutazichukua na hatua ambazo tutachukua kurekebisha njooni mutuilize mwakani sio leo.(*Makofi*)

Leo nikikujibu nitakujibu tu lakini msingi wangu mkubwa ni *program* ambazo tumeziingiza kwenye bajeti ndio zitajibu changamoto ambazo zisemwa, amesema Mhe.Waziri Mohammed hapa. Kama hutukwenda kuzitekeleza bado maswali yatabaki pale pale. Tupeni fursa tukafanye kazi tukatekeleze muone kama kweli ilani ya CCM hakukamilika 100% ili mwakani muingie kwenye uchaguzi nyinyi 2020 iko karibu, na katika kilio kikubwa cha wananchi ni afya maji.(*Makofi*)

Let us address those issues na mimi nasema tuko tayari kuzi-*address* nakuhakikishieni kabisa nchi hii iko salama, chini wa uongozi mwenye hekma na busara wa Dkt. Ali Muhammed Shein nchi yetu iko salama. Nyinyi hamuoni fakhari hata wanasema wataapishwa hawasemi tena sasa kama wataapishwa hamuoni fakhari, viapo vimeisha nasema hata wale wanaosema wataapishwa kila siku asubuhi hawasemi tena sasa, au mnawasikia nyinyi mnawasikia nyinyi hawapo kwa sababu hakubagua mtu hata mmoja, nirudie. (*Makofi*)

Nasema hata wale waliokuwa asubuhi na jioni walikuwa wakiapishwa na viapo vinafutika halafu vinarudi tena hawafanyi tena wamebaki kusema kwenye vifuu sasa, lakini kwa sababu ya kazi aliyoifanya Dkt. Ali Mohammed Shein aloahidi kwamba

atawatumikia Wanzanzibari kwa nafasi yake na kwa uwezo wake wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Hili naomba na sisi tujifunze sana kila mmoja alipo atimeze wajibu wake bila ya ubaguzi wa aina yoyote.(*Makofi*)

Wanaotaka ajira tuwape ajira kama nafasi zipo mradi ana *qualification* na utaalamu wake tumpe nafasi, anayetimiza wajibu wake hata kama rangi yake hatuipendi mwache atimize wajibu wake, maana nalo ni tatizo. Nilikuta mimi tatizo hilo hospitali daktari *very efficiently* anafanyakazi yake kweli kweli, lakini kwa bahati mbaya wenzangu wengine hawamtaki. Nauliza kwa nini aa maana yake sio mwenzetu, sio mwenzetu lakini anatibu watu wetu, au mwenzetu vipi zaidi ya hilo. Maana kiapo tulichokula hapa ni kuwapa huduma watu wote bila ya kubagua. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninachokiomba kwetu sisi tutimizeni wajibu wetu wa kikatiba, lakini kubwa zaidi kwamba sote safari yetu ni moja kesho tunakutana na Mwenyezi Mungu. Nilikaa na madaktari bingwa nikawaambia, ni aibu sisi leo tunatumia bilioni karibu saba kuwapeleka wagonjwa nje, tatizo ni nini maana ndicho kilio kimoja kikubwa. Wakaniambia tuna matatizo yetu, kwanza tuko wachache na pili hatuna vifaa na kadhalika. Lakini kubwa zaidi Mnazi Mmoja sio hospitali ya rufaa, Mnazi Mmoja imekuwa hata anayeugua mafua anakwenda Mnazi Mmoja. Njoo Mhe. Waziri uone, kwa hivyo mimi ni *specialist* badala ya kutibu matatizo ya ki- *specialist* natibu maradhi ya kawaida. Kwa hivyo, sipati muda wa kufanya kazi yangu *those are facts*. Huyu sio mkorofi.
inject
Mhe. Rais akasema kazi yako moja ya kufanya kubwa ni ku-*ingest* Mnazi Mmoja, punguzeni idadi ya kwenda kule. Nikashukuru sana Kamanda hapa Mhe. Haji Omar Kheir, namkabidhi vituo na vituo hivi tunataka kwenda na *policy* ya Cubans. Cubans wana-*Very Strong Primary Health Care*, yaani ukitoka kule chini kuna daktari kamili. Ndio maana Mhe Rais akasema tusomesheni madaktari kwa wingi. Tumepeleka vijana wengi *SUZA* wanasoma, tumewapeleka vijana wengi nje kusoma nakuhakikishieni katika miaka miwili au mitatu tutakuwa na madaktari wa kutosha hapa na wataalamu wa kutosha tutawapeleka vijijini wakaweze kufanya kazi vizuri zaidi, ili Mnazi Mmoja na hapo hatimaye Mkoani hospital iwe kweli ni hospitali ya rufaa, hiyo ndio mipango ya serikali.

Mimi nawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe, hebu hii *vision* aliyonayo Mhe. Rais twende nayo pamoja. Mimi pengine wengine siwalaumu kwa sababu ni hamjaielewa ndio nikaona nichukuwe nafasi hii niwaeleze kidogo, mwenzetu anatizama wapi na sisi tunatizama wapi. Anaitizama nchi katika maeneo tofauti kabisa, anasema *why Zanzibar Country like a Cuba*, kwamba sasa *health industry* ni kubwa. Niliwakuta mawaziri kutoka Quwait kila pahala, Cuba wanawaajiri madaktari wanachukua na ma-*nurse*, *why not Zanzibar*. Tunaweza tukawasomesha vijana wetu, mradi wakubali kusoma vizuri. Mimi nafikiri tukishirikiana pamoja tunaweza tukafanya kazi hizi pamoja.

Mhe. Naibu Spika, mafungu yote ya fedha niliyoyasema ndugu yangu Mhe. Mohamed Said Dimwa ninazo hapa takwimu zote, ukitaka nikujibu hapa hapa nitakujibu, kama unataka kwenye mafungu nitakujibu fedha zote zilizopangwa namna matumizi yake

yatakavyotumika ninayo. Lakini nafikiri baada ya maelezo haya inatosha. Msingi tulindeni sera yetu ya *ASP*, ndio iliyotukomboa leo tuko hapa ndani ya nyumba hii, tusingekuwa hapa Mhe. Hamza Hassan, kama sio *ASP* tusingekuwepo hapa, habari ingekuwa nyengine na CCM imeendeleza hapa. Kwa hivyo, tuendelee kuwakatisha tamaa wale wanaofikiri mkono utaanguka na fisi atautia mkononi, tuwakatisheni tamaa, haukatiki huu mpaka 2020. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nimetoa nambari yangu ya simu, tumetoa nambari ya simu ya Naibu Waziri, tumetoa nambari za simu za Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, kama kuna tatizo lolote tupigieni siku. Jana mtu mmoja kanipigia simu saa 6:00 za usiku akaniambia niko Mnazi Mmoja hapa nimekaa dakika 45 sijampata mtu wa *X-Ray* kunipiga *X-Ray*. Nikamwambia huyo daktari aliyekuwa hapo nipe nizungumze naye, akanipa nikazungumza naye. Aaa! Mhe. Waziri mimi ni daktari mdogo tu nimekuja hapa lakini daktari mwenyewe sasa hivi atatokea. Baada ya dakika tano tu daktari akatokea, kumbe maskini alikuwa ana dharura kidogo, akaja akamuhudumia akaondoka. Simu yangu iko wazi saa 24. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama ni kutembelea hospitali mimi natembelea kweli kweli na ushauri wenu wote mliotupa suala la usafi ni letu sote. Nataka nimalizie kwa hili, suala la usafi waheshimiwa ni letu sote. Tumshukuru Mwenyezi Mungu mara hii hatukupata *cholera* kwa juhudi zilizochukuliwa na wenzetu wa serikali za mitaa kusafisha na sisi tukapiga dawa, tuendelee na *exercise* hizi. Lakini suala la usafi ni kila mmoja wetu, kila mmoja wetu ana wajibu wa kuwa msafi kwa mazingira yako kwa ofisi yako, kwa pahala pako pa kazi, unapolala na kadhalika. Hili lazima tulifanyie kazi katika halmashauri yetu yote, ndio nchi yetu itapungua na matatizo tunayozungumza sasa, sio muhimu kuongeza madaktari, sio muhimu kuongeza hospitali, muhimu kuwa wasafi. Kwa hivyo, suala la vyoo vile vichafu na nini tuondokane nalo, hospitali hapatakiwi pawe chafu na majumbani hapatakiwi pawe pachafu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Afya wanyanyuwe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Naomba sasa nimwite tena mheshimiwa mtoa hoja Mhe. Waziri wa Afya.

Samahani Mhe. Waziri wa Afya. Kuhusu utaratibu naam Mhe. Mjumbe.

UTARATIBU

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri. Mimi mwenyewe na Mhe. Simai Mohammed Said kwa hotuba aliyotoa Mhe. Waziri, sisi tunaondoa jina letu la kupiga buti. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana. Mheshimiwa mtoa hoja Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU H01 - WIZARA YA AFYA

Kifungu H0101	Ofisi Kuu Pemba	65,964,000
Kifungu H0104	Idara ya Kinga	179,475,000
Kifungu H0106	Idara ya Uendeshaji na Rasilimali Watu	7,500,000
	Jumla Kuu:	**252,939,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU H01 - WIZARA YA AFYA

Kifungu PH0101	Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya	14,074,387,000

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia katika kifungu hiki niliomba ufafanuzi wa kifungu kidogo cha HH01010105 Huduma za Kuimarisha Kinga ya Jamii. Mwaka jana 2017/2018 kilitengewa shilingi 2,212,828,000, lakini mara hii kimetengewa shilingi 65,176,000. Nilikuwa nataka kujua tu, kuimarisha huku hatuwezi kuziimarisha afya tena au vipi mbona pesa kidogo sana ambazo mara hii kimetengewa.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, kifungu hiki mwaka jana ilikuwa kimepata fedha kutoka kwa wahisani na mwaka huu hawakupata fedha kutoka kwa wahisani. Kwa hivyo, tulichokifanya ni kuhamisha katika fungu la *OC* ile fedha ambayo tutaitumia katika mwaka huu.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, inawezekana ikawa pengine sahihi au si sahihi, hii sehemu nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri aje atupe ufafanuzi vipi vya kuweza au ana utaratibu gani, wana mikakati gani ya kuweza ku-

destroy hawa *mosquitoes* na nzi, ili kuweza kuondasha maradhi ya kipindupindu na mangineyo, wako katika utaratibu gani.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, sijui kama umemuelewa Mhe. Mjumbe.

Mhe. Waziri wa Afya: Ndio maana Mhe. Mwenyekiti, wakati najibu nilisema suala la usafi ndio la muhimu, na nikasema kwamba tunashukuru sana ndugu zetu wa manispaa wameanzisha kazi ya kubeba taka na kupiga dawa, hata idadi ya nzi wamepungua kiasi fulani. Kwa hivyo, tunaomba hiyo *exercise* iendelee, naamini kabisa tutaweza kupambana na suala la usafi, lakini nasema jukumu la kuwa wasafi sisi wenyewe ndio litasaidia tatizo hili ambalo analizungumza.

Mhe. Nadir Andul-Latif Yussud: Nakubaliana nae, lakini na wizara vile vile itie dawa kwa wingi Mhe. waziri.

Kifungu PH0101	Progaramu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya	14,074,387,000

Kifungu PH010

Mhe. Spika: Nawaona watu wanne, nitawapa watatu tu katika hao, ngojea tuangalie *list* yetu Mhe. Hamza, Mhe. Bi Panya Ali Abdalla na Mhe. Mohammed Said Dimwa Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo hukutia nia kwenye kifungu hichi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti naomba kwa ruhusa yako nilitia nia kuzuia fungu la mapato hospitali ya Mnazi Mmoja hatujafika lakini nitaomba unipe *priorty* kwa sababu Mhe. Waziri hakututendea haki kwa mujibu alivyotujibu maelezo yangu nitakuja kutoa hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hatujafika itakauwa unachukua nafasi ya mtu sasa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: *No,* hio ilikuwa natoa kama angalizo, kwa sababu unajua Mhe. Mwenyekiti, tatizo hizi nafasi zinakuwa adimu kupatikana. Mhe. Mwenyekiti katika fungu hili nilijaribu kuchangia katika hizi hospitali zetu ambazo tunazimbandisha hadhi za Wilaya, kwa bahati mbaya sana Mhe. Waziri alikuwa anasema lakini hoja zetu *specific* alikuwa hazijibu, sasa nilizungumzia hospitali ya Kivunge. Mhe. Mwenyekiti, maneno yote ambayo nilizungumza sikubahasha, tumekwenda *field* na tukaona. Kule yule daktari ambae anafanya *operation* sio daktari wa serikali. Hapa katika kuimarisha hospitali za vijiji na hospitali za rufaa naona mnatazamana hapo msije mkaniambia fungu silo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tatizo sio kuwa ndilo au silo. Tatizo ni kwamba unatuhutubia tena, tukifika wakati huo ...

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sasa hoja yangu ndio nasema Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hakutujibu kwamba yule daktari ambaye sisi tulipokwenda tumemkuta daktari

ambaye kaajiriwa na *NGOs*. Lakini vile vile hakuna *nurse* wala *orderly,* yule mfuaji wa nguo ndio kageuka *nurse*. Mhe. Waziri, hakujibu hoja zetu *specific,* alikuwa anapiga ulumbi tu hapa. Naomba jawabu.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri anakumbuka.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Hamza Hassan Juma mimi nakuheshimu sana. Kwanza nimesema tumeelezea *criteria* ambazo hospitali ile inaweza kuwa ya mkoa. Daktari aliyeajiriwa ambaye ame-*retire* ameajiriwa na *HIPS* ile *organization* inayotusaidia sisi, hakuajiriwa na serikali. Haijakataza serikali kuajiriwa mtu ambaye ame-*retire,* tuna *retired officer*s chungu nzima wana mikataba ofisini, tunawaajiri na wanafanya kazi. *As long* ni *efficient* anafanya kazi yake vizuri. Kutokana na upungufu wa madaktari tulionao tukakubaliana na ndugu zetu wale, kama kuna daktari anakaa kule kule anaweza kupewa fursa hiyo achukuliwe afanye. Wenzetu wapo *very specific* hawachukui mtu ovyo ovyo, ni *highly qualified* anafanya kazi yake vizuri.

Pili, tumepeleka madaktari sita sisi tayari Kivunge. Yule aliyekuwepo tumemuondosha kwa sababu kwanza hakuwa daktari wa upasuaji, tukasema tumlete hapa kwa sababu ni kijana *very efficient* ni mzuri apate mafunzo Mnazi Mmoja ili a-*qualified* na kazi anayoifanya ndio maana yuko Mnazi Mmoja hivi sasa. Lakini tumeshapeleka madaktari wengine sita Kivunge hivi sasa, tunataka kui-*promote* ile hospitali. Maelezo sikubabaisha hata kidogo.

Mhe. Hamza Hassan Juma miaka yangu yote zaidi ya 37 ndani ya Bunge na Baraza la Wawakilishi sijawahi kubabaisha mimi. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa kwa nini pale sisi hatuchukui daktari wa serikali, na daktari yule alikuwepo amemaliza muda wake ameajiriwa na NGOs baada ya kuajiriwa na serikali. Lakini Mhe. Waziri ananiambia amepeleka madaktari sita sasa itabidi hoja yangu niondoe niende nikafanye ukaguzi rasmi. Hoja yangu ilikuwa kuhusu suala la daktari, lakini pia na *nurse*. Maana yake yeye kasema amepeleka madaktari sita. Kwa sababu pale tatizo lilikuwa daktari pamoja na ma-*nurse* vile vile hapana. Mhe. Waziri labda atufafanulie sasa hivi katika kile kitengo cha upasuaji je, tumemshapata pale daktari bingwa? Lakini vile vile na wale wasaidizi wake tumewapata?

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa hatuivurugi CCM, wala hatuisemi CCM, tunazungumza watendaji wa serikali ambao wanapewa dhamana na CCM wafanye wajibu wao.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tena. *HIPS* ni *NGO* iliyofanya mkataba na serikali, na *HIPS* wanaleta sio tu madaktari hawa tunaowachukua sasa hivi, wanaleta hata wanafunzi ambao tayari wanakuwa kwenye kufanya *research* wanakuja wanafanya kazi na sisi chini ya madaktari wetu. Ni mpango na ni mradi wa muda mrefu tunaoendelea, wapo Makunduchi, wapo na Kivunge. Hilo la kwanza.

La pili, mimi naomba nimhakikishie kitu kimoja, tukimaliza hizi shughuli twende pamoja Kivunge. Kama unafikiri napiga nadharia, tukimaliza shughuli twende Kivunge tukaone hali halisi ilivyo, hata leo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mheshimiwa tutakwenda tuendelee.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kushukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake. Lakini bado na mimi tatizo langu liko katika hospitali ya Kivunge kwa daktari huyu huyu wa upasuaji. Kwa sababu hapo hospitali kwa hakika kunatofautiana kati ya lugha ya Mhe. Hamza Hassan Juma na lugha ya kwangu. Kwa sababu mimi namkumbuka daktari Maulid Abdalla Khamis ambaye alikuwa anafanya upasuaji na ni kijana mzuri sana. Lakini kwa kipindi hichi hayupo na sisi wananchi wa kijijini kule tulikuwa tumeitikia wito mzuri kabisa wa kwamba tupunguze msongamano katika hospitali ya Mnazi Mmoja na tupate huduma katika hospitali zetu za vijijini na hilo lilikuwa linawezekana na lilikuwa liko vizuri. Sasa nataka kujua, kwa sababu wananchi wa Kivunge wa Mkoa wa Kaskazini, wana mategemeo makubwa ya daktari wa upasuaji pale na tushategemea, kuonekana daktari huyu hatumuoni na wala hatujui yuko wapi. Kwa hivyo tunapata shida na tunataka kujua lini wanatufikiria kutuletea daktari ambae ataweza kutatua shida zetu hizi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwanza daktari Maulid namfahamu sana mimi ni mchapa kazi mzuri, lakini sio *surgic*, si daktari wa upasuaji, akikamatwa na kesi yeyote ya upasuaji, tuna hatia, tulichokifanya ni kumchukua tukampeleka Mnazi mmoja apate *training* asomeshwe maana yake pale tunafanya na *training* vile vile, tukapeleka madaktari wengine sita. Sasa kama kuna mashaka ya hilo najua anapendwa sana, hata mimi nampenda sana kwa kazi, hata mimi nilisikitika, kwa nini amehamishwa, wakanambia sio *surgin*, anachukua kwa sababu ya mashida tulionayo na *risk* kufanya hiyo kazi, ndio hayo tunapata mtu kakatwa mkono, kafanywa nini, kafanywa nini, unampa mtu ambae sio *professional*. Tukasema hatuwezi kuendesha uhai wa binaadamu kwa kubahatisha tumpe mtu na *profession* yake afanyekazi kijana hodari mzuri, tena *doctor* Jidawi aliniambia Mimi mwenyewe nimem–*train* huyu kijana *he is very good*, tumlete hapa Mnazi mmoja apate *training*, yuko hapa Mnazi mmoja anafanyakazi vizuri na atapata taaluma. Madaktari sita tumepeleka pale kama kuna tatizo jengine tutakwenda kutatua tu tupo pamoja mimi na wao.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe Mwenyekiti. Hee, Napata mshtuko sana kama tunafanyiwa majaribio kwanza napata mshtuko. Lakini kwa kijana huyu alivyo na waziri anavyonijibu nashukuru, kwa sababu akim-*train* kidogo yuko vizuri sana huyo kijana, anaweza akawa msaada kwetu sana, lakini tu nilitaka kujua kama hii shida imeondoka tayari daktari wa upasuaji tunae na hatubabaiki ili tukaweza tena kuja mjini, kama unavyojua tunawasumbua sana wananchi kutoka shamba kuja mjini. Ikiwa daktari yupo mimi sina matatizo, lakini kama daktari wa upasuaji hatuna, namuomba sana Mhe. waziri atumie busara zake zote ili aupunguze msongamano katika Hospitali ya Mnazi mmoja.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa na vifungu viwili sijui utarihusu niseme vyote au kimoja kimoja, ya maelezo ya vifungu vina pesa nyingi tu. Sasa nilikuwa nataka niseme vyote:

(1) Kifungu HH01020101 - Huduma za Hospitali za Wilaya, Wilaya na Hospital za Rufaa

Kilichopangiwa 2017/2018 imepangiwa shs. 15,360,581,000 lakini mara hii kimevuka mara mbili zaidi shs. 33,806,154,000. Hicho kimoja nilikuwa ninataka nijuwe ufafanuzi wake hasa pesa hizi tunazipeleka huko kwa nini, halafu nitasema hichi chengine.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nimelitolea maelezo nilisema ongezeko mnaloliona kubwa limeongezeka, kwanza ni bajeti yetu kwamba imeongezeka, pili tunataka hizi huduma ziboreke, sasa huwezi kuboresha huduma bila ya kuwa na fedha, ndio *increase* ya hii pesa iliyoko.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. waziri lakini hoja yangu hizi pesa ni nyingi sana, na hizi ni pesa za wananchi tunazipeleka, maradufu zimeongezeka kuliko mwaka jana, *commitment* ya serikali nini atapokuja kwenye bajeti ya mwakani, hichi alichokipanga tunaweza hapa tukamsulubu kwa sababu tunataka *commitment* ya serikali kwenye fungu hili.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kama alinisikiliza vizuri kabla ya pesa kupewa Mhe. Rais alitwita, alitwambia hizi pesa mnakwenda kuzitumiaje, nataka mniridhishe tukakaa nae siku nzima, tukampelekea na *program* zote akaridhia, ndio maana tukaileta kwenye bajeti hii sisi. Kwa hivyo, *commitment* ya serikali ipo wala si yangu peke yangu ya serikali nzima, tunaisimamia bajeti hii serikali nzima, na mdhibiti na mkaguzi wa serikali yupo atadhibitisha yale ambayo tunayatumia, na PAC ya Bunge ipo, ya Baraza la Wawakilishi itathibitisha yale ambayo tunayatumia. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, muhimili wa serikali na muhimili wa Baraza upo kitu kimoja tofauti, wanapokaa na Mhe. Rais anaweza akawakubalia hivi na hivi na hivi, lakini hapa tunapitisha za wananchi, nakubaliana nalo hilo, lakini litakapokuwa *condition* itakapokuja mwakani wameomba pesa zaidi hii, Mungu atapotuweka hatujaona mafanikio yeyote pesa hizi pengine zisipite. Naomba niende kwenye hoja ya pili hilo nimeliruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, Hoja yangu nyengine ni:-

Kifungu HH01020202 - Huduma za Uchunguzi wa *sample* za *ZFBA.*

Mwaka jana imepangiwa shs. 120,000,000 lakini safari hii zimezidi zimekuwa ni shs. 1,135,100,000 sasa nilikuwa nataka kujuwa *sample* gani zinaweza kuchunguzwa na mbona pesa hizi zimezidi sana kuliko mwaka jana, kuna vitu vingapi, pengine kuna maabara au nini, nini imefanywa tungeomba maelezo ya kina.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2017 walipata ruzuku, na mwaka huu mbali ya ruzuku shs. 335,000,000 lakini mishahara yao pia imeingizwa hapa. Kwa hivyo ndio maana kuna tofauti ya hizi pesa. Mwaka jana hatukupata ruzuku, mwaka huu kuna ruzuku na halafu kuna mshahara umeingia hapa kwenye shs.1,135,000,000.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kunakuwa kuna *contradiction* kwa sababu unapotia vifungu hivi vidogo kwenye sehemu moja na bila ya maelezo ya kudumu ndio huwa tunapata wasiwasi, lakini hili tutalipeleka na itabidi tuliandikie vyengine kwenye Kamati ya Bajeti tukikutana na serikali si kupunguza fungu lakini kuandika vizuri huku mwanzo wa kifungu hichi. Kwa sababu unapotia mishahara hapa sisi tunapata wasi wasi. Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu PH0102 Program Kuu ya Huduma za Tiba

Jumla ya Program Kuu ni shs. **60,574,595,000**

Kifungu PH0103

Mhe. Mwenyekiti: Basi nitaanza kulia nitamalizia kushoto kabisa nitaanza na Mhe. kwahivyo nikutajeni kabisa, Mhe. Kwaza, Mhe. Suleiman Makame Ali, Mhe. Hamza, Mhe. Nadir, halafu tutamalizia na Mhe. Dimwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, niliweka nia ya kuzuia mshahara wa Waziri, na nia yangu ipo, na hoja yangu hasa waziri hakunijibu, na kulikuwa tatizo la malimbikizo ya *call allowance* kwa hospitali mbili nilizungumza, (1) hospitali ya Mnazi mmoja (2) Hospitali ya Kivunge. Lakini walinzi hospitali ya Kivunge, sasa nikasema kwa kuwa wenyewe Mnazi mmoja wameshindwa na wanawafanyia kadhia hii watu ambao wana haki za msingi, za kulipwa malipo haya, nikasema nalishulikia hili fungu la Mhe. waziri anipe tu *commitment* yake kuwa atalisimamia vipi hizi haki zao za msingi kwa hawa watu wa hospitali ya Mnazi mmoja, ili haki yao kama wanavyopata wafanyakazi wengine wapate basi sina tatizo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninakubaliana nae kuna *delay* imetokea miezi mitatu ya *call allowance* baadae wiki mbili zilizopita tukaa na watu wetu wa hazina na tukalitatua hilo tatizo na ninamuhakikishia kabisa kama tuna tatizo lilibaki niko tayari kuchukua *commitment* kuweza kulimaliza.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwanza nakushukuru kwa hiyo hatua ambayo umesema umekaa na hao watendaji wako lakini kadhia hii, ni mbaya na wanaofanyiwa ni madaktari tunaowategemea kwenda kuwatibia watu wetu. Sasa isiwe ndio tu mpaka tunasubiri bajeti watu hawa wanalipwa, maana imekuwa kama Wizara ya Mawasiliano ndio wanaziba mashimo sasa hivi njia ya *Aiport*, sasa tusifike pahala tukaenda huko. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mimi niko kwenye HH01030301 kwenye Uratibu wa Utekelezaji shughuli za Wizara ya Afya Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna kuratibu shughuli zote za kiutawala kinga na tiba. Nilipokuwa nikichangia nilizungumza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo alikwenda kufungua kituo cha Afya Ndagoni, naipongeza sana serikali, kwa kuwaondoshea wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo aliahidi kwamba daktari yule atampatia Vespa na aliahidi na ahadi ya Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ilikuwa ni Waziri ni ahadi ya serikali, na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ameshaondoka lakini napita ametoa agizo wameniletea kimemo hapa kwamba alitoa agizo kwamba agizo lile halikutekelezwa. Mhe. Hamad Rashid nampongeza sana kwamba alisema kuna hulka, ni kweli kutokana na agizo hili, kuwa Mhe. Waziri alitoa agizo lakini halikutekelezwa. Kwa hivyo mimi nilitaka nijuwe tu, ni lini Vespa ile atakabidhiwa yule kijana, ili aweze kutoa huduma kule Ndagoni. Wananchi wetu wa Ndagoni wapate kunufaika na serikali yao ya Mapinduzi Zanzibar. Ahsante Mhe. Wenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba huduma hizi tumeshazigatua, lakini bado nitashirikiana naWaziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Vikosi vya SMZ ili tuone ni namna gani tutamsaidia Daktari huyo apate usafiri. Tutahakikisha hawa watu wetu wote wanapata usafiri wa kuweza kufanyia kazi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, *inshaallah* tupo tutaona, na tutaendelea kuhimiza hilo *inshaallah*. Tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa nina suala dogo tu. Lakini Mhe. Waziri kutokana na muda pengine hakuwahi kulitolea ufafanuzi. Nilielezea kwamba mpango unaofikiriwa na Wizara ya Afya kuhusu suala la kuacha kuajiri Ma-*orderly* na kuajiri kampuni binafsi kwa ajili ya usafi katika hospitali zetu sasa kwa bahati mbaya sana Mhe. waziri linaonesha pengine alipo *note* hakulitaja, *at list* nipate ufafanuzi tu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimemfahamu sana Mhe. Hamza Hassan Juma, kwanza niseme Mhe. Mwenyekiti, utamaduni uliozoeleka sasa hivi, kwa *outsource* baadhi ya huduma zinazotolewa katika sehemu nyingi, ukenda Muhimbili pale utakuta wame *outsource* watu wakutengeneza bustani, wame-*outsource* watu wa kusafisha na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kugundua kwamba kuna tatizo moja kubwa sana la kuona kwamba watu wetu ambao wanapewa hizi huduma hawawezi kuzifanya *efficiently* na hospitali zinaendelea kuwa chafu tukasema hebu tu-*outsource* na serikali ikaona ni jambo jema tukasema na ndio maana tumekubaliana kwamba tu–*outsource* zile *service* ambazo zinaweza kutusaidia. Lakini tunavyofanya hivyo tunafanya nini, tunaangalia ndani ya vikosi vyetu sisi tulivyo navyo kwanza, katika hizi taasisi zetu tulizonazo, kwa mfano: tuna walinzi wa JKU nakadhalika wanafanya hizo kazi, tuna *outsource* watu wazuri lakini wapo kwenye taasisi za serikali, ndio maana halisi tunataka kuzifanya, tutafute ambao wataweza kusimamia kazi hiyo kuweza kuifanya kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikupe mfano wa pili, nimekwenda Mnazi mmoja nikuta kuna taka nyingi sana, nikaenda kwa wenzetu wa mafunzo tuka-*outsource* kwao wakaja wakatutufanyia usafi. Kwa hivyo hizo ni kazi ambazo zinafanyika kwa kutumia hizi taasisi ambazo zipo ndani ya serikali, usiwe na wasiwasi Mhe. Hamza hakuna atakae kosa ajira katika watu wetu. Ma-*orderly* wetu wanafanya ndani hawa watakuwa wanafanya nje ya Hospitali yenyewe. Ma –*orderly* wataendelea kuweko kule ndani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika sana na kauli ya Mhe. waziri kwamba wale vijana wetu sio kama watatolewa kazini wataendelea kufanya kazi, isipokuwa hizi kazi ambazo watakazo zi *outsource* kwamba tutazitoa kwa taasisi zetu za serikali, kwa bahati nzuri tuna idara maalum ambao wana vijana wengi ambao wanakwenda kujitolea lakini, vile vile kuna mambo ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili ni suala ambalo Mhe. Waziri amelizungumza, jee, kuna muongozo wowote ndani ya wizara wa kimaandishi kwa sababu tatizo letu anaweza akasema yeye, kama tunavyojua leo yupo kesho hayupo, tunataka atupe *commitment* jee, hili suala lipo kimaandishi kwamba hizi kazi zipewe taasisi za serikali? Kwa sababu pale kama tunavyozungumza ile ni dhima kubwa kwa ajili ya siri za wagonjwa *ethic* vile vile za wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba tu wajumbe wakasome maamuzi ya Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii mwaka jana waliaazimia hili jambo,kwa hivyo sio la serikali hata kama yenyewe hapa imetoa maamuzi na Baraza hili likaridhia, kwa sababu taarifa ilisomwa hapa ndani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, samahani Mhe. Mwenyekiti, kamati ya Baraza tunashauri mambo mengi lakini hayatekelezwi mengine, sasa ndio maana nikasema, sawa kamati ilishauri, jee serikali imetoa muongozo kwa sababu najua tatizo *commitment* pale Mkurugenzi ee, au Katibu Mkuu, kama hakuna andiko hawezi akafanyia kazi vitu ambavyo alivisikia au vipi, kwa hivyo nafikiri ule muongozo wa serikali jee, upo kimaandishi. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie kabisa serikali hii inaheshimu sana sana maamuzi ya lako, sana kabisa kabisa na mimi naomba ni *sort down* hii kazi tunayoifanya hapa ni matokeo ya michango yenu mnayoitoa hapa ndani. Rais anasikiliza kila kipindi kinachotokea anasema kule wajumbe wanasema, kwa hivyo maamuzi yaliyotolewa na Kamati halafu yakaja hapa yakapitishwa na Baraza hayo ni maamuzi sio wenyewe tupo ndani ya Baraza hili hili lazima tuyaheshimu. Nakuhakikishia kabisa wala usifikirie maamuzi mengine. La pili Mnazi mmoja ina *board*, wakishapata maamuzi kama haya yanakwenda kwa utaratibu wao kwenye *board* yao inapitisha *board*, halafu *board* kazi yake ni kumshauri waziri, waziri wananiletea na mimi naipeleka serikalini ndio utaratibu wa kiserikali. Mhe Hamza usiwe na wasiwasi, kabisa kabisa, nakutoa wasiwasi kabisa kila kitu kitakwenda vizuri.

Mhe. Nadir Abul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kumalizana na kabisa na Mhe. waziri kwa sababu kama nilivyoeleza kwenye mchango wangu kwamba anapiga kazi, mtu haki yake apewe, lakini na hata kwa *speech* aliyotupa leo ingekuwa tunagombea urais mimi na yeye angekuwa keshanishinda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kuna mambo mawili naamini kibinaadamu inawezekana kayasahau wakati nilipokuwa nikichangia. Nilizungumza kwamba siamini wala haitotokezea kwamba hospitali ya *Al-Rahma* au *Global* kwamba wawe wataalamu au wawe na vifaa kuliko serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia hospitali ya Mnazi mmoja. Kwa nini nilizungumza, Hospitali ya Mnazi mmoja ambayo inatibu wananchi wote hasa watu wanyonge, ina mashine moja au labda iliyokuwa kubwa ziko moja moja, au unakuta labda mbili nikazungumza kwamba wana utaratibu gani, wafanya vipi kwenye mashine za *CT Scan, MRI* na nyenginezo kuwa angalau wanazo tatu tatu, *in case* imeharibika moja wana nyengine. Hii imetokana kwamba wananchi wanyonge wanaumia sana kwenda kutoleshwa shs. 200,000. Shs. 400,000 hospitali nyengine. Ni lini sasa utaratibu wao wakuweza kuleta mashine zile nyingi kwenye hospitali ile.

Mhe. Mwenyekiti, Lakini jengine ambalo nataka kumalizana nae nilizungumza kwenye Kituo cha Chaani Masingini cha Jimboni mwangu kijengwe kipya, mimi nilimwambia na nilisema kwamba nitazuia fungu asilimia 20%, ili aje anipe majibu tutafanya vipi, kwa sababu sehemu ili ina raia zaidi 9000, ambao wanahitaji matibabu na hakuna kituo. Mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Chaani nipo tayari kutoa matofali 8000 na mifuko ya saruji 200, ili tuweze kujenga kituo kile. Sasa nasubiri Mhe. waziri anambie na yeye kama wizara wataanza kujenga *foundation* au kuweza kutafuta wafadhili tukijenge kituo kile *before* 2020. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, Bahati nzuri tumeingia katika Uchaguzi Rais wa CCM, kapata kura nyingi, kwa hiyo mara hii utanipa nami.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nishukuru sana hili la pili, la kusema kwa yuko tayari kusaidia kutoa matufali 8000 kuanza ujenzi, na sisi kwa upande wa serikali tutampa *support* ya hali ya juu na siku itakayoanza ule msingi pale nami niko tayari na Mhe. Haji Omar tuje pamoja pale kwa sababu tushagatua kitu ili tuone kabisa juhudi zetu za pamoja tunawezesha wananchi kuweza kuweka kituo. Kwa hivyo hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili la mashine hizi anazosema ni kweli ni muhimu sana kuwa na mashine mbili, tatu. Lakini mashine hizi kama huna watu wakuzihudumia ni tatizo. Nitakupeni mfano ulio hai. Mkoani hospital kuna vifaa hivi sasa vimewekwa pale havina wataalamu wa kuvihudumia, kwa hivyo suala la kuwa na vifaa jambo moja, la kuwa na watu wa kuvihudumia ni jambo la pili. La kwanza hivi tulivyonavyo tuhakikishe tuna wataalamu wa kutosha wa kuweza kuviendesha la pili, tuhakikishe vile vile, hivi tulivyonavyo kama kweli vinatumika kikamilifu halafu tuagizia kitu chengine cha ziada badala ya kuagizia mashine tukaiweka tu pale kungoja ikaharibika. Ukiweka hitumii kwa mashine za kisasa hivi ambazo *digital* mara nyingi ukichelewa kidogo tu zinaharibika inabidi uagizie mpya.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa utaratibu huo naomba tukubalieane tu. Kwanza hizi ziliopo tuhakikishe zinafanya kazi, zina watu wa kuzihudumia sawasawa nitakupa mfano tu tuna *radiographer* mmoja tu sasa hivi, haiwezekani lazima tuwe na watu zaidi wa kufanya kazi. Kwa hivyo nasema tatizo la kwanza hebu tupate *human resource* ya kutosha, halafu tuhakikishe vifaa tulivyonavyo tunavitumia vizuri, wazo lake siyo baya hata kidogo pale ambapo tuna mahitaji tutafanya tu Mheshimiwa. Nakushukuru sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mheshimiwa, moja nimeridhika nalo la hospitali yangu ya Chaani, lakini kutokana na wingi wa wananchi ambao wanatibiwa ndani ya hospitali ya Mnazi Mmoja *a special* imetokezea ajali mfano ya basi kama iliyotokezea juzi Muyuni watu wamepata ajali zaidi ya ishirini pengine katika wale kumi wanataka *CT Scan* au wanataka *MRI* tuangalie moja itaweza kuweka *waiting list* wagonjwa wangapi. Sasa ningeomba hata kama hakuna *specialist* wakasomeshwe au tuajiri kutoka sehemu yoyote mpaka wetu sisi warudi na mashine *at least* tuwe nazo mbili au tatu kama tulivyo kwa sababu wananchi ni wengi lakini Mhe. Mwenyekiti tuendelee nafikiri Mhe. Waziri atalifanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kumalizana na Mhe. Hamad kwa sababu bado nimechangia na nimetoa nia nyingi sana. Mheshimiwa hapa nilizungumza sera na hapa nitazungumza sera sizungumzi kifungu, nilisema kuna nyumba za madaktari wakati mimi nikifanya kazi pale nilikuwa nazijua zipo Vuga, Michenzani, Kikwajuni, Kwamchina mwanzo, Mchina Mombasa na sehemu nyingine. Nyumba zile nilikuwa nataka kujua ziko wapi, Mhe.Waziri hakunijibu hapa alipokuwa akijibu nilikuwa nataka kujua je bado zipo kwenye milki ya Wizara ya Afya au ziko wapi kwa sababu Madaktari wanapata taabu sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nakumbuka limejibiwa na Naibu Waziri lakini nitampa nafasi ili akujibu. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Wakati Naibu Waziri anajibu yeye alikuwa hayupo ndani. Nyumba zile zote nilisema ni 32 na Vuga unaposema zipo nyumba 4, hizo nyumba ziko Majenzi, Majenzi ndio waliipa Wizara ya Afya. Kwa hivyo mmiliki hasa halali ni Shirika la Nyumba wakati ule tulikuwa tunaita Majenzi, ndio wametukabidhi sisi tutumie hizo nyumba, kwa hivyo zipo katika misingi hiyo si za Wizara ya Afya kwa maana hiyo, lakini sisi tumekodi kwao tunatumia kutoka kwao.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mheshimiwa napata kigugumizi au ukakasi, kwa sababu kuna nyumba hizi watu walirithishana juu kwa juu walipigiana matiktaka na ninazijua sasa kama si za wizara ya afya ni za Majenzi basi pengine wamepewa na Majenzi sawa tuendelee.

Kifungu PH0103	Program kuu ya uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Afya	18,604,017,000
Jumla Kuu		**93,253,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi

bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU - H02 Hospitali ya Mnazi Mmmoja

Kifungu H0201 Kitengo cha Uongozi na Utawala

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kuweza kunipa nafasi hii, nilipokuwa nikichangia mchango wangu nilitoa takwimu za huduma ambazo zinazotolewa na Bima ya Afya kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja nilisema wagonjwa walikuwa karibu 4,600, hospitali ya Arahma 30,500 na Hospitali ya Global wagonjwa 39,000 sasa Mhe. Mwenyekiti nilizungumzia sijaridhika na mapato yanayokusanywa na hospitali ya Mnazi Mmoja, sasa bahati mbaya sana Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi alikuwa anataka kutugombanisha na Chama chetu cha Mapinduzi lakini vile vile na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa aliposema kwamba sisi sera yetu ni elimu bure, akasema turudi Kisiwandui, Mhe. Mwenyekiti, sisi Kisiwandui tusharudi tushakaa na ndiyo maana tukapitisha sera ya Bima ya Afya, ukiangalia kwenye ukurasa wa 37 ambao kitabu hiki yeye mwenyewe Mhe. Waziri ndie aliyekuja kututolea ufafanuzi kwa hivyo amesema hapa kifungu cha 105 "kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, hii ni sera ambayo Chama cha Mapinduzi ilikwisha kuikubali lakini tatizo umekuwa mdorongo wa urasimu suala la Bima ya Afya kwa hospitali ya Mnazimmoja, suala hili tumeshalizungumza sana na ukiangalia hapa wakati kuna wafanyakazi hawa ambao waliokwenda wakatibiwa Al Rahma wapi ndio hawa hawa wakwezi na wakulima, mtu anapokwenda na kikadi chake cha Bima ya Afya anaweza kupata huduma. Lakini tatizo lililokuwepo mtu anapokwenda hospitali ya Mnazi Mmoja anapata kipimo kimoja vipimo vitatu anaambiwa nenda Al Rahma vipimo viwili anaambiwa nenda Global vipimo vyengine anaambiwa aende kile kiosk cha hapa Kilimani. Sasa Mhe. Mwenyekiti hili asiliseme kwamba labda turudi kwenye sera zetu za Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu akiri kwamba kutokana na *un-efficiency* ya hospitali ya Mnazi Mmoja ndiyo maana wagonjwa hawaendi pale, sasa atwambie hili atupe jawabu la uhakika sio atwambie turudi Kisiwandui. Mhe. Mwenyekiti hili suala mimi limeniudhi sana hapa tatizo tumesema serikali inatoa pesa nyingi sana tunaambiwa Bodi ya Madawa inatoa *hundred percent* lakini ukienda hospitali dawa hakuna tunataka maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Umefahamika Mheshimiwa nafikiri tumpe nafasi Mhe. Waziri ili aweze kujibu. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza Mhe. Hamza Hassan nataka nikuhakikishie kabisa sipendi kabisa mgombane na Chama cha Mapinduzi hata kidogo, ningekuwa napenda ilikuwa tufanye *sabotage*, lakini tusifanye *sabotage* kwa sababu nataka tufanikiwe na nchi yetu ibaki katika amani suala la vyama ni jambo jengine kabisa. La kwanza hilo la pili labda hakunielewa pale nilipokuwa naeleza

nilisema hivi, ni kweli Chama cha Mapinduzi chenyewe hasa ukisoma kwenye ilani ilimezungumzia suala la Bima, katika kutekeleza hili serikali imefanya yafuatayo:-

Kwanza tumeangalia sheria mwaka jana mnakumbuka mlibajeti bilioni 2 kukaundwa kamati za wataalam mbali mbali tukatengeneza sheria tukamaliza tukaangalia mifumo ya Bima ambayo inafaa katika nchi yetu, tukapeleka tupo kwenye *stage* ya serikali. Tatizo la Mnazi Mmoja lililotokea tulikuwa wakati fulani tunachangisha pale Mnazi Mmoja ndiyo maana mapato yakapanda, iliposimamishwa ile ya kuchangia mpaka utaratibu mzima ukamilike ndiyo mapato yakateremka tunachofanya hivi sasa wala siyo sababu ya vifaa na kadhalika.

Tatizo kubwa ni kwamba watu walikuwa wanachangia halafu tukasimamisha kuchangia mwezi wa Disemba mwaka jana tukasema hapana wacha turudi katika utaribu kwanza tuone je watu wetu watachangia au tutarudi katika bima kwa hivyo ni vitu viwili tofauti, suala la Bima na suala la kuchangia. Tatizo la pale tulikuwa tunachangia ndiyo mapato yakawa yanaongezeka siyo suala la Bima, suala la Bima mara hii tukasema basi wale ambao wana Bima wakienda Mnazimmoja na kwenyewe wapate huduma ya Bima kwa sababu wanazo Bima zao tayari kwa mfano Wawakilishi hao wakienda pale bima si iko tayari kulipa kwa nini wasilipe. Kwa hivyo tukawambia Mnazimmoja wekeni sasa utaratibu wa kuhudumia watu wote ambao wanataka kutumia bima watumie bima na siyo Mnazi Mmoja peke yake hospitali zetu zote sasa hivi tutaweka utaratibu wale ambao wana kadi za bima waweze kutumia kadi zao za bima ili serikali au shirika nao waweze kupata mapato.

Kwa hivyo ni vitu viwili tofauti kabisa wala sina nia Mhe. Hamza ya kuwagombanisha naomba muendelee vizuri mmalize ugomvi wenu, muimarishe chama chenu na mimi naimarisha cha kwangu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe.Mwenyekiti, kwanza nashukuru Mhe. Waziri kasema hana nia ya kutugombanisha na Chama chetu na nataka nimthibitishie kwenye Chama cha Mapinduzi wala hakuna ugomvi mambo safi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kwa sababu hapa tunataka kuisaidia serikali na kumsaidia yeye mwenyewe Mhe. Waziri, hoja yangu hapa hospitali ya Mnazi Mmoja tunaambiwa tusichangie sawa, lakini hii kwamba hatuchangii ina maana tunachangia mara mbili zaidi na nikatoa mfano unapokwenda mtu ana matatizo ya kusafishwa damu kule wanaita *Dialysis* Mhe. Mwenyekiti mpira ule wa kushughulikia kusafisha ile damu haupatikani anaambiwa nenda Global, Global analipa laki mbili na nusu kama tungekuwa tumeweka pale *donation* watu wakachangia shilingi elfu hamsini hamsini ingelikuwa haijambo au hata elfu thelathini lakini tatizo wanambiwa wananchi kwamba ile huduma inapatikana bure lakini bure pale anakwenda anapata huduma lakini sasa vile vifaa vinakwenda kununuliwa Global sasa ndiyo hapa hii hoja yangu, je hii katika bodi ya madawa katika huu mgao hakuna hivi vifaa ambavyo vya kusafishia damu kwa sababu *otherwise* kama hatuchangii bado wananchi tunawarejesha kule kule wanakwenda hospitali za serikali hawapati huduma, wanakwenda hospitali za binafsi wanapata huduma zilizokuwa bora.

Kwa hivyo hata ule utekelezaji wetu wa ilani hapa bado utakuwa hautekelezeki vizuri, sasa hapa ndiyo nilikuwa nataka maelezo je, katika yale maeneo ambayo hasa hili nililolitaja serikali mna mpango gani kwa sababu mpaka sasa hivi bado wanaendelea kununua hiyo mipira. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwanza vifaa vyote vya *Dialysis* tunavyo tumekamilisha kabisa hakuna kifaa ambacho sasa hivi hakuna kila kitu kipo kwenye stoo tunakuhakikishia kabisa. Ni kweli vilikwisha tukasimamia tukahakikisha kabisa havipungui.

Mhe. Mwenyekiti, Tatizo moja lazima tulikubali, tulikuwa na tatizo sana la ukusanyaji wa data mahitaji yetu hasa ni nini. Nakupeni mfano nilikwenda kwenye wodi ya wazazi nikawauliza hivi tunahitaji hii mipira ya kuzalia kina mama mita ngapi, nikaambiwa thelathini elfu ndiyo tunazoagizia lakini ukipiga hesabu pale haraka haraka unaona mahitaji ni 99 elfu nikajua hapa kuna tatizo la data, nikasema kumbe tuna tatizo la data. Kwa hivyo tumeagizia mipira siyo tena thelathini elfu tumeagizia laki moja na zaidi kuhakikisha kabisa tunayo *supply* ya kutosha kila pahali. Kwa hivyo tunasema kulikuwa na matatizo hayo sasa hivi tumeya-*unlock* nakuhakikishieni kabisa kila kitu tutahakikisha kabisa kipo kwa mujibu wa utaratibu tulioweka.

Mhe. Mwenyekiti, hiki tunachokizungumza sasa hivi ni kwamba hawa watu wenye bima wakienda pale hospitali ya Mnazi Mmoja wanataka kutumia bima yao watumie na wao bima. Mimi nina bima yangu na fursa ipo pale niende pale nikatumie bima yangu ndiyo hicho tunachokifanya sasa hivi Mhe. Hamza kurudisha utaratibu huu kuhakikisha yule ambaye anataka kutumia bima tuhakikishe kwamba kila kitu cha kuweza yeye kutumia bima kinapatikana hospitali. Anachosema ni kweli kabisa wakati mwingine tulikuwa hatuna vitu wanakwenda huku na huku, sasa tumeweka utaratibu tena pahala maalum kabisa anaetaka kutumia bima yake aende akatumie bima yake.

Nasema hili kwanini, kunatuna wagonjwa wengine wanatoka Tanga, wanatoka Dar es saalam, wanatoka sehemu mbali mbali wakija wanakuja na bima zao hata wageni tuweke utaratibu mzuri wa kupata haya mapato ambayo hakuna sababu ya kupata. Utaratibu wa nchi nzima kuwa na bima bado hiyo ni *process* ya serikali inaendelea na hatimae maamuzi yatatoka mimi naamini kabisa watu watakuwa na bima hatimae. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Waziri inaonesha sijui hizi taarifa wanazokupa watendaji wako zinakuwa sahihi, kwa sababu wiki moja tu iliyopita mwananchi wangu ananambia Mheshimiwa mama yuko hospitali unatakiwa mpira nimeambiwa tukanunue Global, leo Mhe.Waziri anasema hivi vifaa vyote vipo na vinapatikana bure. Sasa Mhe. Waziri hizi takwimu unazotupa labda wewe unazipata wapi maana yake mimi naweza baadae tukatafuta ile tarehe ya mgonjwa halafu tukenda pale ili sasa tujuwe inawezaekana kuna *sabotage* za chini kwa chini na ndiyo maana tukasema bohari ya madawa ukiangalia takwimu mwaka huu karibu bilioni nane zimetumika zile nne za serikali na zile nyingine lakini kwanini hivi vifaa vinakuwa havipatikani.

Mhe. Mwenyekiti hebu atupe Mheshimiwa hii aliyosema kwamba kule mpaka kwenye *Dialysis* vifaa vinapatika kuanzia lini.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tatizo lako lipo wiki moja nyuma, waziri anajibu leo inawezekana hilo tatizo limetatuka siku mbili zilizopita. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti kwanza ulivyosema ni sahihi lakini jengine nimwambie, nimetoa mfano hapa jamani mimi nimekwenda kwenye wodi ya wazazi nikaambiwa dawa fulani hakuna, tulipotizama kwenye bohari dawa zipo na nikasema kabisa kuna tatizo la *coordination* nimelisema hapa jamani, hilo ni tatizo la msingi kabisa Mhe. Hamza nakubaliana na wewe anaweza mtu mwingine kwa mfano, mwingine anataka kumtoa upepo tu akakwambia kitu fulani hakuna ili amtoe upepo. Hakuna malaika pale ndani lakini kwa upande wa serikali tumezihakiki kabisa katika maghala yetu yapo na ndiyo maana tumejenga hata ghala ndani ya hospitali ya Mnazimmoja isiwe sababu kwamba vitu viko mbali tunatizama kwenye ghala la Mnazimmoja pale je hakuna vipo. Kwa hivyo nasema yapo matatizo ya msingi kabisa ya binadamu yapo lakini nasema serikali kwa upande wake imejitahidi kuhakikisha kabisa vifaa vyote vipo na kukiwa na upungufu wowote twambieni tutatafuta, mimi mwenyewe nimeshudia unavyosema Mhe. Hamza nimepiga simu naambiwa huyu mgonjwa aliyewa ametafunwa na mbwa tukaambiwa kuna dawa hamna anatakiwa akanunue shilingi laki tatu na nusu, mimi na Mhe. Naibu Waziri tukapiga simu bohari hii dawa hamna tukaambiwa ipo lakini tumekwenda pale juu tukaambiwa haipo mimi mwenyewe binafsi, sasa hilo ni tatizo *communication* siyo kwamba kitu hakipo nakubaliana na wewe kabisa katika hilo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe.Hamza tunaendelea maana yake ushaongea mara tatu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, leo Mhe. Waziri aliitaja CCM hapa na sisi wengine hii CCM inatuuma kweli kweli, juzi tulipitisha kamati teule kuhusu majengo ya wizara ya elimu na tukapendekeza wizara ya afya na niliyataja nafikiri ukija ukiangalia katika kumbukumbu zako utaliingiza. Nadhani na hili la bohari na *supply* ya madawa nafikiri ukija ukikaa ukija sasa katika zile hadudi rejea utakazowapa Wajumbe tuliingize ili twende tukajiridhishe.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala halikubaliki kwa sababu kwanza Waziri mwenyewe kakiri huku hospitali anaambiwa hakuna lakini anapiga simu bohari anaambiwa zipo kule bohari wanasema tayari wameshaleta zinafikia wapi, au watu wanauza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. naomba tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa Mhe. Mwenyekiti nakubali tuendelee lakini naomba ulizingatie.

Kifungu H0201	Kitengo cha Uongozi na Utawala	712,417,000
Jumla kuu		**712,417,000**

Kifungu H02	Hospitali ya Mnazimmoja	14,802,000
Kifungu PH0201	Program kuu ya uchunguzi na matibabu	704,063,000

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe Waziri kwa uwazi wake ule aliosema hajawahi kushindwa kwenye serikali wala kwenye siasa na kuna muda alipoona mambo hayaendi vizuri kule kwenye chama cha CUF akatoka akaunda chake inaoneka mambo yake yanaenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu niliwahi kuchangia kwenye program hii nikazungumza suala la *Chemistry Analyzer* mashine ile lakini nikazungumza pia kwenye mtambo ule wa kuzalisha *oxgen* nikasema humu mnafanyika *sabotage* kubwa na ni vifaa muhimu. Sasa kwa sababu hajashindwa kazi, maana hata waziri aliyepita ulisema yote kakukabidhi lakini moja lile la tabia za hawa wafanyakazi ambao tulikuwa tunawazungumza kwenye bajeti yetu ilikushinda hata na yeye katika kufanya ziara yule hajasema tu lakini alimkuta mfanyakazi kaweka miguu juu ya meza hilo hajakwambia nafikiria, lakini sisi tunalijua. Sasa inawezekana ukamkuta huko juu ya meza kakaa kabisa, sasa nilikuwa nataka kauli ya serikali katika maeneo haya yote mawili kwa ubora wake. Lini Mhe. Waziri utakwenda kuyasimamia ili kadhia hii isiwepo. Nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nikubaliane kabisa kwenye *Chemistry Analyser* kulikuwa na tatizo na nimekutana na uongozi tumelizungumza nategemea tukimaliza shughuli hii hapa kwenda kulikabili hili jambo. Suala la *Oxgen* ule mtambo huu ni mkataba wetu pamoja na Orio na maktaba bado haujesha tumewambia kabisa wao watukabidhi mtambo ukiwa umekamilika, na kwa bahati mbaya walipofunga mtambo ulikuwa na matatizo kidogo walifunga chombo ambacho siyo sahihi kwa hivyo tumewambia warekebishe halafu ndiyo waweze kukabidhiwa rasmi. Kwa hivyo sisi hatujakabidhiwa rasmi na hata hiyo *oxgen* ambayo tukiwa tunakwenda kununua tunawa-*bill* wao kwa sababu bado hawajatukabidhi kwa hivyo nakubaliana nae kabisa tutakwenda kuyasimamia yote mawili kwa pamoja.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa nafasi nyengine, lakini na majibu ya Mhe. Waziri kwanza nayaunga mkono ni jitihada ya serikali. Lakini lipo tatizo katika majibu hili hujalijibu la uharibifu baadhi ya wafanyakazi wasiokuwa waaminifu. Unaonaje ukachukua jitihada ya kwenda kuweka CCTV Camera katika ule mtambo wetu wa uzalishaji *oxygen* nilikuwa nataka hiyo tu *commitment* yako ili bajeti ijayo kama yanatokea haya maana yake tujue tu kuna muarubaini mwengine tukushauri vizuri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mimi nimepokea ushauri wake Mheshimiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: tuendelee.

Kifungu PH0201	Program Kuu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu	704,063,000
Kifungu PH0202	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja	14,097,938,000
Jumla Kuu		**14,802,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Kifungu kilikuwa kimeshapita linahojiwa lile Fungu Kubwa ni jumla Kuu. Yaani lilikuwa limeshapitishwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Tumepitisha fungu ambalo linamalizia 01 lakini 02 ile PH.

Mhe. Mwenyekiti: Tulikwisha kulihoji Mheshimiwa likapigiwa kura likapitishwa, sasa hii ya mwisho ni jumla Kuu ya vifungu vyote viwili ndiyo tuliyoihiji mwisho itakuwa imekupita.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niwahoji wale wanaokubaliana na Hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwenye *order paper* yetu shughuli zimekamilika kwahiyo naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuruni sana kwa michango yenu kwenye Wizara hii. Pia niishukuru serikali kupitia Mhe. Waziri wa Afya kwa majumuisho yake, maana yake leo ilikuwa ni *lubricants* yale majumuisho, kwa michango yenu kwa namna mlivyoitoa nilitegemea shughuli hii ingeweza kutufikisha saa 9:00. Lakini yale majumuisho ambayo Mheshimiwa alikuja kuyatoa hapa yamekuwa kilainisho kizuri tu. Kwa hivyo nakupongezeni sana sana. *(Makofi)*

Baada ya hapo naomba sasa niakhirishe shughuli za Baraza mpaka kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8.21 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 6/6/2018 saa 3:00 za asubuhi)